**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA TANO**

**Kikao cha Nane – Tarehe 9 Novemba, 2006**

*(Mkutano ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**DUA**

*Spika (Mhe. Samuel J.Sitta) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAAM ISSA KHATIB):**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Bodi ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu kwa Mwaka 2005 *(The Annual Report and Accounts of the National Board of Accountants and Auditors for the Year 2005).*

Taarifa ya Mwaka ya Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana kwa Mwaka 2004/2005 (*The Annual Report of the Capital Markets and Securities Authority Tanzania for the Year 2004/2005).*

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 97

**HOSPITALI YA MKOA WA IRINGA**

**MHE. PINDI H. CHANA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi Ibara ya 66 ya Ilani hiyo, imeahidi kupunguza vifo vya watoto wa chini ya umri wa miaka mitano (5), vifo vya uzazi na kuongeza jitihada katika kupambana na magonjwa ya milipuko:

(a) Je, Serikali inafahamu kuwa Hospitali ya Mkoa wa Iringa ni ndogo na haikidhi idadi ya wagonjwa na katika Wodi ya watoto, watoto watatu (3) wanalala kitanda kimoja na kuambukizana magonjwa?

(b) Je, Serikali inafahamu kuwa kuna upungufu mkubwa sana wa Wauguzi katika Hospitali hiyo na nyi ngine za Serikali nchini?

(c) Je, Serikali ina mpango gani kushughulikia matatizo yaliyoelezwa kwenye sehemu (a) na (b) ya swali hili na kupanua au kujenga Hospitali nyingine ya Mkoa wa Iringa itakayokidhi idadi ya wagonjwa katika Mkoa wa Iringa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA :** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu Swali la Mheshimiwa Pindi H. Chana, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Hospitali ya Mkoa wa Iringa ina jumla ya vitanda 32. Wastani wa wagonjwa ni 40 – 45. Idadi ya wagonjwa kati wodi ya watoto yaani wodi namba 5 inaongezeka na kupungua kwa vipindi tofauti na wakati mwingine kulazimu watoto zaidi ya mmoja kulazwa kwenye kitanda kimoja. Hali hii husababishwa na Halmashauri za Iringa, Manispaa na Kilolo kutokuwa na Hospitali za Wilaya na ongezeko la watu katika Halmashauri hizo bila ongezeko la vitanda katika Hospitali ya Mkoa *(Makofi)*.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la kuambukizwa magonjwa, ni kwamba kabla mgonjwa hajapelekwa wodini kulazwa, uchunguzi wa kitaalam hufanywa na madaktari na hivyo mgonjwa hupelekwa wodini kwa kuzingatia aina ya ugonjwa anaoumwa kwa sababu kuna magonjwa yanayoambukizwa na yasioyoambukizwa.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inafahamu kuwa kuna upungufu mkubwa wa wauguzi katika Hospitali ya Mkoa wa Iringa. Hospitali ya Mkoa wa Iringa hivi sasa ina wauguzi 89 na wanatakiwa wauguzi 122, hivyo Serikali inatambua kwamba kuna upungufu wa wauguzi 33.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbali mbali ili kukabiliana na matatizo mbali mbali yanayozikabili hospitali zetu ikiwepo ya Hospitali ya Iringa. Kwa upande wa Mkoa wa Iringa Serikali imechukua hatua zifuatazo:-

(i) Kuomba eneo ambalo hivi sasa lina nyumba za watumishi wa Magereza ambalo lipo karibu na Hospitali ili nafasi hiyo itumike kupanua Hospitali na kuwezesha kuongeza idadi ya Wodi na Vitanda. Maombi haya yapo ngazi ya Wizara, kinachosubiriwa ni majibu ili kama itakubalika, upanuzi huu ufanyike.

(ii) Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Iringa inaendelea na utaratibu wa kuifanya Hospitali ya *Mission Ipamba* kuwa Hospitali Teule ya Wilaya.

(iii) Mheshimiwa Spika, katika kutatua tatizo la watumishi, Serikali imetoa kibali cha muda wa miaka mitatu kuajiri wataalam wa afya wakiwemo wauguzi kwa Wizara ya Afya na ustawi wa Jamii.

Vile vile Wizara sasa inawapangia Vituo vya kazi wataalam wa afya moja kwa moja mara wanapohitimu vyuoni. Mkoa wa Iringa unaendelea kupanga safari zenye fedha kila mwaka kulingana na bajeti inayopewa kwa ajili ya mishahara. Kwa mwaka huu wa fedha, Hospitali imetengewa nafasi za ajira 46 na kwa upande wa wauguzi nafasi 11.

Mheshimiwa Spika, lengo ni kujaza nafasi wazi kwa haraka ili kutoa huduma bora kwa wananchi.

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri. Kwa niaba ya watu wa Iringa, ningependa kujua yafuatayo:

Kwa kuwa Serikali imesema kwamba inatambua na kufahamu kwamba yapo mapungufu ya nafasi ya hospitali hiyo na ina mpango mahiri na madhubuti. Ni lini sasa Serikali inatarajia kuanza utekelezaji wa mpango huo wa kupanua Hospitali na ni kiasi gani *estimated budget* ambayo Serikali inadhani itatumia?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA :** Mheshimiwa Spika, kwa sasa, mpango wa Serikali ni kuhakikisha kwamba tunaimarisha Zahanati na Vituo vya Afya ili kupunguza msongomano katika Hospitali ya Mkoa na mipango ya baadaye kama ilivyosema kwamba, tukiisha kubaliwa kupewa eneo la Magereza, Serikali nitafanya makisio kwamba ni kiasi gani kinachotakiwa katika kupanua hospitali hiyo na pia inategemea na upatikanaji wa fedha. Namwomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira wakati Serikali ikiwa inafanya mipango yake ya kuimarisha Hospitali ya mkoa wa iringa.

**MHE. ROSEMARY K. KIRIGINI:** Mheshimiwa Spika, Ahsante kwa kuniona. Namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Kwa kuwa Waziri amekiri dhahiri kwamba kuna upungufu wa wauguzi, lakini kulikuwa na tabia ya wauguzi kupangiwa maeneo ya kazi lakini wanakuwa hawaripoti kwenye maeneo hayo na hatimaye husababisha upungufu mkubwa wa wauguzi hususan Mkoa wetu wa Mara ambao unaupungufu mkubwa wa wauguzi. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anatuambiaje wananchi wa Mkoa wa Mara ambao tuna upungufu mkubwa sana wa wauguzi katika hospitali zetu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA :** Ni kweli Serikali inatambua kwamba kuna upungufu mkubwa wa watumishi katika hospitali mbali mbali za Mikoa na Wilaya, ndio maana Serikali sasa hivi imeamua kwamba wale watumishi wanaotoka vyuoni, wanapangwa moja kwa moja katika Wilaya husika. Hapo zamani ilikuwa wakimaliza, wanakaa kwanza nyumbani, halafu nafasi zinatangazwa. Sasa ikitangazwa nafsi ya Mara na ikitangazwa nafsi ya Dar es salaam, mtu anakimbilia zaidi Dar es Salaam kuliko Mara.

Lakini kwa mpango wa sasa hivi wa kuwapangia moja kwa moja kwenye vituo husika, mimi nina hakika kwamba tatizo hili litapungua. Na vile mpango wa Serikali wa kuwasomesha wauguzi wengi na watumishi wengi wa afya, nafikiri baada ya miaka miwili/mitatu, tatizo hili litapungua.

**MHE. LUHAGA J. MPINA**: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii niweze kuuliza swali la nyongeza. Katika Semina Elekezi ya Afya, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alitoa wito kuwa wale wauguzi ambao walisoma Darasa la saba na kisha kwenda mafunzo ya mwaka mmoja na baadae kwa sababu waraka alibadilishwa, walioondolewa kazi, alitoa wito kwamba watu hawa warejeshwe kazini ili kutatua tatizo la wauguzi katika zahanati zetu. Kwa kuwa tatizo hili ni kubwa sana kule kwetu vijijini, na kwa kuwa wataalam hawatoshelezi, Je, ni lini Serikali sasa au ni lini Wizara sasa itatekeleza agizo hilo la Mheshimiwa Rais? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii! Naona sasa hili linaelekea kwenye taaluma yenyewe:

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana! Kuhusu kwamba Mheshimiwa Rais alisema kwamba wale manesi au wakunga waliokuwa wana elimu ya darasa la saba warudishwe kazi, Ukweli ni kwamba Mheshimiwa Rais alishauri kwamba wale wakumba ambao wameishia darasa la saba lakini wamepewa kozi za miaka mine au zaidi, watambulike kwamba wana utalaam na kwamba taluma yao siyo darasa la saba. Lakini naomba niirekebishe kwamba siyo kwamba walifukuzwa kazini, ila kwamba ameshauri tuwaajiri. Nilikuwa naomba kurekebisha hilo.

Kwa hiyo, ni kwamba Wizara ya Afya sasa inapanga utaratibu ili kuona kwamba wale darasa la saba ambao wana elimu au wamepata mafunzo ya Uuguzi au na fani mbali mbali wataajiriwa kama kawaida.

Na. 98

**Barabara ya Kutoka Kidatu - Taweta**

**MHE.CASTOR R. LIGALLAMA** aliuliza:-

Kwa kuwa barabara kutoka Kidatu – Ifakara – Namwawala – Mbingu – Mchome – Chita – Mpanda hadi Taweta ni barabara muhimu kwa Uchumi wa Wilaya ya kilombero; Na kwa kuwa sehemu kubwa ya barabara hiyo huwa mbaya sana wakati wa masika hasa kipande cha kutoka Ifakara kwenda Taweta. Serikali kwa kuthamini mchango mkubwa unaotolewa na wananchi wa eneo hilo katika uchumi wa taifa; na kwa kuzingatia kuwa barabara hufuata bidhaa; Je, itakubali kuiingiza barabara hiyo katika barabara za kitaifa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la mheshimiwa Castor R. Ligallama, Mbunge wa Kilombero, kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali inathamini mchAngo mkubwa wa wananchi wa Kilombero katika uchumi wa taifa na kuwa iko pamoja nao katika kuhakikisha uchumi unakua na muindombinu inaendlezwa ili kuwafikia wananchi kwa urahisi na wao kusafirisha bidhaa zao bila kukwama. Barabara anayoizungumzia Mheshimiwa Mbunge ni barabara tofauti ambazo ni barabara ya Kidatu – Ifakara na Ifakara – Taweta. Kidatu – Ifakara ni sehemu ya barabara kuu, wakati barabara ya ifakara – taweta ni barabara ya Mkoa ambazo zote n I za kitaifa na huhudumiwa na Wakala wa Barabara nchini *(TANROADS)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia mchango wa uchumi wa wakazi wa Wilaya ya kilo,mbero, Serikali kupitia Wakala wa barabara imefanya na inaendelea kufanya Matengenezo yafuatayo:-Mheshimiwa Spika, bnarabara ya kidatu – ifakara yenye urefu wa kilometa 75, kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2005/2006 kulikuwa na mradi mkubwa uliogharimu kiasi cha shilingi bilioni 1.6 ambazo zilitumika kufanyia kukarabati barabara hiyo na kuhusisha matengenezo ya :-

▪ Kuweka changarawe na kushindilia;

▪ Kuweka lami nyepesi sehemu korofi kipande chenye urefu wa kilometa 10 ambacho kilianzia Kiberege – Siginali;

▪ Kujenga makaravati; na

▪ Kujenga mifereji.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya barabara hii kipande cha Kibaoni – Ifakara chenye urefu wa Kilameta saba ipo chini ya mpango wa kujengwa kwa kiwango cha lami ambapo mtaalam mshauri ameshateuliwa kwa ajili ya usanifu. Katika Bajeti ya mwaka 2006/2007 matengenezo yafuatayo yatafanyika ili kudumisha barabara hiyo:-

- Matengenezo ya muda maalum yatakayogharimu Shilingi milioni 57.4;
- Matengenezo ya sehemu korofi, Shilingi milioni 26.04;
- Matengenezo ya kawaida, Shilingi milioni 108.75;
- Matengenezo ya madaraja, Shilingi milioni 64; na
- Vile vile kuna ujenzi wa madaraja ya kudumu mawili katika vivuko vya Mto kiberege na Sagamaganga.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Ifakara – Taweta ina urefu wa Kilometa 207 ambapo kilometa 25 ni za lami, eneo la Kihansi – Mlimba, Kilometa 150 ni za changarawe na kilometa 32 ni za udongo. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2006/2007 matengenezo yafuatayo yamepangwa kufanyika katika Kilometa 175 (Ifakara – Utengele) ambazo hupitika:-

- Matengenezo ya muda maalum, Shilingi milioni 51.6;
- Matengenezo ya sehemu korofi, Shilingi milioni 52; na
- Matengenezo ya kawaida, Shilingi milioni 85.02.

Mheshimiwa Spika, kwa kilometa 32 (Utengule – Taweta) ambazo ni za udongo hazipitiki wakati wa mvua. Matengenezo yatakayogharimu kiasi cha Shilingi milioni 82 yamepangwa kufanyika ili kipande hicho cha barabara kiweze kupitika kwa kipindi cha mwaka mzima. Kazi zifuatazo zimeshakamilika:-

- Kufungua barabara kwa *bulldozer* ambapo Kilometa nane zimekamilika;
- Kuunda na kushindilia barabara kilometa 16 zimekamilika; na
- Makalvati ya zege yameshatengenzwa na baadaye yatapelekwa eneo la ujenzi kadri kazi zinavyoendelea.

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza. La kwanza ni kueleza umuhimu wa barabara hii. Barabara hii ni kama vile mshipa wa damu wa Wilaya yetu kama Aota kiuchumi kwa sababu inapitiwa na Kata 17 kati ya Kata 19 za Wilaya ya Kilombero. Kwa hiyo, naomba nimwulize Naibu Waziri kwamba, tayari barabara hii katika Awamu ya Kwanza kipindi cha Serikali ya Awamu ya Tatu, yamejengwa madaraja zaidi ya 40, madaraja ya kudumu, mazuri yenye gharama za mabilioni. Je, kwa nini Serikali haiwezi kwenda tena kuongea nao ili waanze kazi ya kukamilisha ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami ambayo ndiyo ilikuwa madhumuni yao kwamba awamu ya pili wajenge kwa lami baada ya kumaliza madaraja?

Swali la pili, barabara hiyo imepita kwenye mashamba makubwa, mashamba ya Gereza la Kiberege, Mashamba ya Gereza la Idete, Shamba la Lwipa, Shamba la *COTACO* – Mgeta, Shamba la Chita *JKT* ambayo yote hayo tunayatafutia wawekezaji. Ili kuwavutia wawekezaji, miundombinu ya barabara ikiimarishwa, hatuoni kwamba Serikali yetu itakuwa imetekeleza Ilani ya Uchaguzi ya kusema kwamba Serikali itatafuta wawekezaji kwenye mashamba makubwa ili kuboresha maisha ya wananchi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Serikali inatambua kwamba barabara hii ni muhimu sana na kweli inapita katika Kata 16 na mimi ni mmojawapo kati ya watu waliotembelea barabara hii na nafahamu kiuchumi inasaidia sana katika Taifa letu. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali ndio maana inapanga fedha kila mwaka ili kuhakikisha kwamba barabara hii inapitika. Kwa kweli kwa kufikia kiwango cha lami, Serikali mpaka sasa hivi haina mpango huo. Ila nimhakikishie tu kwamba barabara hii itaimarishwa mwaka hadi mwaka ili iweze kupitika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu madaraja ambayo yalijengwa na Swiss, kwa kweli niwashukuru sana ndugu zangu wa Swiss kwa msaada mzuri waliotufanyia katika kujenga madaraja hayo ambayo ni imara sana. Sasa kuhusu kurudi tena kwenda kwa mfadhili na kuomba, huo ni mpango mwingine na mambo mengine tofauti. Naomba

nipokee ombi hilo na tukishirikiana na Wizara ya Miundombinu kuhakikisha kwamba twende tukaombe tena msaada kama huu. Kama watatukubalia, itakuwa ni vizuri, wasipotukubalia tutatafuta mbinu nyingine.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake la pili, nafahamu kabisa kwamba barabara hii imepita kwenye mashamba makubwa ambayo wakulima wanalima mazao yao. Hilo linafahamika na kama nilivyosema hapo mwanzoni, kuimarisha barabara hizi ni ili kuwavutia wawekezaji na pia ziweze kupitika kwa urahisi. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tushirikiane kuhakikisha kwamba barabara hii inapitika angalau kwa mwaka mzima na sisi Serikali tutapanga fedha mwaka hadi mwaka katika kuimarisha barabara hiyo.

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Eneo hili linalozungumzwa hapa, yaani Taweta na Tanganyika linapakana na Jimbo la Njombe na Jimbo langu. Wakati wa masika, watu wa Tanganyika na Taweta mahitaji yao hutegemea Wilaya ya Njombe – Jimbo langu. Kwa kuwa hivi sasa trekta liko Taweta na eneo kutoka Mlimba mpaka Taweta ni *Regional Road*, kutoka Njombe mpaka Lupembe karibu na mpaka ni *Regional Road*, ila sehemu ndogo tu ambayo iko chini ya *nowhere:* Je, kwa nini Waziri asitumie nafasi hii wakati trekta liko pale kukamilisha ile sehemu wakati huu mvua hazipo ili angalau wakati wa kiangazi watu hawa waweze kwenda Njombe kwa urahisi kuchukua mahitaji yao muhimu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu! Ingawa sina hakika kilichopo pale trekta au ni greda, lakini majibu Mheshimiwa. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli barabara hiyo ya Njombe – Lupembe pamoja na barabara za Ifakara na watu hao wanapata huduma aidha upande wa Wilaya ya Kilombero au upande wa Wilaya ya Njombe. Naomba Mheshimiwa Mbunge nilipokee ombi lake na tulifanyie kazi. Kwa sasa siwezi nikatoa majibu ya haraka haraka. *(Makofi)*

Na. 99

**Upungufu wa Mahakama za Mwanzo**

**MHE. MGANA I. MSINDAI** aliuliza:-

Kwa kuwa kuna tatizo la upungufu wa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo na kwa Mahakama zenye Mahakimu hukaa eneo moja kwa muda mrefu hali inayosababisha kutawaliwa na mazingira ya eneo husika na wengine kusahau au kuanza kutumia madaraka yao vibaya na kwa kuwa Mahakimu hawana nyenzo za usafiri wa kuwawezesha kufika kwenye maeneo yao kirahisi:-

(a) Je, Serikali inasemaje juu ya upungufu wa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo hizo na lini itatatua tatizo hilo?

(b) Je, ni lini Serikali italeta Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo Kirumi ili kumrahisishia kazi Hakimu anayetoka Ibaga kwenda Kirumi kutekeleza majukumu yake bila usafiri wa uhakika?

(c) Je, ni lini Serikali italeta Mahakimu kwa Mahakama za Mwanzo za Iyambi na Kinyangiri ambako majengo yapo?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mgana I. Msindai, Mbunge wa Iramba Mashariki, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuna Mahakama za Mwanzo 1,105 nchi nzima wakati idadi ya Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo ni 713. Takwimu hizi zinaonyesha kuwa kuna upungufu wa Mahakimu 392 wa Mahakama za Mwanzo.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na upungufu huo, Serikali inafanya mikakati ifuatayo:-

(i) Serikali inaendeleza jitihada za kupanua Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto ili kuongeza idadi ya wahitimu ambao watakuwa na sifa za kuwa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo.

(ii) Serikali inaajiri Wahitimu wenye sifa kutoka Vyuo vingine vinavyotambulika na Serikali kuwa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo katika mwaka huu wa fedha Mahakimu 100 wa Mahakama za mwanzo wataajiriwa.

(iii) Kuajiri kwa Mkataba Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo Wastaafu wenye sifa nzuri za utendaji na nidhamu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na upungufu huo uliopo wa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo, inalazimika baadhi ya Mahakimu kupangiwa vituo vya kutembelea. Ili kukabiliana na adha ya usafiri, Serikali imeandaa mpango wa kuwakopesha Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo pikipiki. Ni Sera ya Mahakama kuwahamisha Mahakimu waliokaa muda mrefu kwenye kituo kimoja kwenda vituo vingine. Inawezekana kabisa kwamba wapo Mahakimu ambao wamekaa katika Kituo kimoja kwa muda mrefu, lakini hii sio sera ya Mahakama. Naomba Mheshimiwa Mbunge ashirikiane na Wizara yangu kurekebisha dosari hiyo.Kwa kuwa uhaba wa Mahakimu wa Mahakama ya Mwanzo ni 392 nchi nzima, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali itafanya kila iwezalo ili kuhakikisha kuwa Mahakama za Mwanzo zote ambazo zina majengo zikiwepo zile za Kinyangiri na Iyambi, zitapatiwa Mahakimu kadri watakavyokuwa wanahitimu na kuajiriwa. *(Makofi)*

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Kwa kuwa Mahakama ni mhimili

mmojawapo wa dola na kwa kuwa pamoja na maeneo yote yaliyozungumzwa katika swali la msingi na majibu yote ya Naibu Waziri yameonyesha dhahiri kwamba mhimili huu umelala usingizi, maana kesi nyingi zinazoamuliwa na zenye matatizo makubwa ni zile zilizoko Vijijini ambako Mahakama hazitoshelezi, Mahakimu hawatoshelezi: Je, mhimili huu sasa una mpango gani mahsusi mbali na yanayotendeka sasa ya kesi nyingi kuamuliwa na Mabaraza ya Usuluhishi ambayo yanaleta manyanyaso na maonezi makubwa hasa kwa akina mama, katika kuchukua hatua za msingi kumaliza tatizo la kupelekea Mahakimu ili waweze ku-*cover* hizo nafasi za kesi zinazoamuliwa bila kufuata sheria?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, mhimili wa Mahakama kweli ni mmojawapo wa mihimili mitatu ya dola, lakini sio kweli kusema kwamba umelala usingizi. Tunao upungufu wa wafanyakazi katika mihimili yote mitatu na huu ni mmojawapo. Ni upungufu wa kawaida wa wanyakazi katika mihimili yote mitatu. Lakini kama nilivyosema, tunakusudia kuajiri Mahakimu 100 mwaka huu wa fedha na utaratibu huu utaendelea mpaka Mahakama zote za Mwanzo na za Wilaya zitakapokuwa na Mahakimu wa kutosha.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria kwa majibu mazuri sana ya nyongeza kwa swali la Mheshimiwa George Simbachawene. Ni kweli kabisa Mahakama ni mhimili na pasipo Mahakama kufanya kazi vizuri, basi na haki nayo inatetereka ndani ya nchi. Kwa hiyo, nakubaliana na Waheshimiwa Wabunge kwamba kuna umuhimu wa kuongeza Mahakama na Mahakimu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jibu alilotoa Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba tutaongeza Mahakimu, basi napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge na Watanzania kwamba kupitia maboresho ya Sekta ya Sheria, moja ya eneo ambalo linapewa umuhimu ni kuongeza Mahakama na Mahakimu. *(Makofi)*

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili niulize swali dogo la nyongeza kuhusiana na Wizara hii ya Sheria.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yao. Lakini pamoja na hali ilivyoelezewa ya Ukosefu wa upungufu wa Mahakimu katika Mahakama za Mwanzo, pamoja na hawa Mahakimu wachache waliopo katika Mahakama hizi za Mwanzo. Mahakimu hawa wamekuwa wakifanya kazi katika mazingira magumu sana. Kwa mfano, Hakimu anayefanya kazi ya kusikiliza kesi katika Tarafa ya Ndago, ndiye Hakimu yule yule anayekwenda katika Mahakama ya Mwanzo ya Kaselya na anayekwenda Mahakama ya mwanzo na Ulugu, kote kuna umbali na hana usafiri. Lakini wamekuwa wakitumia usafiri wa wale wale watu wanaowashitaki, usafiri ule ule mmoja jambo ambalo ni hatari sana. Je, Wizara iko tayari kuwapatia japo hawa Mahakimu wachache wa Mahakama za Mwanzo japo usafiri tu ili kuweza kuepuka matatizo yanayojitokeza pale wanapofanya uamuzi katika kesi zao?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli wafanyakazi wengi wa Serikali wana matatizo ya usafiri. Hii ni kwa Walimu, Mabwana Shamba na pia ipo kwa Mahakimu. Kwa upande wa Mahakimu, Wizara yangu inaanzisha mpango wa kuwakopesha pikipiki ili waweze kupunguza tatizo hili la usafiri. Kwa kweli tutajitahidi kwa wale ambao wanatambelea Mahakama mbalimbali wapate usafiri kwanza kabla ya hawa ambao wako kwenye vituo kama *permanent*. Kwa hiyo, swali la Mheshimiwa Mbunge tunalichukua na tutalifanyia kazi kwa utaratibu huo. *(Makofi)*

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kunipa nafasi hii, ili niweze kuuliza swali kuhusiananа Wizara ya Sheria. Katika majibu yake ya msingi namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, pamoja na Mheshimiwa Waziri kwa majibu yao. Lakini pamoja na hali ilivyoelezewa ya ukosefu na upungufu wa Mahakimu katika Mahakama za Mwanzo. Pamoja na hao Mahakimu wachache waliopo katika hizi Mahakama za Mwanzo, Mahakimu hawa wamekuwa wakifanyakazi kwa mazingira magumu sana. Kwa mfano Hakimu anayefanyakazi ya kusikiliza ya kusikiliza kesi katika Tarafa ya Ndago ndiyo Hakimu yule yule anayekwenda katika Mahakama ya Mwanzo ya Kaselia na anakwenda Mahakama ya Mwanzo Urugu, kote kuna umbali na hana usafiri. Lakini wamekuwa wakitumia usafiri kwa wale wale watu wanaowashitaki usafiri ule ule mmoja jambo ambalo ni hatari sana. Je, Wizara ipo tayari kuwapatia japo hawa Mahakimu wachache wa Mahakama za Mwanzo, japo usafiri tu ili kuweza kuepukana na matatizo yanayoweze kujitokeza pale wanapofanya uamuzi katika kesi zao? Ahsante. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Killimbah kama ifuatavyo:-

Ni kweli wafanyakazi wengi wa Serikali wana matatizo ya usafiri, hii ni kwa walimu, Bwana Shamba na pia iko kwa Mahakimu. Kwa upande wa Mahakimu Wizara yangu imeanzisha mpango wa kuwakopesha Mahakimu hawa pikipiki, ili waweze kupunguza tatizo hili la usafiri. Kwa kweli tutajitahidi kwa wale ambao wanasafiri wanatembelea Mahakama mbalimbali wapate usafiri kwanza kabla ya hawa ambao wako kwenye vituo ambao wako *permanent*. Kwa hiyo, swali la Mheshimiwa Mbunge, tunalichukua na tutalifanyia kazi kwa utaratibu huo. (*Makofi*)

Na. 100

**Mtoto wa Kike Kuolewa Kabla ya Miaka 18**

**MHE. SUZAN A. J. LYIMO (MHE. LUCY OWENYA)** aliuliza:-

Kwa kuwa Tanzania imejiwekea malengo ya kuinua hali ya maisha kwa Watanzania wote wakiwemo wanawake; na kwa kuwa elimu bora ni njia mojawapo ya kumkomboa mwanamke na kumwondolea umaskini.

Je, Serikali ina mkakati gani na Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 inayohusu mtoto wa kike kuolewa kabla ya miaka 18 ambayo inamuathiri kisaikolojia ikiwa ni pamoja na kumkosesha nafasi ya kupata elimu bora na ya kutosha?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Lucy Owenya, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo: Ninakubaliana naye kuwa Tanzania imejiwekea malengo ya kuinua hali ya maisha kwa Watanzania wote wakiwemo wanawake na kuwa elimu bora ni njia mojawapo ya kumkomboa mwanamke na kuondokana na umaskini kama ilivyoainishwa kwenye Sera ya Elimu ya Mwaka 1995, MKUKUTA, Malengo ya *Millenia* na Azimio na Ulingo wa *Beijing*, ambayo husisitiza juu ya Maendeleo ya Mtoto wa kike pamoja na mengine.

Mheshimiwa Spika, sote tunajua kwamba kuozesha mtoto wa kike chini ya miaka 18 ni ukiukwaji wa haki za binadamu kwa sababu viungo vya mtoto vya uzazi vinakuwa bado havijakomaa. Mtoto wa namna hii anapopata mimba hushindwa kujifungua na huweza kuwa kilema, kufariki au kupata msongo wa mawazo. Vile vile endapo atajifungua salama basi hushindwa kumlea mtoto wake. Mtoto wa namna hii hukatishwa masomo na kuendelea kuwa mjinga na maskini.

Mheshimiwa Spika, Tanzania imesaini na kuridhia matamko, maamizio na itifaki mbalimbali za kikanda na kimataifa yanayolinda haki za wanawake wakiwemo watoto wa kike ambazo zinabainisha umri wa kuolewa mtoto wa kike kuwa ni miaka 18.

Aidha, Sera ya Maendeleo ya Mtoto ya Mwaka 1996 imebainisha mtoto kuwa ni yule aliye chini ya miaka 18. Hata hivyo, Sheria ya Ndoa ya Tanzania ya mwaka 1971 inabainisha umri wa kuolewa mtoto kuwa ni miaka 15 ambayo kufuatana na Sera ya Maendeleo ya Mtoto na sababu za kibaolojia anakuwa bado ni mtoto. Kwa kutambua hili Serikali inaendelea na mchakato wa kurejea sheria hii, ili Muswada uweze kuandaliwa na kuletwa Bungeni kwa ajili ya kuridhiwa kuwa sheria.

Mojawapo ya vipengele vitavyoangaliwa kwa makini ni kifungu kinachohusu umri wa kuolewa kwa mtoto wa kike.

Na. 101

**Barabara ya Mtukula – Lusahunga**

**MHE. PHARES K. KABUYE** aliuliza:-

Kwa kuwa, mwanzoni watu wa Mkoa wa Kagera walianza kufurahia ujenzi wa Barabara ya Mtukula – Kagoma – Lusahunga kwa kiwango cha lami lakini kwa zaidi ya mwaka mmoja imekwama kabla ya kufika Lusahunga:-

Je, ni lini barabara hiyo itaendelea kujengwa na kufika Lusahunga kama ilivyokuwa imepangwa na ni lini pia barabara ya kutoka Kalebezo hadi Bwanga itaanza kujengwa?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Phares Kashemeza Kabuye, Mbunge wa Biharamulo Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki zimepanga kutekeleza miradi ya barabara katika kanda tano na mradi huu ni mmojawapo wa miradi iliyokubalika kutekelezwa chini ya mradi wa mtandao wa Barabara za Afrika Mashariki. Barabara hiyo yenye urefu wa jumla ya kilometa 290 imepangwa kujengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mradi huu ulipangwa kutekelezwa kama ifuatavyo:-

(i) Barabara ya Mtukula – Muhutwe (km.112), sehemu hii ya barabara imejengwa kwa mkopo toka Benki ya Maendeleo ya Afrika, pamoja na Serikali ya Tanzania na imekamilika na kufunguliwa rasmi mwezi Novemba, 2004.

(ii) Barabara ya kutoka Muhutwe – Kagoma (km 24) sehemu hii ya barabara imejengwa kwa mkopo toka Mfuko wa Maendeleo ya nchi zinazotoa mafuta kwa wingi dunia (*OPEC*) pamoja na Serikali ya Tanzania. Ujenzi umekamilika na barabara imefunguliwa rasmi mwezi Novemba, 2004. *(Makofi)*

(iii) Barabara ya Kagoma – Lusahunga (km. 154) mkataba wa ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami umesainiwa tarehe 13 machi, 2006 kati ya Serikali ya Tanzania na Kampuni ya *China State Construction Engineering Corporation* kutoka China. Muda wa utekelezaji wa mkataba huo ni miezi 39. Kwa wakati huu, mkandarasi, ameshakamilisha kazi za maandalizi ya awali zikiwemo za kuleta vifaa na mitambo eneo la kazi, ujenzi wa kambi na kazi za ujenzi wa barabara zimeanza. Kampuni inayohusika na usimamizi wa kazi hizo ni *International Consultant and Technocrats Pvt. Ltd.* kutoka India. Mradi umefadhiliwa kwa pamoja kati ya Serikali ya Tanzania na Benki ya Maendeleo ya Afrika.

Mheshimiwa Spika, barabara ya kutoka Kalebezo hadi Bwanga, ni sehemu ya barabara kuu ya Mwanza – Geita- Bwanga hadi Biharamulo. Kama ilivyokuwa kwa barabara zingine kuu katika ukanda wa ziwa, barabara hii yenye urefu wa kilometa 69 imo katika mpango wa kujengwa kwa kiwango cha lami. Kwa wakati huu kampuni ya kizalendo ya *Data Consult Ltd.* inakamilisha kazi ya kuifanyia usanifu wa kina barabara hii. Kukamilika kwa kazi hiyo, ndiko kutatuwezesha kubaini gharama halisi za ujenzi na hivyo kuanza mikakati ya kutafuta fedha hizo.

Na. 102

**Uwekaji wa Minara ya Simu Maeneo ya Zanzibar**

**MHE. ASHA M. JECHA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, imefikisha miundombinu ya barabara, maji na umeme katika maeneo mbalimbali ya vijijini kama vile Koani, Machui, Kidimuni, Kiboje, Uzini, Mpapa na kadhalika; na kwa kuwa ofisi za sekta mbalimbali zipo katika maeneo hayo kama vile Makao Makuu ya CCM na Serikali ya Mkoani Unguja, Kambi ya Jeshi Ubago na Dunga, Vituo vya Polisi Mwera, Machui na Dunga, Kambi ya J.K.U. Machui na Bambi na kwa kuwa mawasiliano ya simu za mkononi ni nyenzo muhimu ya kuwasilisha kwa haraka, nyenzo ambayo kwa sasa haipatikani kwa urahisi kutokana na kutokuwepo kwa minara ya simu katika maeneo hayo:-

Je, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, haioni kuwa sasa ni wakati muafaka wa kuchukua hatua za makusudi kuzishawishi kampuni za simu kujenga minara ya simu katika maeneo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Asha M. Jecha, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Serikali inatambua mchango unaotolewa na makampuni ya simu nchini ambao huwanufaisha watumiaji na kuwawezesha kuwasiliana na hivyo kurahisisha huduma za kijamii na kiuchumi kwa wananchi. Serikali inaipongeza Kampuni ya Simu ya *Zantel* kwa kueneza mtandao wa simu katika Visiwa vya Pemba na Unguja kwa zaidi ya asilimia 85. Maeneo yaliyotajwa na Mheshimiwa Mbunge, ni baadhi ya maeneo machache ambayo bado hayajafikiwa au yana mawasiliano hafifu. Hata hivyo, Serikali kupitia Mamlaka husika ya mawasiliano inaendelea kuyashawishi makampuni yanayotoa huduma hizo kuendelea kupanua uwigo wa shughuli zao ili ziweze kuwafikia wananchi wengi zaidi.

Katika kuzingatia suala hilo Kampuni ya *Celtel* inategemea kuanza kutoa huduma zake katika maeneo ya Mwera mwanzoni mwa mwaka 2007. Maeneo mengine ya Koani, Machui, Kidimuni, Kiboje, Uzini, Mpapa, Ubago, Dunga na Bambi yanafanyiwa utafiti wa masoko utakaofuatiwa na utoaji wa huduma katika kipindi cha mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya *TIGO* ina mpango wa kujenga mnara eneo la Bambi kabla ya mwezi Machi 2007. Mnara huu utawezesha kampuni hiyo kutoa huduma katika maeneo ya Koani, Machui, Kidimuni, Uzini, Mpapa, Ubago, Dunga, Mwera na Bambi bila ya matatizo. Kwa upande mwingine huduma za Kampuni ya *Vodacom* zitaweza kuwafikia wananchi waishio maeneo ya Ubago, Mwera, Kidimuni na Mpapa pindi tu ujenzi wa mnara wa mawasiliano wa Masingini utakapomalizika.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wateja wa simu hizi za mikononi wamekuwa wengi katika maeneo mbalimbali, hivi ni kiwango gani hasa cha wateja wanapotimia wanastahili kujengewa mnara karibu yao? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge ameuliza swali kwamba ni wateja kiasi gani inatakiwa wafikie ili kujengewa mnara. Napenda kujibu swali hilo ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Makampuni ya Simu, hufanya tathimini za kiuchumi na kibiashara katika kuweka minara hiyo. Lakini kama ambavyo Serikali imekuwa ikiwasisitizia kwamba ni nia ya Serikali wananchi wote bila kujali biashara au uchumi wao waweze kufikiwa na huduma ya simu na ndiyo maana tumekuwa tunawahimiza na wao wamekuwa wakiweka minara na kueneza huduma za simu katika maeneo mbalimbali.

Pale ambapo kuna matatizo ya wananchi kuwa maskini sana ndiyo maana Sheria ambayo itaanza kuzungumzwa leo Bungeni itawezesha huduma za simu na mitandao mingine ya mawasiliano kuwafikia maeneo mengine ambapo uwezo ni mdogo.

Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge, Khalifa na Waheshimiwa Wabunge, wote waelewe kwamba nia ya Serikali na Makampuni haya ni kujaribu kueneza huduma za simu nchi nzima. (*Makofi*)

Na. 103

**Kuwajali Askari wa Vita vya Idd Amin**

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA** aliuliza:-

Kwa kuwa wakati wa vita kati ya Uganda na Tanzania, wakati wa utawala wa Idd Amin Askari wengi walipoteza maisha yao na kwa kuwa askari wengi walistaafishwa wakiwa hai lakini wakiwa na ulemavu. Je, askari hao ambao sasa hawawezi kufanyakazi nyingine, Serikali inawaangalia kwa mfumo gani wa mapato?

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Yahya Kassimu Issa, Mbunge wa Jimbo la Chwaka, kwanza napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, mnamo mwaka 1978 nchi yetu ilivamiwa na Majeshi ya Uganda. Kutokana na uvamizi huo, Amiri Jeshi Mkuu wa Tanzania, alilazimika kutangaza vita dhidi ya Majeshi ya Uganda. Vita hivyo vililenga katika kuilinda nchi yetu na siyo vinginevyo. Hata hivyo vita dhidi ya Majeshi ya Uganda vilisababisha baadhi ya Wanajeshi wetu kuumia na wengine kupoteza maisha.

Kwa wale walioumia, walifanyiwa uchunguzi wa afya zao. Baadhi yao walionekana kutoweza kumudu kazi za kijeshi. Walioshindwa kumudu kazi za kijeshi walistaafishwa kwa mujibu wa sheria na taratibu za kijeshi na wale walioonekana kuweza kumudu kazi nyingine, waliajiriwa jeshini kama raia. Wote waliostaafishwa Jeshi, walilipwa haki zao kulingana na kiwango cha ulemavu walioupata.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Yahya Kassim Issa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hakuna utaratibu ulioandaliwa wa kumsaidia kimapato mwanajeshi aliyepata ulemavu vitani. Mwanajeshi aliyepata ulemavu wakati akiwa vitani, Serikali inamsaidia kumlipia matibabu pale anapojisikia kuumwa kutokana na athari za vita.

Mbali na msaada huo wa matibabu, pia hulipwa posho ya kujikimu kwa siku anazokuwepo kwenye matibabu, ikiwa matibabu hayo yanayohitajika yanapatikana nje ya Mkoa anaoishi.

Aidha, kwa kuzingatia sera ya watu wenye ulemavu pamoja na huduma zinazotolewa kwa watu wenye ulemavu kupitia ustawi wa jamii, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, italiangalia zaidi suala hili katika juhudi za kuona ni jinsi gani, Wizara inaweza kuwasaidia zaidi wanajeshi waliopata ulemavu kutokana na vita. Nawaomba wale wote waliopata ulemavu waendelee kuwa na subira.

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa watu hawa waliopata ulemavu waliweka historia ya nchi yetu na kwa kuwa watu hawa hivi sasa wana jamii inayowategemea katika maisha yao.

(a) Je, Serikali, haioni kwamba ifanye utaratibu maalum ili kuwapatia fedha kwa kila mwezi ili kujikimu maisha yao? (*Makofi*)

(b) Je, uongozi wa jeshi umewahi kuwapitia watu hawa na kuwafariji kutokana na matatizo yaliyowapata na kama imewapitia wanajeshi wangapi walipata ulemavu katika vita? (*Makofi*)

**SPIKA:** Hilo la mwisho la wangapi nadhani linahitaji takwimu. Lakini yale mawili mengine Mheshimiwa Naibu Waziri unaweza kuyajibu.

**NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza awali Wizara yangu inaipitia sera ya watu wenye ulemavu kuona katika sera ile ni maeneo gani watu wenye ulemavu wanaweza wakasaidiwa. Kadhalika, tunaangalia huduma wanazozipata watu wenye ulemavu kupitia ustawi wa jamii.

Tutakapokamilisha na sisi kama Wizara tunaandaa utaratibu wa kuweza kuwasaidia zaidi hawa wanajeshi waliopata ulemavu. Swali lake la pili kuhusu kuwapitia hawa wanajeshi waliopata ulemavu nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba mimi mwenyewe pamoja na Mheshimiwa Waziri, tumewapitia wanajeshi waliopata ulemavu na tumewasikiliza malalamiko yao na vilio vyao na ndiyo maana tunaangalia utaratibu wa kuweza kuwasaidia zaidi.

Kuhusu takwimu wanajeshi wote waliopata ulemavu kutokana na Vita vya Kagera walikuwa ni 804. (*Makofi*)

**MHE. ZUBEIR ALI MAULID:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kuwa huu ulemavu walioupata askari hawa ni tofauti sana na ulemavu ambao watu wameupata katika mazingira ya ajali za barabarani. Huu ni ulemavu ambao umepatikana watu wakiitetea nchi. Sasa Serikali haiwezi kuweka mpango wa makusudi kabisa kwa sababu baadhi ya askari hawa hata mwenyewe Mheshimiwa Naibu Waziri, ni shahidi kwa sababu ndani ya jimbo langu ninao na amekwisha kutembelea watu hao na nilikuwa naye tulipokuwa tukiwatembelea watu hao na nilikuwa naye tulipokuwa tukiwakagua. *(Makofi)*

Je, Serikali haioni kuwa kuweka utaratibu maalum wa makusudi bila ya kujali kwamba kuna huo mpango wa kuwahudumia walemavu kupitia katika maeneo mengine, lakini nikaweka mpango wa makusudi wa kuwahudumia kwa sababu hali za watu hawa si nzuri hata kidogo ni mbaya wanategemewa na watu, lakini ulemavu walioupata hawawezi hata kujihudumia wenyewe nafsi zao. Serikali iweke mpango wa makusudi wa kuwahudumia. Je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana nami kwenye hili? (*Makofi*)

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, Serikali imetambua vilio na kauli za Waheshimiwa za Wabunge kuhusu suala hili la askadri waliopata ulemavu. Tunapenda kuliahidi Bunge lako Tukufu kwamba Wizara inayohusika italitafakari na kuleta maelezo juu ya hatua zake wakati wa Bajeti. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kumaliza utata kwenye hilo. Sasa tunahamia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Na. 104

**Serikali Kuwasaidia Wanafunzi wanaomaliza Darasa la Saba**

**MHE. AMINA C. MPAKANJIA** aliuliza:-

Kwa kuwa zamani wanafunzi waliomaliza darasa la saba, lakini hawakubahatika kuchaguliwa kwenda sekondari walikuwa wakipelekwa kusomea fani mbalimbali kama vile ufundi na ualimu na hivyo kundi kubwa la vijana waliomaliza darasa la saba, kuweza kujiendeleza na kujiajiri au kuajiriwa tofauti na hali ilivyo sasa ambapo vijana wengi

huishia mitaani pindi wanapomaliza darasa la saba na kukosa nafasi za kuendelea na masomo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kufufua mpango huo ili kuwasaidia vijana wanaomaliza darasa la saba?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Amina Chifupa Mpakanjia, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Wizara ya Elimu na Mafunzo wa Ufundi, kwa kupitia Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES), inatarajia wanafunzi zaidi ya asilimia 50 ya wahitimu wa darasa la saba kujiunga na Elimu ya Sekondari ifikapo mwaka 2009. Sehemu kubwa ya wanaobaki watapata mafunzo ya ufundi staidi kupitia mpango wa upanuzi wa vyuo vya Ufundi unaoandaliwa. (*Makofi*)

Kwa hivi sasa, kuna vituo vya mafunzo vya ufundi stadi vipatavyo 819 nchini, vyenye uwezo wa kuchukua jumla ya wanafunzi 100,653 kwa mwaka. Kati ya hao ni asilimia 75 ni wahimu wahitimu wa darasa la saba. Ni matumaini ya Wizara kuwa hatua hizi zitasaidia kupunguza kwa kiasi kikubwa idadi ya vijana wanaobaki mitaani baada ya kumaliza Elimu ya Msingi.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa hakuna mafunzo ya ualimu kwa wanafunzi wanaomaliza darasa la saba. Kiwango cha chini cha kujiunga na Vyuo vya Ualimu kwa sasa ni kuanzia waliofaulu Kidato cha Nne.

**MHE. AMINA C. MPAKANJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuweza kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri lakini nina maswali mawili.

(a) Kwa kuwa imethibitika ya kwamba elimu ya msingi haimwandai kijana wa Kitanzania, kuweza kujitegemea au kuanza kuyamudu maisha yake kwa yule ambaye anakuwa amekosa kwenda sekondari. Pia kwa kuwa wanafunzi asilimia 70 ya shule nyingi nchini Tanzania, wamekuwa hawapati nafasi ya kuendelea na masomo ya sekondari na wengi wao wazazi wao ni maskini hawana uwezo wa kuwalipia kusoma katika shule za Sekondari za binafsi. Aidha hawawsezi kwenda katika vyuo, hawana uwezo huo kabisa wa kulipa hata katika hivyo vyuo vya ufundi ambavyo Mheshimiwa Naibu Waziri amevisema.

Je, Serikali sasa iko tayari kulirudisha lile darasa la nane ambalo lilikuwepo miaka ya nyuma liwe maalum kwa ajili ya wanafunzi ambao hawajapata nafasi ya kuendelea na Sekondari wapate mwaka mmoja tu wa mafunzo ya ufundi ambayo yatawawezesha wao kwenda kujiajiri na kuyamudu maisha yao mitaani?

(b) Kama hilo la kwanza litakuwa haliwezekani. Je, Serikali sasa iko tayari kutoa agizo ama tamko kwa Halmashauri zote nchini Tanzania kuorodhesha majina ya wanafunzi ambao wamemaliza darasa la saba, lakini wamekosa nafasi ya kuendelea na sekondari ili wapate mafunzo kutoka kwa Maafisa Maendeleo, Maafisa Kilimo, Maafisa Ardhi, Maafisa Elimu, ambao wengi wao wameonekana hawana kazi za kufanya huko vijiji? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Amina Chifupa kama ifuatavyo:-

Ni kweli idadi ya wanafunzi ambao hawapati nafasi ya kuendelea *Form One* ni wengi. Lakini ombi la Mheshimiwa Mbunge la kutaka turudishe darasa la nane kwa ajili ya kujifunza shughuli za ufundi stadi mpango wa Wizara, baada ya kuunganisha *VETA* katika Wizara ya Elimu, suala la mafunzo ya ufundi, yatatiliwa mkazo na kama ilivyo katika Ilani ya Uchaguzi ambapo imeagizwa ifikapo mwaka 2010 kila Wilaya iwe imeshapata walau chuo kimoja cha ufundi stadi. Hivyo suala hili la kurudisha darasa la nane halitakuwa tena la msingi zaidi ni kila Wilaya ianze kujipanga ili kila Wilaya iwe na Chuo cha Ufundi kitakachoweza kuchukua vijana wengi ambao wanakosa nafasi ya kuendelea masomo ya Sekondari.

Kuhusu swali lake la pili kuwa Wizara itoe maagizo kwa wale walioshindwa ili waweze kupata mafunzo kutoka kwa Maafisa Kilimo, Maafisa Maendeleo na Wizara ya Elimu, hili suala kila Wizara ina mpango wake wa kuweza kuwachukua Maafisa Ugani au maafisa ambao wanaweza kusaidia katika Wizara hiyo. Lakini Wizara yetu ina mpango wa kuwaendeleza vijana ambao wamekosa nafasi ya kuendelea na masomo ya sekondari katika Vyuo vya *VETA*. Vyuo vya *VETA* si vingi vipo 21 tu.

Lakini mpango wa Serikali katika Wizara yetu unaandaliwa ili kuhakikisha kwamba vyuo hivi vinasambaa nchi nzima. Idadi hivi sasa ya vyuo binafsi ambavyo vinaendeshwa na Mashirika ya Dini, watu binafsi ni zaidi ya vyuo 819. Kwa kiasi hiki tukiweza pia kuongeza vyuo vya kila Wilaya tuna uhakika kwamba vijana wengi watapata nafasi ya kuweza kujiunga na ufundi stadi ili kuweza kujiboreshea maisha yao ya kila siku.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niongezee taarifa baada ya majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi kutokana na swali la nyongeza la Mheshimiwa Amina Chifupa Mpakanjia, kama ifuatavyo:-

Suala la kuwa na elimu ya msingi ya miaka saba ni sera. Sera yetu ya elimu ya mwaka 1995 inayotumika mpaka sasa inasema elimu ya msingi ni ya miaka saba. Kwa hiyo, kubadili ghafla haiwezekani mpaka hapa ambapo sera itakuwa imebadilishwa na kubadilisha sera siyo jambo la kuamua leo tu ghafla ni suala ambalo linahitaji umakini sana na kushirikisha jamii kwa sehemu kubwa sana. Kwa hiyo, nilitaka nimwambie

Mheshimiwa Mbunge kwamba kubadilisha kurudi miaka minane siyo jambo rahisi kwa sababu ndiyo sera ya elimu ilivyo hadi sasa.

Ningependa niongezee kwa jibu zuri alilotoa Mheshimiwa Mwananzila, kwamba katika jibu lake la msingi alieleza wazi kwamba Wizara ya Elimu sasa hivi inaandaa mpango wa upanuzi wa mafunzo ya elimu ya ufundi. Kwa msingi huo kupata wanafunzi wengi zaidi itategemea maandalizi ya mpango huo na kukamilika kwa mpango huo ambao utatusaidia kuelekeza kwa jinsi gani vyuo vya ufundi vitafika katika ngazi ya Wilaya. Lakini hata hivyo tunaelewa kwamba vijana wanahitaji mafunzo ya ufundi kwa sababu si wengi ambao wataendelea na elimu ya juu. Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Hii imechokoza mambo sasa.

**MHE. SUZAN J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa somo la stadi za kazi lilikuwa linasaidia sana wanafunzi pindi wamalizapo shule ya msingi kujitegemea. Lakini somo lile linafundishwa kinadharia na siyo kwa *practical*. Je, Wizara inasema nini kuhusu hili? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kumekuwepo na malalamiko ya Wazazi na walezi kwamba mafunzo ya ufundi stadi katika elimu ya msingi yamekuwa hayafanyiki kwa vitendo, lakini Wizara yangu baada ya kubadilisha mitaala na kuona umuhimu wa mafunzo ya ufundi stadi, tunasisitiza na kuwaelekeza Maafisa Elimu na hasa Wakaguzi wahakikishe kwamba mafunzo kwa vitendo yanafanyika katika ngazi ya elimu ya msingi ili watoto waweze kujipatia stadi ambazo zitawasaidia katika maisha yao. *(Makofi)*

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali imechukua hatua madhubuti kabisa kumpunguzia gharama mzazi kwa kulipia ada shilingi 20,000 kwenye shule za Sekondari za Serikali na hiyo imeongeza nafasi nyingi. Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka kulipia kiasi hicho hicho kwenye shule za *Private* ili wanafunzi wengi zaidi waweze kuhudhuria mafunzo ya sekondari? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA):** Mheshimiwa Spika, Wizara ya Elimu katika Sera yake ni kujaribu kupunguza gharama ya kumsomesha mwanafunzi ili kumwezesha hata mtoto anayetoka katika familia maskini aweze kusoma bila matatizo.

Sasa Wizara ilipoweka kiwango hiki ni kwa ajili ya wale watakaokuwa wamefaulu kwa kiwango kinachoridhisha na kuweza kuingia katika shule za sekondari za Serikali za Kutwa.

Sasa kufanya mpango huo uende hata kwa shule binafsi siyo rahisi kwa sababu uwezo wa Serikali kufidia fedha zile ambazo hazitakuwa zinalipwa na wazazi ni mdogo kifedha. Hivyo, bado Serikali itaendelea na mpango wake wa kuwatoza ada ya

Sh.20,000/= tu wale wanaofaulu na kuingia katika shule za Serikali na siyo shule za watu binafsi.

Na. 105

**Umeme – Vyanzo vya Nishati ya Umeme**

**MHE. RAYNALD A. MROPE** aliuliza:-

Kwa kuwa Tanzania ina vyanzo mbalimbali vya nishati ya umene na imedhihirika kwamba vyanzo rahisi ni vile vinavyotokana na gesi ya asili, makaa ya mawe na maji na kwa kuwa, tuna vyanzo vikubwa vya makaa ya mawe vya Kiwira na Mchuchuma ambavyo vina uwezo wa kuzalisha zaidi ya Megawati 400:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani kabambe ya kuyatumia makaa ya mawe ili kuzalisha umeme wa kutosha?

(b) Kwa kuwa mradi wa Mchuchuma ulikuwa chini ya *Mtwara Development Corridor* na Serikali imeunda Wizara Mpya ya Miundombinu. Je, mradi huo utakuwa chini ya Wizara gani?

(c) Je, kuna wawekezaji wowote ambao wameonesha nia ya kuwekeza kwenye miradi ya Kiwira na Mchuchuma na Serikali itathibitisha vipi kwamba mikataba haitafanana na ile ya *IPTL* na *Songas?*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Raynald Alfons Mrope, Mbunge wa Masasi, nitoe maelezo ya nyongeza ya kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge, kwa umakini na ufuatiliaji wa umeme kwa kutumia makaa ya mawe na mradi wa Mchuchuma na pia kwa kufuatilia masuala ya *Mtwara Corridor* kama ambavyo nimekuwa nikieleza hapa Bungeni. Serikali inatilia mkazo upanuaji wa wigo wa vyanzo vya uzalishaji wa umeme nchini.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naomba kujibu swali la Mheshimiwa Raynald Mrope, Mbunge wa Masasi, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali ina mpango kabambe wa *Power Sector Master Plan (PSMP)* wa miaka 25. Mpango huo unaainisha vyanzo muhimu vikiwemo nishati mbadala ya uzalishaji umeme kwa kutumia makaa ya mawe, ukubwa wa mradi, makisio ya gharama na wakati muafaka wa utekelezaji wa mradi. Mradi wa Mchuchuma umejumuishwa kwenye mpango wa *PSMP* niliyoisema.

(b) Mheshimiwa Spika, mradi wa Mchuchuma upo chini ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko. Na usimamizi wake na utekelezaji wake unafanywa na *NDC*.

(c) Mheshimiwa Spika, kampuni sita kutoka Kenya, Uganda, Afrika Kusini, Australia, India na Israeli zimeonyesha nia ya kuwekeza kwenye mradi wa Mchuchuma. Kuhusu mradi wa Kiwira Wizara yangu imekamilisha majadiliano na kampuni ya *Kiwira Coal and Power Company Limited* ambapo itapanua uzalishaji wa umeme kutoka megawati 6 za sasa hadi kufikia megawati 200 ifikapo mwaka 2008 kwa gharama za dola za Marekani milioni 260.

Kutokana na umuhimu wa kulinda maslahi ya Taifa na kwa kuzingatia tahadhari tulizopewa kuhusu wawekezaji wanaojali maslahi yao tu. Serikali kupitia Wizara yangu imeandaa Kamati maalum ya wataalam ili kupitia mapendekezo na kupendekeza njia nzuri za kupata mwekezaji ambaye atazingatia maslahi ya pande zote mbili. *(Makofi)*

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Nakushukuru Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Maswali yangu nataka kuyaelekeza zaidi katika swali langu la (b) kwamba kwa kuwa hivi karibuni imegunduliwa gesi nyingi sana *Mnazibay* huko Mtwara katika ukanda huu wa *Mtwara Development Corridor* kuna gesi yenye uwezo wa kuzalisha mpaka megawati 400.

Sasa ni lini kwa kuzingatia umuhimu huu ni lini Serikali itakubaliana nasi kuunda Sekretarieti Mtwara itakayokuwa inaangalia fursa hizi mpya ili iweze kufanya kazi ya kuleta viwanda vya mbolea, viwanda vya plastiki, viwanda vya gesi, kilimo, matumizi ya nyumbani na kadhalika, ni lini Serikali itaona umuhimu huo?

La pili, linalofanana na hilo kwa kuwa Waziri mwenyewe amesema kwamba *NDC* ndiyo inayoshughulikia maendeleo ya *Mtwara Development Corridor,* hivi karibuni Mkuu wake Mheshimiwa Kanali Simbakalia, kateuliwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Kigoma.

Sasa ndiyo basi kwenye *Mtwara Corridor* maana yake hatuoni cheche zozote siyo Wizara ya Miundombinu, siyo Wizara ya Viwanda, hakuna lolote linalotokea. Sasa hii *Mtwara Corridor* kuondoka kwa Simbakalia ndiyo maana yake ni mwisho wa haya maendeleo ambayo sisi watu wa Kusini kwa kweli tulikuwa tunategemea sana sana kuwepo na maendeleo hayo ambayo kwa muda mrefu hayajatokea? *(Kicheko/Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Kuunda Sekretarieti nafikiri sasa hivi iko bayana Serikali imekwishatoa tu siyo pendekezo na linafanyika sehemu nyingi kila Mkoa sasa hivi unaunda sekretarieti yake ya kuangalia vyanzo vyake vya maendeleo na kuweza kuweka kuwavutia wawekezaji katika maeneo yao. *Tanzania Investment Centre* imekwishaanza kuweka Idara zake sehemu mbalimbali jinsi kila eneo linavyoomba kusudi kuwasaidia namna gani ya kuweza kutumia rasilimali ambazo zipo katika Mikoa hiyo kuweza kuvutia wawekezaji. Kwa hiyo, nafikiri hilo halihitaji tamko la Serikali liko bayana wanaweza kutumia fursa hizo.

La pili, kuhusu kwamba hakuna kinachofanyika. Nafikiri hii si sahihi. Labda ni kwa sababu tu taarifa zilikuwa hazijamfikia Mheshimiwa Mrope, ingawa labda anazifahamu lakini hazioni moja kwa moja zina mahusiano na ile *programme* ya *Mtwara Development Corridor.*

Kwanza utafiti yakinifu wa barabara ya Mtwara hadi *Mbambabay* umeishakamilika kwa kutumia *Kuwait Fund* baadhi ya maendeleo hadi sasa yapo katika *design stage* kwa utekelezaji. Pili, kivuko cha kuunganisha Tanzania na *Mozambique Unit Bay* sasa hivi kimeanza kufanyiwa kazi na kinagharamiwa kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na *Mozambique.* Tatu, kivuko kikubwa cha kuunganisha ambacho kinajulikana kama *Heavy Duty Ferry Crossing* cha kuunganisha Tanzania na *Mozambique* kwa kupitia maeneo ya *Mbamba Bay* na *Nkata Bay* utafiti umekwishafanyika na pesa sasa hivi zinatafutwa.

Kulikuwepo na *study* ya reli toka Mtwara mpaka Liganga na Mchuchuma imefanywa na *Japanese Development Institute* na iko tayari katika *stage* ya majadiliano. Kuna Meneja aliyeajiriwa ambaye yuko *NDC* ambaye anaratibu miradi hiyo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mrope nataka kukuhakikishia na Wabunge wenzetu wote kwamba kazi ya *Mtwara Corridor* siyo maneno tu inafanyika mpaka sasa hivi. Ahsante sana.

**MHE. DEVOTA M. LIKOKOLA:** Ahsante Mheshimiwa Spika. Napenda pia kushukuru kwa ajili ya majibu mazuri ambayo Mheshimiwa Waziri ametupa. Kwa kuwa Serikali iliahidi kuwaelimisha wananchi wa Mkoa wa Ruvuma na wananchi wa Mikoa ya Kusini inayohusika na *Mtwara Corridor* juu ya mradi huu wa *Mtwara Corridor.* Je, kazi hiyo imeshaanza na kama haijaanza ni lini itaanza? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Waziri wangu kwa majibu mazuri ambayo yameniokoa. *(Kicheko/Makofi)*

Ni kweli shughuli za *Mtwara Development Corridor* zinafuatiliwa kwa makini na Serikali hatua za kuwaelimisha wananchi kwa namna watakavyofaidika na miradi hiyo itaendelea na itaanza kote ili wajue kwamba Ukanda wa *Mtwara Development Corridor* utawafaidia wananchi wa Mikoa yote mitatu ya Mtwara, Ruvuma pamoja na Lindi. Elimu mzuri itatolewa kuwaelimisha wananchi namna ya kushiriki katika maendeleo ya Ukanda wa Mtwara.

**SPIKA:** Tunaendelea Waheshimiwa. Swali linalofuata linaelekezwa Wizara hiyo hiyo. Linaulizwa na Mheshimiwa Maige, Mbunge wa Msalala. Kama taarifa zangu ni sahihi, hili ni swali la kwanza anauliza tangu alipofunga ndoa mwezi wa tisa. *(Kicheko/Makofi)*

Na. 106

**Miradi ya Maendeleo Sehemu za Madini**

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE** aliuliza:-

Kwa kuwa Sekta ya Madini inakuwa kwa kasi na pia inachangia kwa kiwango kikubwa pato la Taifa, na kwa kuwa jimbo la Msalala lina utajiri mkubwa wa dhahabu; na kwamba mgodi mkubwa kabisa wa madini hayo ni Bulyanhulu katika Jimbo la Msalala.

Je, kuna miradi mingapi ya maendeleo katika Kata ngapi na yenye kiasi gani iliyotekelezwa/inayotekelezwa kwa ushirikiano na ufadhili *KMCL* kama sehemu ya wajibu wake kwa jamii – *Social Corporate Social Resaponsibility* katika kipindi cha 2000-2005?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, na mimi nampongeza kwa kuuliza swali la kwanza baada ya kuoa. Karibu kwenye klabu ya wanandoa. Sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ezekiel Magolyo Maige, Mbunge wa Msalala, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba sekta ya madini inaendelea kukua kwa kasi kubwa katika kipindi cha miaka kumi iliyopita na kuwa chachu ya maendeleo katika nchi yetu. Kwa mfano, mchango wa sekta ya madini katika *GDP* umeongezeka kutoka asilimia 1.7 miaka kumi iliyopita hadi kufikia asilimia 3.2 mwaka 2005. Tathmini ya madini yanayouzwa nje ya nchi imeongezeka kutoka asilimia 2 ya thamani ya mauzo yote ya nchi katika kipindi cha miaka 10 iliyopita hadi kufikia asilimia 52 ya mauzo yote hadi sasa. Fedha iliyowekezwa katika sekta ya madini pia imeongezeka kutoka dola milioni 20 miaka kumi iliyopita hadi kufikia dola bilioni 1.5 hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, Jimbo la Msalala lina utajiri mkubwa wa madini ya dhahabu hususan katika eneo la Mgodi wa Bulyanhulu. Sera ya Madini ya mwaka 1997 inazungumzia umuhimu wa migodi kuchangia maendeleo ya jamii inayozunguka migodi hususan katika nyanja za ujenzi wa miundombinu, kijamii na kiuchumi kama vile upatikanaji wa nishati, usambazaji maji, usafiri, mawasiliano, huduma za afya, elimu na burudani. Aidha, Sera ya Madini inahimiza makampuni ya madini kuchangia maendeleo ya uchumi kwenye maeneo ya migodi kwa kutumia rasilimali zinazopatikana katika maeneo hayo ikiwa hali ya kiuchumi inaruhusu, jambo ambalo migodi mingi mikubwa hapa nchini imekuwa ikifanya.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyo kwa migodi mingine mikubwa iliyopo hapa nchini, mgodi wa Bulyanhulu unaomilikiwa na kampuni ya *Kahama Mining Corporation Limited (KMCL)* umekuwa ukijihusisha katika utoaji huduma mbalimbali za kijamii na kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, jumla ya miradi 22 ya kijamii yenye thamani ya dola za Marekani milioni 15,984 imetekelezwa na *KMCL* tangu mwaka 1999 hadi 2005. Aidha, *KMCL* imetenga dola za Marekani milioni 5.4 katika mwaka huu wa fedha kwa ajili ya

maendeleo ya jamii inayozunguka mgodi huo. Orodha ya miradi yote ya maendeleo ambayo imetekelezwa na *KMCL* katika kipindi cha 1999 – 2005 itakabidhiwa kwa Mheshimiwa Mbunge mara baada ya kipindi hiki cha maswali.

Mheshimiwa Spika, Kata zilizonufaika na miradi ya kijamii ya *KMCL* ni tatu nazo ni Kata ya Bugalama iliyoko katika Jimbo la Msalala, Kata ya Mwingiro ambayo iko katika Jimbo la Geita na Kata Igalilimi iliyomo katika Jimbo la Kahama.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu itaendelea kuhimiza migodi mikubwa kuongeza michango yake katika kuleta maendeleo ya jamii inayozunguka migodi hiyo.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Nashukuru Mheshimiwa Spika kunipatia nafasi niulize niulize swali la nyongeza na pia nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake ambayo kimsingi yanaonyesha takwimu ambazo zimeandaliwa na wenye mgodi wenyewe kuhusika.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kumekuwepo malalamiko kutoka kwa wananchi hasa kutokana na wao kutoshirikishwa katika kupanga vipaumbele ya maendeleo yao na miradi mingi ambayo ipo au imekuwa ikitajwa na mgodi huu kwamba imetolewa au imetekelezwa kwa wananchi. Ukweli wake ni kwamba imenufaisha mgodi wenyewe kwa sababu katika hizo dola milioni 15 inajumlisha gharama ya umeme kutoka Shinyanga kuja mgodini, inajumuisha gharama ya maji kuja mgodini kutoka Mwanza. Inajumlisha gharama za kujenga nyumba nafuu kwa wafanyakazi wa mgodi huo ambazo kwa ujumla zinalenga wenye mgodi kuliko wananchi.

Je, Serikali iko tayari sasa kushirikiana na hawa wenye mgodi ili kutekeleza vipaumbele ambavyo ni vya wananchi kwa sasa ambavyo ni pamoja na kujenga shule za sekondari katika Kata mbalimbali ikiwemo Shule ya Sekondari ya Bugalama, kusambaza umeme kwenye maeneo muhimu ya jamii kama sokoni, Bugalama, kijiji cha Kakola na Shule ya Sekondari ya Bugalama na Zahanati ya Bugalama? *(Makofi)*

Swali la pili, kwa kuwa moja ya kipengele katika mkataba wa Serikali na *Kahama Mining* pamoja na kwamba mkataba huo umekuwa ni siri kubwa unazungumzia kwamba Kampuni itakuwa inatoa kodi ya 0.3 asilimia kwenye Halmashauri kwa ajili ya maendeleo. Hii ni nje ya dola laki 2 ambazo zimeanza kulipwa mwaka huu. Je, Serikali iko tayari sasa kutusaidia wana Kahama ili kipengele hiki cha mkataba kiweze kutekelezwa na Halmashauri iweze kupata pesa za kutengeneza barabara ambayo ni mbaya sana inayotoka Kahama kwenda Kakola, ambayo pia watumiaji wakubwa ni wenyewe *Kahama Mining?*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kuhusu fedha za mradi zinazotolewa kwa vijiji vinavyozunguka. Ni kweli kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge kwamba wakati mwingi wawekezaji na wenye migodi husaidia vijiji na Halmashauri wakati mwingine bila kuwahusisha wananchi wenyewe katika kutoa vipaumbele. Ninaomba kutumia nafasi hii kuwataka wenye migodi yote

nchini kuwashirikisha wananchi wakati wa kuamua ni vipaumbele gani ambavyo wananchi wanavihitaji katika maeneo yote yanayozunguka migodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la asilimia 0.3 ya *service leavy* ambayo wachimba migodi wakubwa wanatakiwa kuitoa kwa Halmashauri na hawajatoa. Wizara imegundua kwamba kipo kipengele hicho cha kisheria ambacho kinawafanya wenye migodi mikubwa kudai kwamba watatoa tu asilimia 0.3 baada ya kutengeneza faida kwenye migodi yao. Na kwa hiyo lipo tatizo la *interpretation* kama asilimia 0.3 zitolewe kwa wananchi baada ya mgodi kutengeneza faida au itolewe baada ya mgodi wenyewe kupata ile *growth revenue* yaani mapato yote wanayoyakusanya kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, naomba nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba Wizara itapitia tu upya kipengele hiki cha sheria ili kuona kama *interpretation* ya halali ni ipi ili wananchi au Halmashauri kama zinastahili kupata asilimia hiyo wapewe bila kipingamizi. *(Makofi)*

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Utajiri ulioukumba wananchi wa Msalala naona na Mkoa wa Lindi unaanza kunukia. Sasa hivi wachimbaji wadogo wadogo wako katika Mkoa wa Lindi wakichimba madini. Je, Mheshimiwa Waziri atatueleza ni madini ya aina gani mpaka hivi sasa yameanza kuonekana katika Mkoa wa Lindi?

**SPIKA:** Hili ni swali jipya. Kwa hiyo, ningeomba liulizwe kwa sababu litasaidia sisi kufahamu madini yaliyoko Mkoa husika. Mheshimiwa Lembeli umehangaika sana, sasa uliza swali la mwisho la nyongeza.

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Nakushukuru Mheshimiwa Spika, kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa mgodi huu wa Bulyanhulu hutumia barabara ya Kakola-Kahama hadi Isaka kusafirisha hususan mchanga kwa kutumia malori makubwa ya zaidi ya tani 40 kiasi ambacho kimeathiri kwa kiwango kikubwa barabara hii na uwezo wa Halmashauri ya Wilaya ya Kahama kuitengeneza barabara hii ni mdogo sana. Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwashauri Bulyanhulu kuitengeneza barabara hii ili kuwaondolea kero wananchi wa maeneo ambako barabara hii inapita? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye swali la nyongeza. Mgodi wa Bulyanhulu na hawa wachimba mgodi wametenga dola za Marekani milioni 5.4 na nimeleza pia kwamba ni vizuri wenye migodi hii wakawashirikisha wananchi kikamilifu katika kuamua vipaumbele wanavyovitaka.

Ni matumaini yangu kwamba Mheshimiwa Mbunge, rafiki yangu, kwa kushirikiana na Halmashauri na wanamgodi hawa watakaa kutoa vipaumbele ili barabara aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge, ijengwe kwa kasi inayotakiwa.

Na. 107

**Rasilimali ya Ardhi Tanzania**

**MHE. ZAYNAB M. VULU** aliuliza:-

Kwa kuwa katika nchi zote za Jumuiya ya Afrika Mashariki na hata nchi jirani kama Rwanda na Burundi hakuna nchi hata moja yenye rasilimali ya ardhi Ambayo ni nzuri na haijatumika kama Tanzania:-

(a) Je, Serikali imejiandaa vipi ili rasilimali hiyo muhimu isichukuliwe na wageni na hasa Shirikisho la Afrika Mashariki litakapoanzishwa rasmi?

(b) Je, Serikali inafahamu kwamba miongoni mwa vitu vinavyotamaniwa na baadhi ya jirani zetu ni ardhi yetu ambayo ni nzuri sana?

(c) Kama Serikali imeliona hilo. Je, Watanzania na Serikali yetu kwa ujumla tunailindaje rasilimali hiyo muhimu kisheria?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Zaynab Matitu Vulu, Mbunge Viti Maalum, swalli lake lenye vipengele (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kwamba rasilimali ya ardhi ni kitu kikubwa na muhimu cha kutunzwa na kulindwa vizuri. Kwa misingi hii Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995 na Sheria ya Ardhi ya 1999 zilitungwa ili kuhakikisha kuwa kuna utaratibu madhubuti wa kusimamia ugawaji na matumizi ya ardhi. Serikali itaendelea kuhakikisha kuwa misingi hiyo iliyowekwa na Sera na Sheria katika umilikaji na utumiaji ardhi ardhi unaendelea kusisitizwa hata baada ya kuanzishwa kwa Shirikisho la Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Fungu la 20 la Sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999, upatikanaji wa ardhi na umiliki wa ardhi kwa wageni upo kama ifuatavyo:-

- Mgeni au mtu ambaye si raia atapewa na kumilikishwa ardhi kwa madhumuni ya uwekezaji na umilikishwaji huu utazingatia masharti ya Sheria ya uwekezaji ya mwaka 1997.

- Ili kulinda ardhi kisheria, ardhi itakayoainishwa kwa madhumuni ya uwekezaji itatangazwa katika Gazeti la Serikali na itamilikishwa kama hati miliki isiyo asili kwa mwekezaji.

- Kampuni, Taasisi au chombo chochote kinachotambulika kisheria ambacho wabia wake wengi ni wageni itatambuliwa kama ni kampuni au taasisi ya kigeni na itamilikishwa ardhi kwa madhumuni ya uwekezaji tu.

- Iwapo muda wa kumiliki ardhi kwa wageni utakwisha au kutenguliwa, haki zote juu ya ardhi hii zitabaki mikononi mwa *Tanzania Investment Centre (TIC)* au katika mamlaka nyingine yoyote itakayotangazwa katika Gazeti na Waziri mwenye dhamana ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, natoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge kushirikiana na Serikali kuhakikisha wageni wote wanapata ardhi kwa kuzingatia Sheria ya Uwekezaji ya mwaka 1977 na Sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999.

**MHE. ZAYNAB M. VULU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri. Nafurahi sana kuona Serikali imezingatia sana kwa suala la wageni na kwa kuwa nchi yetu bado ina eneo kubwa sana la ardhi nikizungumzia ardhi nina maana kwamba kuna madini, kuna kilimo na shughuli zingnezo za ardhi.

Je, Mheshimiwa Waziri anaweza akatuambia Serikali ina mikakati gani au ina mpango gani wa kuweza kuweka matumizi mazuri ya ardhi kwenye kilimo, mipango ya ujenzi wa nyumba na hasa tukizingatia kwenye kilimo na uchimbaji wa madini kwa kutumia nguvu kazi tuliyokuwa nayo ambayo ni vijana ambao watajipatia ajira na Taifa kuleta manufaa? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mhehsimiwa Spika, ni kweli tunatambua uzuri na thamani ya ardhi yetu ya Tanzania na Serikali kwa kupitia Wizara yangu imeunda Kitengo Maalum cha matumizi bora ya ardhi ambayo kwa sasa tumekwishaainisha maeneo mbalimbali ya kilimo. Maeneo mbalimbali ya ufugaji, maeneo mbalimbali ya madini na tunajaribu kuyagawa na kuyapima ili tuweze kuwapatia wananchi ambao watakuwa tayari kuweza kutumia ardhi hiyo.

Hii itawawezesha Waheshimiwa Wabunge wote kwa ujumla kuwasaidia wananchi ambao ni nguvukazi iliyopo kwa wingi ili waweze kutumia ardhi hii kwa manufaa ya kujinufaisha na kusaidia nchi kwa ujumla. *(Makofi)*

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika, kwa kuniona. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika kwa sababu sera ya Taifa ya Ardhi na Sheria ya Ardhi haijaeleweka kwa wananchi huko vijijini. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba inaiweka hii sheria katika lugha rahisi na kuweza kuwaelimisha wananchi vijijini kuelewa umuhimu wa ardhi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali imeona umuhimu wa kuwaelimisha wananchi waijue sheria za ardhi ili kuwasaidia kujua matumizi bora ya ardhi pamoja na kulinda ardhi yao.

Kwa maana hiyo Serikali imeanzisha kitengo kinachoitwa *Spill Strategic Plan for Implimentation of Land Laws* na tayari tumekwisha panga fungu la fedha ambalo litasaidia kutoa elimu nchi nzima ambayo itaelezea sheria ya Ardhi Na. 4, No. 5 na Sera ya mwaka 1995.

Na. 108

**Fidia kwa Wananchi wenye Viwanja Maeneo ya Vyanzo vya Maji**

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE** aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi ambao wamepewa viwanja katika maeneo ya vyanzo vya maji wanaendelea na shughuli zao za maendeleo katika maeneo hayo; na kwa kuwa mara wananchi hao wakishaviendeleza viwanja hivyo, Serikali hutoa amri ya kuhama kwa watu hao kwenye maeneo hayo:-

Je, watu hao watalipwa fidia za mali na muda walioutumia katika maeneo hayo?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Savelina Mwijage, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, maeneo ya vyanzo vya maji ni baadhi ya maeneo ambayo yanapaswa kulindwa kwani yakiharibiwa kwa kilimo au shughuli nyingine huleta madhara ya kimazingira. Madhara hayo ni pamoja na kusababisha maji kukauka na hivyo kuathiri maisha ya binadamu, wanyama na viumbe vingine vinavyotegemea maji hayo. Kwa kutambua hilo sera na sheria mbalimbali, hususan katika sekta za maji, mazingira na ardhi zimeweka masharti ya kulinda maeneo hayo. Kwa mfano, Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995 inatamka kuwa maeneo hayo ni nyeti na hayastahili kumilikishwa kwa mtu.

Sheria za Ardhi za mwaka 1999 pia zinayatambua maeneo hayo kama maeneo yenye madhara na ambayo yanahitaji kulindwa. Sheria hizo zinatambua maeneo hayo kama maeneo ya hifadhi na zinaweka sharti la kuachwa kwa eneo la mita sitini kutoka chanzo cha maji au ukingo wa mto ambalo halitamilikishwa kwa mtu yeyote. Hivyo kumilikisha kwa ardhi katika vyanzo vya maji ni kitendo cha ukiukaji wa sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, iwapo itatokea kuwa wananchi wamemilikishwa ardhi kwenye chanzo cha maji na Serikali kuamuru wahame, wananchi hao wanastahili fidia. Kwa mujibu wa fungu la 3(1)(g) la Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999, Sheria ya Ardhi ya Vijiji ya mwaka 1999 na Kanuni za Sheria za mwaka 2001, fidia itakayolipwa itaazingatia yafuatayo:-

(i) Fidia ya thamani ya ardhi;
(ii) Fidia ya maendeleo yasiyohamishika;
(iii) Posho ya upangaji;
(iv) Posho ya kupoteza fidia;
(v) Posho ya usumbufu; na
(vi) Posho ya usafiri.

Mheshimiwa Spika, posho za usafiri, upangaji na kupoteza faida hazitalipwa kama ardhi inayohusika ilikuwa haikaliwi. Aidha, fidia hiyo inatakiwa ilipwe kamilifu na kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwa wananchi ni kuwa wasilime wala kufuga karibu na vyanzo vya maji ili kutunza mazingira. Aidha, waunge mkono juhudi za Serikali na asasi zisizo za Kiserikali zinazolenga kulinda vyanzo vya maji. *(Makofi)*

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, ninamshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu yake mazuri.

**SPIKA:** Subiri basi, Mheshimiwa sijakurushu, basi kwa kuwa ni haki yako,uliza swali la nyongeza.

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Namshukuru sana Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Je, atakubaliana na mimi kwamba wanaosababisha kugawa viwanja katika sehemu hizo za mabondeni na vyanzo vya maji ni ofisi yake ya ardhi, je, Serikali inawachukulia hatua gani hao watu wanaosababisha kugawa viwanja hivyo na wananchi wapate hasara?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali ma Mheshimiwa Savelina Mwijage, kuwa sina hakika kwamba wanaogawa maeneo ya ardhi ni watu kutoka Wizara yangu. Lakini Serikali sasa hivi kwa kupitia tamko la Makamu wa Rais, tunapitia maeneo yote ya vyanzo vya maji na kutizama kama yaligawiwa kisheria au watu walivamia, basi tutakapomaliza zoezi hilo wale wote ambao waligawa maeneo hayo na kuleta uharibifu wa mazingira watachukuliwa hatua za kisheria. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kuna maswali mawili yamesalia, tutayaweka katika *Order Paper* kwa siku inayofuata.

Ninayo Matangazo machache, kama kawaida nitaanza na wageni. Ninafurahi kutambua kuwepo kwenye *Speakers Gallery, Mrs.* Makamba (Mama Makamba), ambaye ni mke wa Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi. Huyu mama ni maarufu kwa jina la

Mama Januari, karibu sana, tunakukaribisha, Mzee naye ninaona yuko Bungeni, sijui kwa nini amenuna wakati sisi tunamtambulisha mkewe. *(Makofi/Kicheko)*

Mama Januari, amefuatana na Ndugu Gordon Mwakitabu, Katibu wa Katibu Mkuu wa CCM, karibu sana na Ndugu Agnes Hokororo, Afisa Utumishi Makao ya Chama cha Mapinduzi Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni kutoka Ubalozi wa Uingereza Dar es Salaam, Bwana John Bratty Short, huyu ni Afisa wa Mambo ya Siasa na Habari.*Welcome to the House Mr. Bratty Short, I believe your new posting to Tanzania, you are welcomed to Dodoma, you are welcomed to fratenized with Members of Parliaments. Our country and yours enjoy such excellent relations, and we are happy to see you here. (Applause)*

Wapo wageni kutoka Dayosisi Katoliki ya Musoma, ni Wageni Mheshimiwa Gaudentia Kabaka, Naibu Waziri wa Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia, hao ni Masista Suzan Masubi, Sista Clara Nkambi na Sista Max. Karibuni sana, najua ninyi mmezoea mambo ya ulimwengu ujao. Lakini si vibaya mkaja kuyaona haya yetu ya ulimwengu wa sasa. *(Kicheko/Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Omari Kwaangw', Mbunge wa Babati, ni Wajumbe 11 wa Bodi ya *SACCOS* kutoka Babati, *Lake Teachers SACCOS*.

Pale Babati wana ziwa dogo hivi, basi wanaita *Lake* utadhani ni kubwa sana. Lakini ndiyo hivyo tena, sasa Chama hiki kinaitwa *Lake Teahcers SACCOS,* kisichanganywe na mambo kama *Lake Victoria* au *Lake Tanganyika* na *Lake Nyasa,* wanaongozwa na Mwalimu Monica Mungure, ambaye ni Mwenyekiti wao. Naomba wasimame wale wa *Lake SACCOS.* Tunawapongeza sana kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya kuanzisha na kuendeleza *SACCOS,* kama chombo cha kumkomboa mnyonge.

Napenda nitoe pongezi maalum kwa Mwalimu Monica Mungure, kwa sababu kwa utamaduni wetu, si vyepesi mambo haya yakaongozwa na mwanamke, lakini nakupongeza sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, bado kuna mfumo dume jamani, kwa hiyo, huo ni ukweli, ukipata mwanamama kama yule ndiye anayeongoza *SACCOS* kubwa kama ile ya Babati, ni jambo la kufurahi sana. Ahsanteni sana na karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wengine ni Madiwani 15 kutoka Jimbo la Musoma Mjini, wakiwa na watalaam wawili wa Halimashauri ya Mji wa Musoma, wanaongozwa na Mstahiki Meya, Mheshimiwa Swaib Mohamed, wao ni wageni wa Mheshimiwa Vedastusi Manyinyi, Mheshimiwa Gaudentia Kabaka na Mheshimiwa Rosemary Kirigini, karibuni sana tunafarijika sana tukiwaona wenzetu ambao mko karibu kabisa na wananchi katoka huko, kuja kututembelea. Karibuni sana na mtusalime mtakaporejea huko Musoma. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge pia tunao wanafunzi 40 na Walimu wawili kutoka Shule ya Msingi ya Amani ya mjini Dodoma ambao wamekuja kujifunza shughuli za Bunge, ahsanteni wanafunzi na Walimu karibuni sana. *(Makofi)*

Waziri wa Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Joseph Mungai, amependa niwatambulishe wageni wake na hao pia ni wageni wa Mheshimiwa Benito Malangalila, ni Mheshimiwa Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi, Diwani Nyaganilwa, amefuatana na Mheshimiwa Diwani Kaguo, ambaye ni Makamu wa Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mufindi na Diwani Kivenuke, ahsante sana na karibuni sana sisi tunaendelea na kunywa chai bora. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kuna wageni wa Mheshimiwa Abbas Mtemvu, kama ifuatavyo, hawa ni Madiwani na Wenyeviti wa Serikali za Mitaa kutoka Temeke, Mheshimiwa Ali Kinyaka, Diwani Kata ya Mtoni, ahsante sana karibu sana. Mheshimiwa, Mheshimiwa Judith Magembe, Diwani wa Viti Maalum, Mheshimiwa William Mwakabaga, Mwenyekiti wa Mtaa kupitia Chama cha Mapinduzi, Mheshimiwa Iddi Ngandali, Mwenyekiti pia wa Mtaa kupitia Chama cha Wananchi *(CUF)* na Mheshimiwa Hemed Pazi, Mwenyekiti wa Mtaa, kupitia Chama cha Wananchi *(CUF),* karibu sana Waheshimiwa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, binti ya Mheshimwia Makamba, anayeitwa Mwamvita, amebuni Jarida katika Mfumo wa *DVD*. Jarida ambalo linaitwa *Real DVD Magazine,* ni kama Jarida ambalo liko katika mfumo wa *electronic,* Katibu wa Bunge ameruhusu maonyesho ya *DVD* hizo na zitauzwa pale mahali petu pa kawaida pa maonyesho pale. Kwa hiyo mnakaribishwa kuona ubunifu wa binti huyu, ni vizuri Waheshimiwa Wabunge mkamuunga mkono kwa kununua *DVD* hiyo, ina mambo yanayoonyesha vivutio vya nchi yetu, lakini pia na mambo ya utamaduni yaliyo katika nchi yetu, karibuni sana. *(Makofi)*

Kuhusu vikao vya Kamati, Wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, wanaombwa na Mwenyekiti wao Mhehsimiwa Jenista Mhagama, kwamba leo saa tano asubuhi, kutakuwa na kikao cha Kamati hiyo ukumbi namba 219 ghorofa ya pili. Kamati ya Maendeleo ya Jamii, saa tano asubuhi, ukumbi nambari 219. Mheshimiwa Brg. Jen. Hassan Ngwilizi, Kiongozi wa Msafara wa Wabunge waliokwenda Canada, anaomba Wajumbe wote waliokuwa katika msafara huo wakutane leo saa tano asubuhi, chumba nambari 432.

Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu ameniomba nitangaze kuwa Wajumbe wote wa Kamati ya Miundombinu watakutana leo Alhamisi, tarehe 9 Novemba, 2006 saa saba mchana katika ukumbi namba 427 kwa kikao kifupi. Kamati ya Miundombinu saa saba mchana chumba namba 427.

Mheshimiwa William Shellukindo, Mwenyekiti wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara, anaomba kwamba Wajumbe wote wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara ya Bunge wakutane leo saa saba mchana ukumbi namba 133, Kamati ya Uwekezaji na Bishara saa saba mchana ukumbi namba 133.

Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Maliasili na Mazingira, Mheshimiwa Hassan Rajab Khatib, ameniomba nitangaze kwamba Kamati ya Maliasili na Utalii, wakutane saa saba mchana chumba namba 231, saa saba mchana Kamati ya Maliasili na Utalii, wakutane pale chumba namba 231.

Hili ni tangazo kutoka kwa Mheshimiwa Margareth Sitta, Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Waziri anawatangazia Waheshimiwa Wenyeviti wote wa Wabunge wa kila Mkoa wa Tanzania Bara kwamba katika Ofisi ya *CPA* ipo michanganuo ya mgawanyo wa fedha za *MMES,* kwa kila Mkoa, mpango ule wa Sekondari kwa kila mkoa. Mgawanyo huo umeainisha yafuatayo:-

(a) Ujenzi wa nyumba za walimu na vyumba vya madarasa katika kila Wilaya, kwa maana hiyo kila Jimbo;

(b) Vifaa vya kufundishia na kujifunzia;

(c) Kufidia punguzo la ada kwa Shule za Sekondari za kutwa; na

(d) Mpango wa chakula cha wanafunzi.

Mheshimiwa Spika, fedha hizo zimetumwa Hazina ndogo ya kila mkoa kati ya tarehe 11 Oktoba na tarehe 7 Novemba, 2006. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge mnaombwa kupitia kwa Wenyeviti wa Wabunge wa kila mkoa Tanzania Bara, mkazipate taarifa hizi muhimu kwa sababu zitasaidia pia licha tu ya Waheshimiwa Wabunge kufahamu, utekelezaji wa *MMES* katika maeneo yao, utasaidia pia kuisaidia Serikali udhibiti kuhusu matumizi, kwa sababu fedha zimeonyeshwa bayana, siyo tu zilizotengwa na zilizopifikishwa. Nadhani mtakubaliana nami kwamba Waziri huyu anachapa kazi kweli kweli. *(Kicheko/Makofi).*

Mheshimiwa Spika, huo ndiyo mwisho wa matangazo. Tuanatendelea.

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Huduma za Mawasiliano wa Mwaka 2006 *(The Universal Communications Access Services Bill, 2006)*

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Huduma za Mawasiliano wa Mwaka 2006 *(The Universal Communications Access Services Bill, 2006)* sasa usomwe mara ya pili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Muswada huu unapendekeza kutungwa kwa Sheria itakayoweka utaratibu wa Kisheria utakaotoa mwongozo, taratibu na usimamizi wa utoaji wa huduma za mawasiliano nchini hususan katika maeneo ya vijijini. Ili kutekeleza azma

hiyo, inakusudiwa kuanzisha mfumo wa maendeleo utakaotumika, kuhamasisha uenezaji wa huduma za posta, simu, *internet,* tovuti, barua pepe na utangazaji katika maeneo ya Vijijini.

Mheshimiwa Spika, napenda kulikumbusha Bunge lako Tukufu kwamba Muswada huu wa Sheria ya Huduma za Mawasiliano ulisomwa mara ya kwanza Bungeni tarehe 29 Machi, 2006. Hivi sasa umechapishwa upya baada ya kuzingatia maoni na ushauri wa wadau mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, katika azma ya kuboresha mawasiliano nchini hasa maeneo ya vijijini, Serikali imekwisha idhinisha Sera nne kuhusu Sekta nzima ya mawasilino. Sera hizo ni Sera ya Taifa ya Mawasiliano ya Simu yaani *The National Telecommunication Policy of 1997,* ambayo pamoja na mambo mengine imeweka lengo la kusambaza huduma za mawasiliano ya simu kwa wastani wa angalu njia sita kwa kila wananchi 100 ifikapo mwaka 2020.

Mheshimiwa Spika, *Teledensity,* sera hii inaainisha pia umuhimu wa kuwa na Mfuko wa Maendeleo ya Simu Vijijini utakaowezesha kufikia malengo hayo yaliyowekwa ya kusambazwa simu katika maeneo ya vijijini. Sera ya pili ya Taifa ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano yaani *The National Information and Communition Technology Policy 2003.* Sera hii inaweka msisitizo katika kueneza huduma za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano yaani Teknohama vijijni ili kuharakisha juhudi za Taifa za kufikia maelengo ya kukuza uchumi na kuondoa umaskini. Huduma hizo ni pamoja kama nilivyosema na huduma za simu, tovuti, *internet* na barua pepe ambazo ni muhimu sana katika kuendeleza na kuimarisha huduma ya elimu, afya na huduma za uzalishaji na utafuta ji wa masoko kwa ujumla.

Sera ya tatu ni Sera ya Taifa ya Posta, *The National Postal Policy of 2003* ambayo inatoa mwongozo wa namna ya kuboresha viwango vya huduma ya posta kwa wananchi. Sera hii pia inasisitiza umuhimu wa kuwa na mfumo wa maendeleo ya huduma za mawasiliano utakaowezesha huduma hizo kufika vijijini.

Sera ya nne, ni Sera ya Utangazaji. Sera hiyo inasisitiza umuhimu wa kuwa na mtandao bora wa matangazo na kupashana habari kwa njia ya Redio, Televisheni, Magazeti na Machapisho utakazozifikisha huduma hizo kwa wananchi wengi vijijini. Matumizi ya mfuko unaokusudiwa kuleta maendeleo katika maeneo yale ambayo uwekezaji hauna maslahi kibiashara. Hivyo matumizi ya mfuko yatakuwa ni pamoja na kutoa ruzuku kwa wawekezaji au watoa huduma za mawasiliano ya simu, posta, tovuti, barua pepe na utangazaji ambao watakuwa tayari kufanya hivyo katika maeneo ambayo yataanishwa na mfuko.

Mheshimwia Spika, mwelekeo wa sasa wa utoaji huduma za mawasiliano ni wa kushirikisha zaidi sekta binafsi. Sekta binafsi inatoa huduma zake kwa misingi ya kibiashara na kupata faida. Kwa kupitia sheria hii, maeneo ya vijijini na yale ambayo kwa kuzingatia misingi ya kibiashara peke yake hayawezi kupata huduma hizo sasa yataweza kupata huduma za mawasiliano. Sheria hii inaweka taratibu zitakaozwezesha

kusambaza huduma za mawasiliano katika maeneo ya vijiji na hivyo kutimiza malengo ya kisera yaliyotajwa kwenye sera za Taifa za mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, faida za msingi zitakazotokana na Muswada huu ni pamoja na:-

(i) Kuwa na huduma za mawasiliano sehemu zote nchini, hususan vijijini na maeneo yasiyo na mvuto kibiashara.

(ii) Kuwepo kwa mfumo huu kutawezesha sekta nyingine kutekeleza majukumu yake vizuri zaidi vijijini na kwa ufanisi, mfano sekta ya afya, sekta ya elimu, kilimo, biashara, masoko, utalii na utafiti.

(iii) Sheria itachochea uwekezaji kutoka sekta binafsi, itasaidia kuleta mbinu mpya za utendaji kazi, pamoja na teknolojia ya kisasa inayofaa kwa matumizi ya maeneo ya vijijini na hivyo kuboresha utoaji huduma.

(iv) Sheria itachochea upatikanaji wa ajira zitakazotokana na programu mbalimbali za kueneza huduma za mawasiliano.

(v) Itaongeza mchango wa sekta ya mawasiliano katika Pato la Taifa.

(vi) Itafanikisha malengo ya sera ya kila kijiji kuwa na huduma za mawasilinao.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu una sehemu saba kama hivi ifuatavyo:-

Sehemu ya kwanza inahusu Jina la Sheria, tarehe ya kuanza kutumika kwa sheria, sehemu utakapotumika na tafsiri ya maeneo yaliyotumika.

Sehemu ya pili, inahusu uanzishwaji wa mfuko kama chombo cha kusimamia fedha za mfuko. Sehemu hiyo inatoa mamlaka ya kisheria kwa chombo husika ya kuweza kushtaki au kushtakiwa. Uwezo wa chombo hicho kumiliki mali na mamlaka ya kutekeleza majukumu na madhumuni ya kuanzishwa kwake.

Sehemu ya tatu, inahusu kuanzishwa kwa Bodi ya Mfuko, inaainisha majukumu ya Bodi, uwezo wake kisheria katika kutekeleza majukumu yake. Uteuzi wa Mtendaji Mkuu wa Mfuko na wafanyakazi wengine wa Mfuko huo.

Sehemu ya nne, inaweka masharti kuhusu utoaji wa huduma za lazima za mawasiliano ili kuwezesha usambazaji mzuri wa huduma hiyo. Muswada unapendekeza kwamba matumizi ya miundombinu ya mtandao yafanyike kwa gharama nafuu kwa kuzingatia usawa na bila ubaguzi wowote. Aidha,Muswada unapendekeza kuweka masharti yatakayowabana watoa huduma za lazima kwa kuwataka wawasilishe taarifa muhimu kwa mfuko ikiwa ni pamoja na sera na mchanganuo wa aina ya huduma wakatakazotoa. Taarifa hizo lazima zikidhi viwango vya gharama kama vitakavyokuwa vimekubalika na mfuko.

Kwa upande wake mfuko utakuwa na wajibu wa kutoa ruzuku pale inapoonekana inafaa kufanya hviyo ili kukuza au kuimarisha usambazaji wa utoaji mzuri wa huduma za mawasiliano vijijini.

Sehemu ya tano, inahusu vyanzo mbalimbali vya fedha za mfuko, inazungumzia ukaguzi wa mahesabu ya mfuko, inazungumzia taarifa na Bajeti ya kila mwaka ya mfuko huo.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya sita, inahusu kanuni na taratibu za utekelezaji wa Sheria ya Mfuko na vifungu vya mpito ambavyo vitasaidia kuondoa utata utakaoweza kujitokeza baina ya sheria hii na sheria nyingine zinazohusu masuala haya na sehemu ya saba, inahusu marekebisho kwenye sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania yaani *The Tanzania Communication Regulatory Authority Act, 12 of 2003* yatakayofuata yaani *consequntial* kutokana na utekelezaji wa Sheria hii.

Mheshimiwa Spika, ufanisi wa utoaji huduma za mawasiliano hapa nchini, unategemea kwa kiasi kikubwa jinsi Serikali itakakvyoweza kushirikisha uwekezaji wa sekta binafsi. Ushirikishaji wa uwekezaji wa sekta binfasi kwa kiasi kikubwa unatokana na kuwepo kwa sera nzuri na taratibu zitakazoweza kutochochoea uwekezaji upatikanaji wa huduma za mawasiliano. Naamini Serikali imeandaa mazingira mazuri ya kutekeleza azma hiyo. Sheria, Kanuni na taratibu zilizobayana ndiyo nyenzo madhubuti ya kuwezesha kufikia malengo ya sera za sekta nzima ya mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishukuru kwa dhati Kamati ya Bunge ya Miundombinu chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mbunge wa Singida Kusini, kwa maoni na ushauri ambao umesaidia kwa kiasi kikubwa kuwezesha Muswada huu kuwasilishwa mbele ya Bunge letu Tukufu, asubuhi hii.

Aidha, naishukuru Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, hususan Idara ya Mwandishi Mkuu wa Sheria, kwa maandalizi mazuri na msaada wa karibu iliyonipa wakati wa kuwasilisha Muswada huu mbele ya Kamati ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, wakati namwita Mwenyekiti au Mwakilishi wa Kamati ya Miundombinu iliyoupitia Muswada huu kwenye Kamati, natangaza ya kwamba kwenye orodha yangu ninao wachangiaji nane na orodha bado iko wazi. Kwa wale wanaotaka kuchangia tutapokea majina yao kama kawaida. Sasa namwita mwakilishi wa Kamati ya Miundombinu, ili awasilishe taarifa ya Kamati. *(Makofi)*

**MHE. PAUL P. KIMITI (k.n.y MHE. MOHAMED H. MISSANGA - MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, nashukuru kupata fursa hii ili niweze

kuwasilisha maoni ya Kamati ya Bunge ya Miundombinu kuhusu Muswada wa Sheria ya Huduma za Mawasiliano wa mwaka 2006 *(The Universal Communications Service Act, 2006)* kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 70(2). *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba niitumie nafasi hii pia kutoa pongezi zangu za dhati kwa wagombea wa nafasi za Uwakilishi wa Ubunge katika Bunge la Afrika Mashariki walioibuka na ushindi mkubwa sana katika uchaguzi uliofanyika wiki iliyopita. Aidha, nimpongeze Mheshimiwa Ali Ameir Mohamed, aliyeibuka mshindi katika kinyang'anyiro cha uchaguzi wa kumpata Katibu wa Kamati ya Wabunge wa Chama cha Mapinduzi, ambao pia ulifanyika mwishoni mwa wiki iliyopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati yangu nachukua fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa Andrew Chenge, kwa kuteuliwa kwake kuwa Waziri wa Miundombinu. Pia nachukua nafasi hii na ninaahidi kwamba sisi Wajumbe wa Kamati ya Miundombinu tuko pamoja naye, tutamsaidia kila aina ya msaada atakaohitaji ili aweze kufanya kazi yake vizuri.

Pia nampongeza Mheshimiwa Basil Mramba aliyekuwa anaongoza Wizara hii kwa kuteuliwa kwake kuwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko pamoja na Mawaziri na Manaibu Waziri wengine wote walioteuliwa kushika nafasi katika Wizara mbalimbali katika mabadiliko yaliyofanywa na Mheshimiwa Rais hivi karibuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuanza kwa Mkutano huu wa Tano wa Bunge, uliipelekea Kamati yangu kazi ya kuupitia na kuujadili Muswada wa Sheria ya kuanzisha Mfuko wa Huduma za Mawasiliano wa mwaka 2006. Napenda kuchukua fursa hii kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Kamati yangu ilitekeleza kazi hiyo kwa ufanisi wa hali ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, madhumuni ya Muswada huu ni kutoa mapendekezo ili kutunga sheria inayosimamia utekelezaji wa huduma za mawasiliano katika maeneo ya watu wenye kipato kidogo mijini na vijijini.

Aidha, Muswada huu unakusudia kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Huduma za Mawasiliano kwa nia ya kusambaza huduma hiyo ili iwafikie wananchi wengi zaidi na hasa kwenye maeneo yaliyo nyuma kimawasiliano katika baadhi ya sehemu za mijini hasa huko vijijini.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 69(2) ya Kanuni za Bunge za mwaka 2004 Kamati ilipata fursa ya kukutana na wadau husika wa Muswada wa Sheria ya Huduma za Mawasiliano wa mwaka 2006 na kupata maoni na mapendekezo yao. Maoni ya wadau hao yaliwasilishwa mbele ya Kamati tarehe 18 hadi 19 Oktoba, 2006 katika kikao kilichofanyika Ofisi Ndogo ya Bunge, Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati inawapongeza kwa dhati wadau wote muhimu kwa ushiriki wao katika kuandaa Muswada huu ambao ni watumiaji binafsi wa huduma hiyo,

Sekta mbalimbali za Kiserikali na za watu binafsi kama vile Kampuni za Simu Tanzania za *Zantel, Vodacom, Celtel, tiGO* na *TTCL, Cats Net Limited*, Benki ya Posta, Shirika la Posta, *SIMU 2000 Limited*, *Simba Net, TAC Associates, Media Owner's Associations of Tanzania, University Computing Center-UDSM, Dimon Morogoro Tobacco Processor Limited (DMTPL)* na wengine wengi sana ambao sitaweza kuwataja wote lakini walishiriki kwa namna moja au nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati kwa kutambua umuhimu wa kushirikisha Wizara mbalimbali katika maandalizi ya Muswada huu chini ya Wizara husika ya Miundombinu; Ofisi zifuatazo tumeshirikiana nazo kwa karibu sana kufikia muafaka ambao tunauleta mbele ya Bunge hili Tukufu. Ofisi zenyewe ni pamoja na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano Tanzania *(TCRA),* Shirika la Kurekebisha Mashirika ya Umma *(PSRC)* chini ya Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji, Ofisi ya Waziri Mkuu na Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo. *(Makofi)*

Kamati inaipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu ambao utawezesha kuwepo kwa sheria mahsusi itakayoenda na wakati ili kukidhi mahitaji yaliyopo katika Sekta ya Mawasiliano hapa Tanzania. Aidha, sheria hii inakusudiwa kwenda sambamba na kasi ya mabadiliko ya teknolojia ya mawasiliano, namna ya kufikisha huduma hiyo vijijini na kwenye maeneo ambayo hayana maslahi kwa misingi ya kibiashara.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Sheria hii itakayotungwa inakusudiwa kukidhi matakwa ya watoaji na watumiaji wa huduma ya mawasiliano kwa kuweka utaratibu ambao utatoa mwongozo na usimamizi wa usambazaji wa huduma ya mawasiliano na pia kuuwezesha Mfuko wa Maendeleo unaopendekezwa utumike katika kutoa ruzuku kwa wawekezaji, waendeshaji na watoa huduma za mawasiliano ya simu, posta na utangazaji kwa manufaa ya maendeleo ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati inatoa maoni na ushauri ufuatao:-

Mheshimiwa Spika, awali ya yote Kamati inaipongeza sana Serikali kwa kukubali kufanya marekebisho ambayo yalipendekezwa yafanyike wakati Muswada ulipoletwa kwa mara ya kwanza mwezi Machi, 2006. Hii inatoa fursa nzuri kwa Bunge kutunga sheria ambazo zinakidhi matakwa ya watumiaji wa sheria husika na kwa manufaa ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa malengo ya Muswada huu ni mazuri sana kwa maslahi ya maendeleo ya Taifa letu, Kamati inashauri kuwa Mfuko wa Maendeleo ya Huduma za Mawasiliano uanze haraka mara moja na sambamba na uteuzi wa Wajumbe wa Bodi ya Mfuko huo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la matumizi ya miundombinu na usambazaji za huduma ya mawasiliano, Kamati inasisitiza kuwa miundombinu hiyo itolewe kwa gharama nafuu ili kumpunguzia gharama za mtumiaji wa huduma hiyo.

Kamati inashauri kuwa Bodi ya Mfuko wa Maendeleo ya Huduma za Mawasiliano iwe makini katika kutoa ruzuku kwa watoa huduma hiyo; kufanya uhakiki ili kubaini uwezo wa mhusika kabla ya kutoa ruzuku yenyewe. Hii itasaidia kupunguza matumizi mabaya ya Mfuko wenyewe na kutowayumbisha watumiaji wa huduma hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika**,** Mfuko wa Huduma ya Maendeleo ya Mawasiliano uhakikishe kuwa wamiliki wa miundombinu ya kutolea huduma hiyo wanatekeleza wajibu wao ipasavyo kwa mujibu wa sheria. Aidha, kwa wale ambao watakiuka utaratibu wachukuliwe hatua kali ili kulinda haki ya wadau wa huduma hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua nafasi muhimu waliyonayo wadau katika kuchangia Mfuko huu, Kamati inashauri kuwa Serikali iweke utaratibu maalum wakati wa kutengeneza Kanuni utakaowawezesha wadau wengi zaidi kushiriki katika kuchangia Mfuko wa Huduma ya Maendeleo ya Mawasiliano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba Muswada unaelekeza kuhusu kipindi cha utumishi wa Meneja wa Mfuko pamoja na majukumu yake, Kamati inapendekeza Kanuni zitakazotungwa na Waziri ziainishe kuwa Meneja wa Mfuko anawajibika kwa Bodi ya Wakurugenzi. Hii itasaidia kuondoa utata ambao unajitokeza katika sehemu mbalimbali ambao tumeona katika Muswada huo. Tunashukuru ya kwamba baadhi ya marekebisho yameingizwa kufuatana na mapendekezo tuliyokuwa tumeyatoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mafanikio ya Sheria hii yatategemea sana kwa jinsi miundombinu ya mawasiliano itakavyokuwa imeandaliwa na kuleta unafuu wa gharama kwa watumiaji wa huduma hii. Serikali itoe kipaumbele katika kueneza mtandao wa Mkongo *(Optic Fibre)* katika maeneo ya nchi pamoja na ile inayounganisha nchi za nje na hasa za majirani kwa minajili ya kupunguza gharama badala ya kuendelea utaratibu wa *satellite*. Aidha, huduma za msingi za Posta ziimarishwe ikiwa ni pamoja na Shirika lenyewe ambalo hali yake kwa sasa si nzuri.

Mheshimiwa Spika, hitimisho, kwa niaba ya Kamati yangu napenda nikushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha maoni ya Kamati. Aidha, nitumie nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Andrew Chenge, Waziri wa Miundombinu, Mheshimiwa Dr. Maua Daftari na Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga, Naibu Mawaziri wa Miundombinu, Ndugu John Kijazi, Katibu Mkuu wa Wizara ya Miundombinu, pamoja na wataalamu na watendaji wote wa Wizara hii walioshirikiana na Kamati katika kuandaa na kutoa maelezo ya kina pale yalipohitajika. *(Makofi)*

Pia napenda kutoa shukrani za pekee kwa Mheshimiwa Johnson Mwanyika, Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na wataalamu wake wote kwa kutoa ufafanuzi wa vipengele mbalimbali kwa Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati inawashukuru wadau wote niliokwisha wataja hapo awali kwa kushiriki kwao katika *public hearing* na kutoa maoni yao ambayo kwa kiasi kikubwa yamesaidia sana katika kukamilisha na kuuboresha Muswada huu. Kwa

ushirikiano na kazi nzuri ya wadau hao Muswada umeandaliwa na kuwasilishwa kwa ufasaha na kufanya kazi kama Kamati ilivyokuwa imeagiza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee napenda kutoa shukrani za dhati kwa Wajumbe wa Kamati ya Miundombinu ambao walishiriki kikamilifu katika kuuandaa na kuujadili kwa ufasaha na kuuboresha Muswada huu.

Naomba niwatambue kwa majina Wajumbe hao kama ifuatavyo, Mheshimiwa Mohammed Missanga, Mwenyekiti, Mheshimiwa Joyce Masunga, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Khadija Salum Al-Qassmy, Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mheshimiwa Pascal Degera, Mheshimiwa Bakari Faki, Mheshimiwa Felix Kijiko, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, Mheshimiwa Rosemary Kirigini, Mheshimiwa Suleiman Kumchaya, Mheshimiwa Ephraim Madeje, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mheshimiwa Balozi Dr. Getrude Mongella, Mheshimiwa Dr. James Msekela, Mheshimiwa James Musalika, Mheshimiwa William Ngeleja, Mheshimiwa Sigifrid Ng'itu, Mheshimiwa Richard Nyaulawa, Mheshimiwa Mwaka Abrahman Ramadhan, Mheshimiwa Profesa Philemon Sarungi, Mheshimiwa Peter Serukamba, Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir na Mheshimiwa Godfrey Zambi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa kutoa shukrani kwa Katibu wa Bunge, Ndugu Damian Foka pamoja na watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake vilivyo. *(Makofi)*

Aidha, napenda kumshukuru Ndugu Justina Shauri, Katibu wa Kamati hii pamoja na Makatibu Wasaidizi Ndugu Zainab Issa na Ndugu Patson Sobha, kwa kuweza kuihudumia vema Kamati na kuhakikisha kwamba maandalizi yamekwenda vizuri kufuata na taarifa hii ilivyotolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati inaunga mkono kwa dhati kuwasilishwa kwa Muswada huu kufika hapa Bungeni ambao wananchi wanasubiri kwa hamu kubwa sana. Kwa niaba ya Kamati ya Miundombinu, naomba kusema tunaunga mkono hoja hii mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Paul Kimiti, ahsante sana kwa kuwasilisha vizuri maoni ya Kamati ya Miundombinu. Sasa ni zamu ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Sekta hii ya Miundombinu. Karibu.

**MHE. BAKARI SHAMIS FAKI - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani napenda kuwasilisha maoni ya Kambi kuhusu Muswada wa Sheria ya *The Universal Communication Service Access Act, 2006* kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kifungu cha 43(5)(c) na 70(2) Toleo la 2004.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kushiriki tena katika shughuli ndani ya Bunge letu Tukufu tukiwa na afya njema ili kufanya kazi tuliyotumwa na Watanzania katika ujumla wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na mambo mengine yaliyoainishwa na Muswada huu, madhumuni makuu ya Muswada huu ni kuweka mwongozo, taratibu na usimamizi wa utoaji huduma za mawasiliano katika maeneo ya vijijini na ya mijini ambayo kutokana na sababu moja au nyingine yako nyuma kiuchumi. Hili ni jambo jema sana kusaidia maeneo yaliyo nyuma nayo yasiachwe bali yasaidiwe kupata huduma, sawa na maeneo yaliyo mbele kimaendeleo.

Aidha, Muswada pia unalenga kuanzishwa kwa Mfuko wa Maendeleo ya Huduma za Mawasiliano ili kuwafikia wananchi wengi, hususan wale waishio vijijini na kwenye maeneo ambayo hayana maslahi kwa misingi ya kibiashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani wakati inaunga mkono azma ya kupeleka huduma kwa wananchi wa kawaida inapenda kutoa tahadhari hasa ikizingatiwa kuwa azma kubwa ya Serikali ya Awamu ya Nne ni kuwaletea maisha bora Watanzania wote kuanzishwa kwa Mfuko huu kusije kukawa pia mzigo kwa wananchi walio wengi wa vijijini ambao tayari hali yao ya kiuchumi ni mbaya sana. Tunatoa tahadhari hii kwa vile, tumeanza kuwa na kansa ya kuunda mifuko karibu kwa kila jambo. Kambi ya Upinzani imefanya utafiti na kugundua kuwa:-

(a) Mifuko mingi iliyokwisha kutungiwa Sheria na Bunge hili haijaanza kazi ukiacha Mfuko wa Elimu. Inawezekana utekelezaji wa mifuko hiyo iko katika hatua mbalimbali ya utekelezaji, lakini Kambi ya Upinzani ingetegemea kuwa wakati Muswada inaletwa Bungeni tayari kuna *Implementation Plan* na hivyo isingetegemewa kuwa itachukua muda tena kwa Mfuko kuchelewa sana baada ya Sheria kupitishwa na Bunge. Mfano halisi ni Mfuko wa Umeme Vijijini, ambao wala hatujui utaanza lini.

(b) Kwa mujibu wa Kifungu cha 23 cha Mfuko unaopendekezwa vyanzo muhimu vya Mfuko huu ni pamoja na fedha zitakazoidhinishwa na Bunge. Hii ina maana ya kuwa kwa namna mmoja au nyingine, Mfuko huu bado utalenga kupata fedha zake kutoka kwa wananchi wa kawaida (walalahoi) kwa njia ya kodi mbalimbali za moja kwa moja au hata kwa kodi kupitia bidhaa mbalimbali. Mtanzania wa kawaida tayari analipa kodi nyingi. Kambi ya Upinzani ingetegemea kuwa Mfuko huu ungekuwa na ubunifu zaidi kuliko kurudi tena kwenye mifuko ya wananchi wa kawaida ambao wengi wao watazisikia tu bila kufaidi huduma yenyewe kama tutakavyoeleza hapa chini.

(c) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kifungu cha saba, Mfuko huu utasimamiwa na Bodi na Watendaji wa kila siku chini ya usimamizi wa Meneja. Uendeshaji wa Bodi hasa vikao ni gharama, ajira mpya zitakazotokana na Mfuko huu ni gharama, magari mapya ya watendaji wa mfuko yatahitaji kununuliwa bado ni gharama kwa Mtanzania wa kawaida. Ni dhahiri uundwaji wa chombo hiki unaambatana na gharama za lazima.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali iangalie upya suala hili la uundaji wa Bodi hasa ikizingatiwa kuwa tayari kuna Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano yaani *Tanzania Communication Regulatory Authority (TCRA).* Tunadhani ingekuwa busara kiuchumi na kiuendeshaji badala ya kuunda chombo kipya kingeundwa kitengo chini ya *TCRA* kwa malengo ya kusimamia mfuko huu. Sheria inayounda *TCRA* irekebishwe ili kuruhusu majukumu haya mapya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo tutakuwa tunatimiza azma ya kupunguza gharama na hivyo kuleta unafuu kwa mwananchi wa kawaida. Kwa kuifanya kuwa Idara, hatutakuwa na majukumu ya kununua vifaa vipya vya ofisi wala magari mengi yasiyo ya lazima bali yatatumika ya *pool* iliyoko na tutapata faida ya Taasisi kubwa yaani manufaa ya *economies of scale.*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani imefanya utafiti mdogo katika nchi jirani ya Uganda na kugundua kuwa wenzetu ni mfano wa kuigwa katika eneo hili. Uganda uanzishwaji wa mfuko umefanywa na Tume ya Mawasiliano ambayo kwetu inafanana na *TCRA* na kwa utafiti wetu majukumu yote ya msingi kama yanavyopendekezwa na Mfuko huu yameendelea kufanyika vizuri.

Mheshimiwa Spika, kukosekana kwa huduma za mawasiliano katika maeneo lengwa kunatokana na sababu ya msingi ya kuwa kipato cha wananchi ni kidogo sana. Kwa bahati mbaya, hali hiyo ya wananchi katika mengi ya maeneo hayo inaongezewa ugumu na hali ya miundombinu katika vijiji vyetu vingi. Kwa takwimu zilizoko, wananchi wanaotumia au huduma za umeme kwa nchi nzima hawafiki asilimia 10. Kambi ya Upinzani inadhani kuunda mfuko huu kwa peke yake si tiba ya tatizo hili la msingi. *(Makofi)*

(a) Kwa mtaji huu wa watu chini ya asilimia 10 kupata umeme, malengo ya Mfuko huu itakuwa vigumu kuyatekeleza mpaka pale asilimia kubwa ya vijiji vyetu vitakapopata umeme wa hakika, na wenye bei ndogo *(affordable)* ambao watu wa kawaida wataumudu. Vinginevyo, mtu wa kawaida atakuwa anachangia mfuko huu kuwanufaisha daima wenye nacho.

Kwa msingi huo, Kambi ya Upinzani ingependa kupata mkakati na ratiba kamili ya Serikali kupeleka umeme vijijini ili angalau wananchi wanapochangia mfuko huu kwa njia ya kodi zao wawe na matumaini kuwa siku fulani na wenyewe watapata huduma hii muhimu. Umeme ni msingi kwa mawasiliano ya uhakika.

(b) Mheshimiwa Spika, pamoja na umeme ili mfuko huu pia uweze kuwanufaisha wananchi wetu ni lazima kuwe na mtandao wa uhakika wa simu za mezani ili kufanya wananchi wa hali ya chini kumudu gharama za mitandao iliyopendekezwa kwenye Muswada. Kambi ya Upinzani inazo taarifa ya *service providers* waliofunga huduma zao katika baadhi ya Wilaya baada ya kushindwa kuhimili gharama kubwa zinazotokana na bei kubwa ya simu. Matumizi ya *Satellite* nazo kwa sasa pia ni gharama kubwa sana.

Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ieleze kwa kina ni mikakati gani itakayotumika kushusha gharama hizo ili wananchi wote watakapochangia mfuko huu kutokana na vianzio vya kodi wawe na uhakika wa kunufaika na huduma za Mawasiliano inayopendekezwa na Muswada huu. Vinginevyo hakuna faida ya kutunga Sheria ambayo itabaki makabatini kwa muda mrefu bila kuwanufaisha wananchi. *(Makofi)*

(c) Muhimu zaidi ni suala la mkakati wa uhakika wa kuboresha kipato cha Watanzania wa kawaida, mijini na vijijini.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa Watanzania wasiopungua milioni nne sasa wanazo simu za mikononi na au za mezani au zote kwa pamoja. Lakini utafiti mdogo tu unaonyesha kuwa sehemu kubwa ya wananchi hao wanatumia simu hizo kwa ku- *beep,* jambo ambalo kibiashara halina manufaa na wala si la kistaarabu sana. Lakini pia hii ni idadi ndogo sana ikilinganishwa na Watanzania wapatao milioni 36. Lakini ndiyo kielelezo cha Watanzania walio wengi wanapenda kuwasiliana, hawana uwezo, na hivyo njia pekee ni ku *beep* hatuwezi kuwalaumu. Lakini tutawaacha hivyo hadi lini. *Vision* 2025 inazungumzia kipato cha Mtanzania itakuwa dola moja ya Marekani ifikapo 2025.

Kwa utaratibu huo, uwezekano wa sehemu kubwa ya Watanzania wengi kunufaika na mawasiliano haya ni mdogo sana, pamoja na kuwa kila wanaponunua sukari, majani ya chai, chumvi, kiberiti,mafuta ya kupikia, kanga, bia, soda na kadhalika watakuwa wanachangia mfuko huu. Watakaonufaika ni kundi dogo la watakaokuwa nacho. Ili tupate manufaa basi ni lazima kuwe na mkakati mahususi unaolenga si tu kupunguza umaskini lakini kuinua kipato cha Mtanzania kiwe angalau zaidi ya dola 50 kwa siku ili angalau Mtanzania huyo aweze kumudu kwanza mahitaji ya kila siku chakula chake, matibabu yake, kisomo cha watoto wake, pamoja na mawasiliano. Vinginevyo mawasiliano yatakuwa kwa watu wachache tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivyo basi Kambi ya Upinzani kwa dhati kabisa inadhani ni bora Serikali ikaweka mkakati madhubuti wa kuwaongezea kipato wananchi ili waweze kumudu huduma hizo za mawasiliano, sambamba na usambazaji wa umeme vijijini ambayo ni nishati muhimu sana kwa utoaji na upatikanaji wa mawasiliano hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, isitoshe Kambi ya Upinzani inawasiwasi kama kweli utungwaji wa Sheria hii utaikomboa jamii husika, kwa kuwa mawasiliano tajwa yanaenda sambamba na teknolojia ya kisasa na teknolojia ya kisasa inahitaji jamii iliyoelimika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye *Internet Café* nyingi zilizoko hadi sasa, badala ya kunufaika na teknolojia hii ya mawasiliano *programs* nyingi zinazotumiwa na vjijana wetu zinatisha. Vijana wengi wanaangalia programu za ngono badala ya kutafuta programu za elimu au zenye manufaa. Hii kwa kiwango kikubwa inatokana na kiwango duni cha elimu ya vijana wetu. Mtandao unatumika kama burudani zaidi kuliko kuelimisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, tunapotunga Sheria hii, ni vyema tujiulize, je, ni kwa kiasi gani wananchi wetu hasa wa vijijini na wale wa hali ya kawaida watanufaika na huduma hii? Je tumejiandaa kwa kiasi gani kulinda maadili ya Taifa letu ambayo ni rahisi sana kubomolewa na mtandao huu ambao kimsingi hauna wala haujui na wala hautambui mipaka? Tunaweza kutunga Sheria hii, wananchi wakalipia mfuko huu, kumbe wanalipia kumaliza maadili ya watoto wao na hivyo Taifa katika ujumla wake kuathirika kwa kiwango kikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia kuna suala zima la lugha inayotumika na mitandao ambayo watu wetu wengi hawaifahamu. Kwa kiwango kikubwa ndiyo inayofanya vijana wengi kuangalia picha za ngono, kwani hiyo haihitaji kufahamu lugha fulani. Ni vyema tukayatafakari mambo haya yote kabla hatujatunga Sheria.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 19 kinazungumzia Mfuko kutoa Fungu la Fedha kwa *Universal Service Provider.* Lengo hili ni jema na lina nia ya kupunguza makali ya gharama ya huduma kwa mwananchi wa kawaida. Lakini uzoefu katika nchi yetu inaonyesha kuwa vyombo vyote binafsi pale vinapopewa fungu la fedha *subvention* kwa nia hiyo huwa havipunguzi gharama, au vinapunguza kidogo sana, kiasi kwamba maana halisi ya *subvention* inaondoka.

Kambi ya Upinzani ingependa Waziri aeleze kwa kina kabisa ni utaratibu gani atatumia kudhibiti fedha hizi za umma wanazopewa wafanyabiashara hawa kuwa hazitatumika vibaya na kweli zitawapunguzia wananchi makali ya gharama ya huduma hizo kama inavyokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa mfanyabiashara yeyote anapaswa kulipa kodi inayostahili. Hata hivyo kwa vile lengo ni kuwafanya Watanzania wengi inavyowezekana kunufaika na huduma hii muhimu, basi ni vyema Sheria ikatamka bayana kuwa kwa miaka kadhaa hapatakuwa na gharama ya leseni yaani *Universal Service Levy* na kiwango hicho anachosamehewa mfanyabiashara, ikiwa ni pamoja na kodi au ushuru wowote atakaosamehewa kwa vifaa vyovyote anavyoingiza nchini ni lazima kidhibitiwe vizuri ili kuwa na gharama ambayo itabaki ndogo kwa muda maalum ili wananchi wengi zaidi wanufaike na huduma hii.

Mheshimiwa Spika, vinginevyo, kama ilivyo tabia ya wafanyabiashara gharama zote za leseni, ushuru na kodi zitahamishiwa kwa mlaji/mtumiaji wa mwisho yaani *consumer* na hivyo kufanya gharama ya huduma kupanda mara kwa mara. Kwa makusudi kabisa, kuwe na *positive discrimination* katika jambo hili kwa nia ya kuwanufaisha Watanzania wa kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inadhani utaratibu unaotumika kuunda Bodi katika kifungu cha 7 kitakuwa na tatizo kubwa. Kwa mujibu wa kifungu cha 7(3) Mwenyekiti wa Bodi, pamoja na Wajumbe wote watachaguliwa na Waziri. Kati yao wako wanaoingia kwa kofia zao, wapo wanaoteuliwa kutoka wadau wa mawasiliano. Tatizo letu ni kuwa kwa kawaida Mwenyekiti anateuliwa na Rais na wajumbe wanateuliwa na Waziri. Lengo la mgawanyo huu ni uwajibikaji na mamlaka. Kifungu

hiki kinapendekeza wote wateuliwe na Waziri, ni dhahiri kuwa kunaweza kutokea mgongano kwa vile wote watajiona ni wateule wa mtu yule yule na hivyo wote kuwa wanalingana. *(Makofi)*

Kambi ya Upinzani inamtaka Waziri kufikiria upya jambo hilo ili kuwa na utendaji mzuri. Tunapendekeza aidha, Bodi imteue Mwenyekiti miongoni mwao katika kikao chao cha kwanza au Mheshimiwa Rais amteue Mwenyekiti kama ilivyo kwenye Bodi nyingi. Vinginevyo Waziri alieleze Bunge hili sababu za msingi ya badiliko hili. Kwa msingi huo huo, Kambi ya Upinzani inapendekeza tofauti na ilivyo kwenye kifungu cha 9, Meneja wa Mfuko huu ateuliwe na Bodi yenyewe kwa njia iliyo wazi ya ushindani kuliko kuteuliwa na Waziri. Hali ilivyopendekezwa kwenye Muswada huu inapoteza mantiki kabisa kuwa wote Bodi na meneja wanateuliwa na Waziri.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa baada ya kutoa maoni hayo, nitoe shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Waziri na timu yake kwa kuwasilisha Muswada huu muhimu .

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, kwa heshima na taadhima, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Bakari Shamis Faki ahsante sana kwa kutoa taarifa hiyo ya maoni ya Kambi ya Upinzani. *(Makofi)*

Sasa kama nilivyotangaza ninao wachangiaji wanne hadi sasa kwa mpangilio ufuatao wa kwanza ni Mheshimiwa Profesa Idris Mtulia atafuatiwa na Mheshimiwa Margareth Mkanga, Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi, Mheshimiwa Balozi Hamis Kagasheki, Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mheshimiwa Luhaga Mpina, Mheshimiwa Dr.Guido Sigonda na Mheshimiwa Felister Bura. *(Makofi)*

Basi hiyo orodha nitaifuata kama ilivyo. Kwa hiyo, sasa nitaanza na Mheshimiwa ProfesaIdris Mtulia, wakati huo Mheshimiwa Margareth Mkanga, ajiandae.

**MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA:** Mheshimiwa Spika, natoa shukrani kwa kunichagua niwe msemaji wa kwanza kwa Muswada huu. Vilevile naomba kwa kuwa hii ni mara yangu ya kwanza katika Kikao hiki kusimama na kuzungumza, naomba niwapongeze Mawaziri wote walionusurika katika mabadiliko ya Baraza la Mawaziri madogo yaliyofanywa na Mheshimiwa Rais, ningekuwa mimi lazima ningefanya kafara ndogo. *(Makofi)*

Vilevile naomba kuwapongeza wale wawakilishi wetu tuliowachagua kwa ajili ya kuwa Wabunge wa Bunge la *East Africa*. Vilevile naomba kumpongeza Katibu wa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi, Mheshimiwa Ali Ameir Mohamed, kwa kuchaguliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu na Wizara yake kwa nini, kwa sababu Muswada huu ni muhimu, Muswada huu umekuja umechelewa sana, lakini *better late than never*, Muswada huu ni ukombozi

kwa watu wetu. Mtakumbuka wenzetu nyie mnaokaa mijini labda mnaweza kusahau, lakini sisi tunaokaa vijijini nakumbuka wakati wa kampeni za uchaguzi niko Mkongo, ninawaaga familia yangu sasa nakwenda katika *area* ambako hakuna *communication* yaani unakaa kule siku tatu hujui nyumbani kwako kuna nini na wao hawajui wewe kimekutokea nini. Hii ni taabu kubwa, yaani inakufanya hata ile ari ya kutaka kuzungumza saa nyingine ukiwaza nyumbani wanafanya nini, basi huhemewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni kwamba kuna sehemu ya nchi yetu ni tajiri sana, mimi niliwahi kwenda Meatu kule kwa wale wenye ng'ombe na nikapita pale Katesh, Mikoa ile ni tajiri kwa ng'ombe. Lakini ukija Rufiji unakuta ardhi nzuri, maji mengi na hilo pori la Hifadhi ya Selous liko Rufiji zaidi, lakini ukifika kule maendeleo ni duni. Kwa nini, wawekezaji hawavutiwi? Jibu hakuna miundombinu kule na leo hii ukipeleka miundombinu Rufiji itafunguka na Tanzania nzima itafunguka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba sana nisisitize tu kwamba huu ukombozi umeleta haki na haki itazamwe. Ukitazama *Section No. 6* ya Muswada huu ukurasa wa 6, utaona panaulizwa namna ya kuchagua hao watoa huduma na namna ya kuchagua hizo *project* ziende wapi.

Mimi nadhani hapa tuna swali la msingi kabisa, ingekuwa tunafikiria kihospitali, tungefanya *survey,* tungepima wagonjwa wetu, tukajua nani anaumwa zaidi na hapa tungeomba Wizara ifanye *pre-service survey* wapate *database* itakayoonyesha sehemu gani ya nchi wanahitaji zaidi mawasiliano, hususan ya simu. Utaona waziwazi kule Rufiji nadhani tutakuwa wa kwanza. Kwa kweli bila kufanya hivyo, tutakuwa tunaimba wimbo tu, kwa sababu saa nyingine unaweza ukafikiria watoa huduma hizi wana ugonjwa wa kutazama *area* moja tu ya nchi hata kama wakielezwa na Muswada wenyewe kwamba Muswada huu uende vijijini kwa wale ambao wana mapato hafifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa mimi nilikuwa nadhani njia nzuri na ya haki ingekuwa tu tufanye kama Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi walivyosema, kila Kata iwe na Sekondari. Nilikuwa naomba Wizara ya Miundombinu ihakikishe kwamba wale watakaopewa nafasi ya kupata ruzuku hii, basi wahakikishe kwamba kila Makao Makuu ya Kata yawe ya kwanza yaani iwe *priority* kupata huduma hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nataka kurudi ili nizungumze juu ya gharama. Muswada mzuri kabisa unaniongoza kwamba gharama zake ziwe hafifu ili watu wengi wazimudu.

Mheshimiwa Spika, mimi nashangaa sana, kwa mfano, *per capital income* ya India, *UK*, *US* na nchi nyingine za Ulaya ni juu sana kuliko *per capital income* ya Tanzania. Lakini gharama ya kupiga simu katika nchi ambazo ni matajiri ni rahisi sana mara tano hata kumi kuliko kupiga simu katika nchi yetu hii. Sasa ukombozi umekuja, pesa tunatoa sisi, Bunge linaunda mfuko. Tunataka tuhakikishiwe kabisa kwamba hao watakaopata fedha hizi na huduma hizi, tafadhali wazifikishe huduma zao kwa gharama nafuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Muswada huu ndio njia bora tu ya kuhakikisha kwamba watu wetu, sasa ugumu wa kufanya biashara utaondoka. Gharama kubwa za mawasiliano imefanya makampuni mengi washindwe kufanya biashara. Unaweza ukazungumza kwa hela zako, *at per* dola tano ukiwa Ulaya utazungumza kwa muda mrefu zaidi kuliko dola tano ukiwa hapa Dar es Salaam. Kwa hiyo, nadhani tumeshafikia ufumbuzi huu. Naomba sana watekelezaji wawe makini ili tuopate faida ya Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho ninaomba nitazame *Section 7, page 3*, ule uteuzi wa Bodi, ukitazama kwamba Muswada huu fedha nyingi itatoka katika Bunge hili. Lakini Bunge hili hatuwakilishwi! Uteuzi wa Bodi haina Mbunge hata mmoja! Hivi Serikali haituamini? Hivi Serikali tumeikosea nini? Tunapitisha sheria, tunaipa fedha Bodi, hiyo lakini sisi tusiwemo! Kwa hiyo, naomba jambo hili lifikiriwe tena na lifanyiwe mabadiliko kwamba wajumbe watakaokuwa katika Bodi hiyo, na Wabunge nao wafikiriwe wapate nafasi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Ahsante sana! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia moja. *(Makofi)*

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili nichangie Muswada ulio mbele yetu. Lakini kabla ya hapo ningependa kuwapongeza Wabunge wawakilishi wote ambao sote tulishiriki kuwachagua hapa waweze kwenda kutuwakilisha huko mbele ya safari ndani ya Afrika Mashariki, nikitegemea kwamba wao ndio watakuwa Mhimili wa kuweza kuchanganua yale yote yanayohusika ili tuweze kufika huko kwenye Shirikisho la Afrika Mashariki tunalolitegemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zaidi ya hapo ningependa kutoa pongezi kwa Katibu Mpya wa Kamati ya Wabunge wa Chama Cha Mapinduzi, nikiamini umahiri wake utatufikisha mahali pazuri kwa kuwa daraja na mshenga madhubuti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo, ningependa kutoa pongezi kwa Waziri wa Miundombinu, Manaibu wake, Watendaji wa Wizara hii nzima kwa kutuandalia Muswada ambao naamini punde utaweza kuwa Sheria, Muswada ambao umezingatia mengi aliyoyasema kwamba ni kuleta maendeleo ya Mawasiliano katika nchi yetu katika sehemu za Simu, Posta, Utangazaji, Tovuti, Barua pepe na mengineyo yote yale tena kwa bei nafuu sana kwenye maeneo ya vijijini na maeneo ambayo hayana vivutio kwa biashara mbali mbali tena kwa wananchi wote bila ubaguzi wala kuleta hitilafu yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi katika Muswada huu nitajikita kwenye ukurasa wa 10, *part 4* na nadhani mwendelezo wake ukurasa wa 11. Nikianzia na ukurasa wa 10, (b) kibano kidogo huko chini walikosema *reasonable geographical access to public of call boxes across…*

Mheshimiwa Spika, hiyo nimeishukuru sana kwa sababu Muswada umekwisha elekeza kabisa kwamba huduma hii ya *call boxes* itabidi ienezwe Bara na Visiwani ili kuweza kuleta uharaka wa huduma za mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, mimi hili naona ni ukombozi mkubwa kwa sababu mawasiliano ni moja ya nyenzo za kuharakisha maendeleo ya kiuchumi, utamaduni, teknolojia na yote yale, hasa katika ulimwengu huu wa utandawazi ambapo sasa hivi au kwa kutimiza sheria hii itakapoanza kutekelezeka, biashara watu wataendeleza kuzifanya kwa simu wakijua kabisa mzigo wa bidhaa fulani unasafiri leo saa kadhaa kwa urahisi zaidi kuliko ambavyo mambo yanafanyika sasa.

Mheshimiwa Spika, kingine ambacho kimeweza kunifariji katika Muswada huu, ukurasa wa 11, nimefarijika sana Muswada ulipotaja wazi wazi kabisa kwamba huduma hizi zinapaswa zitolewe kwa kujaribu kufikia kwa urahisi zaidi watu wenye ulemavu kwa kiwango sawa na wananchi ambao hawana ulemavu. Ukurasa wa 11! Kwa kweli niseme ni Muswada wa kwanza au nadhani sheria ya kwanza ambayo nimeona watu wenye ulemavu wametajwa kinaganaga. Kweli kabisa! Hili mimi nalipongeza na kwamba ninachoomba ni kuona utekelezaji wa suala hili ukifanyika kweli kikamilifu na kwa haraka iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimkwa Spika, sasa katika hili ningeomba kusisitizia kwamba hawa watoa huduma ambao watapata fedha au ruzuku kutoka Serikalini waendelee kubanwa kuzingatia haya yaliyoandikwa, maana vinginevyo inaweza ikawa ni maandishi, lakini wala wasijali. Mimi nasema hata katika kanuni, moja ya kipengele kitakachomwezesha mtu kupata ruzuku kutoka ile *Fund* tunayoitengeneza, ni atatekeleza vipi suala hili la ku-*provide services* hizi vizuri hata kwa watu wenye ulemavu na wazee na wengine wote. Iwe ni moja ya masharti, licha ya kuangalia ile *Policy* yake, kwa hiyo ndani ya *policy* hilo likae wazi kabisa, ndiyo itakuwa rahisi kabisa kufuatilia utekelezaji wa suala kama hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba sifahamu hili utekelezaji wake utakuwaje, lakini mimi ningependa kushauri, hao watoa huduma wasisitizwe kabisa kwamba wanalazimika kuwa na watalaam, kwa mfano, wa lugha za alama. Kama ni watangazaji, kwa mfano *TV,* wamepewa ruhusa sijui ya kutangazaje huko. *TV* kwa viziwi, ataona tu lakini hatajua nini kinasemwa mpaka pawe na mtafasiri wa lugha ya alama. Kwa hiyo, vitu kama hivi lazima wakumbushwe waweze kuvifikiria hata kabla hawajajiingiza katika biashara kama hii.

Mheshimiwa Spika, huduma hizi za mawasiliano zitatolewa kwenye *call boxes,* kwenye *Internet cafes* huko na mambo yote ambayo tumeelezwa. Hapo pia ningependa wasisitizwe, majengo na sehemu ambazo huduma hizo zitatolewa, lazima ziwe muafaka kwa watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, ngazi za kupanda katika majengo haya inakuwa ni matatizo kwa aina fulani fulani za ulemavu. Hata watu wazima, wazee kupanda na mikongojo inakuwa ni tatizo. Kwa hiyo kwa kukwaza namna hiyo, mafao au manufaa ya Muswada

huu ambao kweli ni kurahisisha mawasiliano haitakuwa sahihi kwa sababu wengi watakosa.

Mheshimiwa Spika, kuna matatizo tena mengine. Ili mawasiliano haya yaweze kufaidisha wananchi wengi kama Muswada unavyosema, ningeshauri, simu kwa mfano hizi za mkononi, labda Bodi itakayohusika na mambo haya au sijui *TCRA,* iweze kufanya ka-*survery* na *research* fulani. Aina ya simu hizi tunazotumia za mikononi ambazo *keyboards* zake ni *flat*, kwa watu wasioona inakuwa vigumu kuzitumia. Sasa sijui kuna utalaam kwamba hata *keyboards* hizi zinaweza zikawa za vinundunundu kusudi wenzetu wasioona inakuwa rahisi kupapasa na akapiga simu mwenyewe. Kwa hiyo hayo yanapaswa kuzingatiwa katika sheria hii ambayo utekelezaji wake kwa kweli utakuwa wa manufaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimefarijika na Muswada huu na ninaamini itakuwa ni sheria kwamba gharama kama wenzangu walivyozungumzia, zitakuwa pungufu kwamba hata watu wasiojiweza, hata watu ambao wana kiwango cha chini cha kipato, wataweza kumudu gharama za kutumia mawasiliano hayo. Sasa hili mimi sifahamu kwamba tutafanya vipi licha ya kwamba tunatumia ruzuku. Tutashusha shusha vipi hizo gharama mpaka kweli ziweze kutumika kwa watu wengine kwa muda mrefu kama mwenzangu alieyetangulia alivyosema, Tanzania upigaji wa simu umekuwa gharama na wengi wamekuwa wakilia hivyo. Huenda ndiyo maana hata wenzetu wa Kambi ya Upinzani wamesema, wengine wanaishia ku-*beep beep* ili wewe unayepokea ndiye uingie hiyo gharama ya kuweza kuzungumza naye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hili sifahamu tutashushashusha vipi pamoja na kwamba wataweza kupewa hizo ruzuku. Lakini bado kunaweza kukawa na vipengele watakavyovitumia hao watoa huduma kuweza kutokukubaliana sawa sawa au kutoweza kutekeleza sawa sawa suala hili la kupunguza gharama kwa watumiaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Muswada huu ni mzuri, lakini kidogo labda ningeweza kujaribu kusisitiza kwamba matumizi ya sheria hii tutakapoiunda, utekelezaji wake unaweza ukawa mgumu endapo miundombinu ya umeme haitaenda sambamba na hili vijijini. Kwa sababu *Internet* inahitaji umeme. Mambo mengi tu ya kisasa haya yanahitaji umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kiwango cha umeme ambacho kwa kweli mpaka sasa tumeshaweza kufikisha huko vijijini nadhani ni kidogo kuliko hamu ya kuweza kufikisha mawasiliano haya mpaka vijijini. Sasa hii inakwenda kwendaje. Nashauri labda sasa *speed* iende kwa pamoja kwamba suala la umeme liwe haraka ili hata sheria hii tutakapoiunda iendane sawa sawa. Vinginevyo, Muswada huu na utekelezaji wake itabidi usubiri, kusubiria maendeleo ya umeme kwenye vijiji vyetu. Kwa hiyo hilo liangaliwe, ama tuharakishe vyote viwili. Lakini kwa ujumla Muswada huu ni mzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, mimi niseme kwa ujumla naunga mkono Muswada huu na hata sheria ambayo tutaweza kuafikiana nayo kwa sababu kwa ujumla wake utatuwezesha kusonga mbele kwa maendeleo ya nchi yetu katika nyanja

mbali mbali. Lakini ninaloomba ni utekelezaji wa haraka, kanuni zilizo wazi, kanuni zitakazoweza kuwaelekeza na kutoa mwongozo mkamilifu kwa watoa huduma kwamba wasikiuke maagizo yaliyopo katika Muswada huu ambao baadae utakuwa sheria.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono Muswada huu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Margareth Mkanga, ahsante sana na pongezi sana kwa jinsi unavyotetea kundi muhimu katika jamii, kundi la walemavu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii. Mimi nitazungumzia kwenye masuala mawili tu. *(Makofi)*

La kwanza napenda kuunga mkono hoja inayoletwa mbele yetu kutokana na umuhimu wake. Hoja hii ukiacha matatizo ya umeme yaliyozungumzwa na mzungumzaji aliyepita, kwa kweli imekuja kwa kuchelewa! Lakini nilitaka niainishe umuhimu wa mawasiliano sehemu za vijijini hasa sehemu za pembezoni mwa nchi yetu kwa kutoa mifano miwili.

Mheshimiwa Spika, mfano wa kwanza mimi natoka Mkoa wa Iringa na nimefanya utafiti sana katika Mkoa ule na najua jinsi wananchi wa Iringa Vijijini na hasa maeneo ya Kilolo, Kalenga walivyoweza kufaidika na mawasiliano ya simu hizi za kisasa kwenye masuala ya kilimo cha mboga mboga.

Mheshimiwa Spika, wameweza kujenga uchumi mzuri sana, wanazalisha mboga mboga nyingi sana ambazo zinauzwa Jijini Dar es Salaam. Lakini kilichowasaidia kwa kweli ni mawasiliano ambayo yanawawezesha kujua bei za wakati huo huo zinazoweza kupatikana kule kwenye Soko la Kariakoo Jijini Dar es Salaam. Hii imewasaidia wananchi wale kuongeza kipato chao na uchumi wa maeneo yale kwa ujumla. Kwa hiyo, ni kweli kabisa mawasiliano ni kitu cha muhimu sana, kinaeleta maendeleo ya haraka katika maeneo ambayo uzalishaji unaweza ukaisaidia nchi hii na hasa maeneo yaliyo pembezoni mwa nchi na yana uwezo wa kuzalisha mazao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mfano wa pili, mwaka jana wote tunakumbuka tulikuwa na uhaba wa chakula ambayo ilitokana na ukame. Tuliona jinsi Serikali yetu ilivyoingilia suala la kununua chakula kwa ajili ya wananchi wetu ili kuziba pengo la chakula hapa nchini. Msimu huu maeneo ya Nyanda za Juu, Rukwa, Iringa na Ruvuma, wamejitahidi sana wananchi wale kulima mahindi na mazao mengine ya chakula. Lakini juhudi zao hizo ilipofika kwenye kuuza, sisi wabunge tumejitahidi kuwahimiza wananchi wale wasiuze mahindi yale kwa walanguzi, wawauzie *SGR*. Tatizo limekuja kujitokeza kwamba *SGR* kwa kweli wameshindwa kununua mahindi yale na wananchi wana mahindi mengi kule vijijini, mengi sana. Sasa wananchi wale, na mvua inaanza kunyesha kule Rukwa, kule Ludewa, kule Ruvuma, wanashindwa kuelewa mahindi yale watafanya nayo nini, na mahindi yale mengine yalinunuliwa yameshindwa kusombwa kwa sababu ya kukosa fedha. Mimi najua Serikali imekuwa ikifanya juhudi kupata pesa za kuweza kununulia mahindi yale.

Mheshimiwa Spika, lakini wananchi wa sehemu zile hawana mawasiliano. Mawasiliano kule ni duni, hakuna. Wanatapatapa, wanakata tamaa na inawezekana kabisa kutokana na ucheleweshaji wa fedha ambayo Serikali ilitakiwa iwe imeshatoa sasa hivi, kuchelewa huko kutawafanya wananchi wakate tamaa na pengine msimu huu unaokuja wasiweze kulima na kuzalisha chakula kwa ajili ya msimu ujao. Lakini haya nasema ni matokeo ya mawasiliano duni, mabaya kwenye maeneo yetu ambayo tunayategemea sana kwa kuzalisha chakula kama maeneo ya Nyanda za Juu, Rukwa, Ludewa na hata maeneo ya Ruvuma.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi naona Muswada huu umekuja kwa wakati wake, tuutekeleze ili iwe sheria, tuhakikishe kwamba wawekezaji na watu binafasi wanajitokeza kuwekeza kwenye maeneo haya ili wananchi wetu waweze kutumia mawasiliano ya kisasa kujua yanayoendelea maeneo mengine ya nchi, kujua mipango ya Serikali ambayo inaendelea ili waweze kuwa na uhakika pengine na mambo yao ya maendeleo kwenye vijiji vyao. Hili nilitaka kulizungumza kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, juzi juzi hapa tumezungumzia kuhusu umuhimu wa kufanya *regulatory impact assessment* na tumehimizwa Waheshimiwa Wabunge tuhakikishe Miswada inayoletwa na Sheria zinazotungwa, ziambatanishwe na *report* inayoonyesha mchakato wa athari na faida zinazoweza kutokana na sheria tunazozitunga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii sheria tunayotaka kuitunga ni ya muhimu sana. Najua itakuwa na faida nyingi sana. Lakini maswali mengi hapa yameulizwa na Kambi ya Upinzani, maswali yameulizwa na aliyetoa mapendekezo ya Kamati na wazungumzaji wenzangu wawili waliopita wamelizungumzia vile vile, kwamba kunaweza kukawa na athari za sheria tutakayoitunga. Lakini najua kunaweza kuwa na faida kubwa.

Mheshimiwa Spika, sasa *regulatory impact assessment* inasaidia kuainisha mapema kabla Muswada au Sheria haijaanza kufanya kazi. Inasaidia kuonyesha athari na faida zinazoweza kutokana na sheria tunayoitunga ili tuweze kuchukua hatua mapema kurekebisha makosa na kasoro ambazo zingeweza kujitokeza kwenye Muswada au kwenye sheria kabla haijatungwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ningependa kutumia Muswada huu ili kwa mara ya kwanza Serikali, Wizara ijitahidi kuufanyia Muswada huu, sheria hii tunayoomba tuipitishe ifanyiwe *regulatory impact assessment* ili ijibu maswali, wasi wasi uliotolewa na Waheshimiwa Wabunge waliochangia kupitia Kamati na kupitia upande wa Upinzani, tupate majibu bayana ili athari zile tuweze kujua namna ya kuzitatua na kurekebisha matatizo mapema kabla sheria haijaanza kufanya kazi. Ni bahati mbaya unaweza ukawa ni Muswada wa kwanza, kufanyiwa *RIA* lakini kila kitu kina mwanzo.

Mheshimiwa Spika, hatujachelewa, Muswada huu una *criteria,* vigezo vilivyozungumzwa vya kufanyia *audit assessment* humu. Kama tunaweza kuzungumzia mambo ya *audit* kwenye kipengele Na. 25, kwa nini basi tusifanye na *regulatory impact assessment*. Hivi vitu viwili vinaenda pamoja, na kwa kweli ukifanya *regulatory impact assessment* vizuri, utakapokuja kufanya *auditing* hapo baadae *(Performance Audit)* unatumia mambo yaliyopitishwa, yaliyokubaliwa, yaliyoonekana kwenye *regulatory impact assessment report*, unatumia kufanya *audit*. Kwa hiyo, *audit* yako inaweza kuwa bora zaidi kwa sababu huku mwanzo mlifanya *regulatory impact assessment*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi naomba sana tutumie Muswada huu na naomba Mheshimiwa Waziri akubali. Wataalam najua wapo, kazi siyo ngumu sana inaweza ikafanywa mara moja, tukaweza kuambatanisha kwenye Muswada huu *regulatory impact assessment report* inayoonyesha jinsi athari zitakazoweza kutokana na

sheria itakayoundwa, lakini hata faida jinsi zinavyoweza kuboreshwa zikawa faida nyingi kubwa zaidi na jinsi haya yanavyoweza kushughulikiwa. *(Makofi)*

Mheshimwa Spika, ningeshukuru sana kwa hilo kama Mheshimiwa Waziri angeweza kuzungumzia na pengine ku-*take note* ili lihusishwe kwenye Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ya kwangu yalikuwa ni hayo mawili. Naunga sana mkono hoja hii kwa sababu ni muhimu kama nilivyosema itawasaidia wananchi walio maeneo ya pembezoni. Nataka nirudie kwa kusisitiza kwamba kungekuwa na mawasiliano kwenye vijiji vya Ludewa, Rukwa, Ruvuma, leo hii wananchi wale hawangekuwa wanababaika kwa sababu hawajui kama Serikali yao inafanya juhudi za kutafuta fedha kwa ajili ya kununua mazao yao, mahindi yao. Lakini kwa sababu hakuna mawasiliano, wanaweza wakakata tamaa na wasiweze kuzalisha tena chakula msimu ujao kwa sababu ya kukosa mawasiliano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuunga mkono hoja hii. Ahsante sana! *(Makofi)*

**MHE. BALOZI HAMIS S. KAGASHEKI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii.

Kwanza, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri, Mheshimiwa Andrew Chenge, kwa mawazo yake aliyoyatoa wakati anatoa hoja yake hapa katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, pia, nataka kusema kwamba nashukuru nimeona *schedule of amendment* ambayo wamei-*table* leo asubuhi. Inasaidia kutoa wasi wasi katika baadhi ya maeneo. Lakini bado yako mengi ambayo ningependa niyazungumzie kwa idhini yao. *(Makofi)*

Mheshimwa Spika, la kwanza, naamini kabisa kwamba kuwa na Sheria ama kuwa na *Bill* hii ambayo tuliyonayo na tukaipitisha, siamini kabisa kwamba hiyo peke yake ndiyo itakuwa imesadia katika kutatua tatizo la mawawiliano katika maeneo ya vijiji katika Tanzania yetu hii. Na tatizo kwa kweli siyo kwamba kulikuwa hakuna sheria ama kulikuwa hakuna utaratibu lakini nadhani yako mengi ambayo yamepitishwa lakini kumekuwa hakuna *assessment* yoyote ya kujua *impact* ya maamuzi ambayo yalipitishwa hapo nyuma, lakini tunajikuta kila mara tunakuja na maamuzi ambayo ni maamuzi mapya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kuhusu suala hili ambalo linazungumziwa na umuhimu wake kwangu mimi sidhani kama ni suala jipya kwa sababu tangu mwaka 1993 wakati Bunge lako tukufu, lilipotazama hili suala lote la *communications* katika Tanzania nzima zilipitishwa *Acts* mbalimbali. Kwa mfano, mwaka huo wa 1993 na hii ameisema Mheshimiwa Andrew Chenge hapa kulipitishwa kwa mfano *Tanzania Communications Act No. 18,* kulipitishwa *Tanzania Telecomunication Company in Cooperation Act No. 19,* kulipitishwa *Tanzania Post Operations Act No. 20* na *Tanzania Broadcasting Act No.*

*6.* Kutokana na hizi *Acts* kumekuwa na vyombo mbalimbali ambavyo vimewekwa kutazama masuala haya ya *communications* na pia kutazama masuala ya Watanzania wanaweza wakahudumiaje katika masuala haya yote ya *communication*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa vizuri kwamba mwaka 2001 wakati *TTCL* ilipokuwa *partially privatized* utakuta ile 35% ya *shares* za *TTCL* zilikwenda katika *MSI International* pamoja na *DEDCON,* Kampuni ya Ujerumani na 65% ikawa *retained* na Serikali. Lakini la muhimu hapa wakati wa hii *exercise* ilipokuwa inafanyika ni kwamba Serikali ilikubali na *MSI* na hawa jamaa walikubali kwamba wataweka 800,000 *additional lines Tanzania.*

Mheshimiwa Spika, lakini kilichotokea ukitazama katika miaka minne ambayo walikubaliana kwamba hizi *lines* zitakuwepo tumekuja kugundua ni *line* 80,000 peke yake ambazo zimewekwa kwa hiyo, tunachosema ni kwamba utaratibu haukuwepo wala hili tatizo siyo kwamba halikujulikana lilikuwepo na *commitment* ilikwishafanywa na Serikali ilifanya *commitment* kwamba itaweka *additional lines* lakini katika hizo 800,000 zilizoweza kufanywa katika kipindi hicho mpaka sasa ni *lines* 80,000 peke yake.

Mheshimiwa Spika, ukitazama kufuatana na uamuzi huo ilikuwa pawepo na *public pay telephones* Tanzania ambazo zingekuwa ni 23,000 lakini zilizowekwa tangu wakati huo mpaka sasa hivi ni 2000 peke yake. Hizi zilikuwa shabaha ni kupanua na kukuza mawasiliano katika Tanzania. Sasa hatuambiwi kwa nini haya hayakufanyika, lakini sasa tunaambiwa kwamba tukiweka hii *fund* tuwe na uhakika kwamba hata haya yatafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini mimi siamini kwamba hiyo ni kweli kwa mfano ukitazama katika upande wa *cellular phones* huu upande wa hizi *handsets* za *telephone* utakuta Tanzania tuna *four service providers* katika hii, wako wakubwa wanne. Kuna akina *Vodacom*, kuna *Celtel*, kuna *Zantel* kuna *tiGO*. Lakini ukitazama *service* ambayo wanaitoa na *cost* ambayo wanaitoa katika Tanzania uki-*compare* na Kenya, Kenya wana *service providers* wawili peke yao. Lakini *cost* katika Tanzania *not with standing* kwamba tuna makampuni manne ambayo yanatoa hii *service* bado gharama yake ni kubwa katika Tanzania kuliko *any country* katika *East Africa* na ni kubwa katika nchi yoyote katika *COMESA*. Huu ni ukweli sasa unajiuliza kwa nini katika hizi nchi nyingine zote hii gharama inakuwa chini, lakini katika Tanzania inakuwa ni kubwa?

Sasa ukitazama kwa sababu ya gharama hizo na mimi nasema kwamba suala siyo kwamba uweke sheria hii, uweke mfuko huu, basi hapo *automatically* Watanzania watakuwa wamefaidika na hapo *automatically* Watanzania watakuwa wamekuwa *access* katika *communication* hapana, nafikiri matatizo yako *more fundamental* kwa kweli iko haja ya kutazama kwa undani zaidi.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri, atazame hili kwa nini gharama katika Tanzania ambapo ungedhani kwamba kwa kuwa tuna *operators* wanne, *competition* ingekuwa kubwa zaidi. Kenya wana *operators* wawili lakini gharama zao zinakuwa ni ndogo. Sisi na Kenya tulianza wakati mmoja, lakini Kenya unakuta kwamba

wanao wateja wengi zaidi kuliko hata Tanzania. Kwa mfano Tanzania mimi *statistics* nilizokuwa nazo na Waziri anaweza akanisaidia labda lakini katika *population* ya Tanzania ya watu milioni 36 tulivyo sasa hivi wanasema kwamba ni milioni mbili peke yao ambao *actually* unaweza ukasema *sustain subscribers* katika mtandao wa hizi simu za mkono. Kwa hiyo, mimi nasema kwamba tatizo siyo kwamba tukiweka sheria hii itasaidia. Kweli inaweza ikasaidia lakini yapo bado yako matatizo ambayo ni muhimu ndani ya Serikali yetu, yako matatizo muhimu ndani ya utazamaji wa hivi vyombo vinatumika vipi na *services* zinakwendaje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bado kuna matatizo ya *equipments* zenyewe. Kwa mfano, hizi *telephones* ambazo zinaletwa hapa Tanzania sidhani kama Serikali inazitazama kuona kwamba ziko katika *standard,* unakuta watu wananunua hizi *telephones* za mkono baada ya mwezi, miezi miwili zimekuwa ni *counter fade* lakini *of course* zinakuja zinaingia Tanzania, hiyo ina- *apply* katika Tanzania *PC* ambazo huwa tunatumia katika *laptops* ambazo watu wanatumia *even* katika *radio* ambazo watu wanatumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi nasema kwamba yako mambo ya msingi ya kuweza kutazama kabla hatujasema kwamba tukipitisha hii sheria kweli itaweza kwa sababu haya mambo yamekuwepo siyo kwamba ni mageni ama ni mapya. Lakini sasa tunasema kwamba tukiweka huu mfuko itaweza kutusaidia. Lakini yako mambo ya kutazama. Kwanza, fedha zitatoka wapi ambazo zitakuwa katika huu mifuko? Ukitazama huu mfuko ambao tunataka kuuweka tayari tunazungumzia kwamba tutakuwa na meneja, tutakuwa na wafanyakazi gani kwa maana nyingine ni kwamba zile fedha nyingi zitakwenda katika utendaji, zitakuwa katika *overhead costs* lakini hazitakwenda katika kuwasaidia watu kama lengo lilivyo. Mimi nadhani hii *operation* nzima sioni kama kungekuwa na ubaya wowote kama ingekuwa hata chini ya *Tanzania Communications Regulatory Authority* kwa sababu hii *authority* bado ina majukumu ya kutazama mambo mengi, ku-*regulate* mambo ya *postal services*, mambo ya *radio, electronic communications* na kadhalika. Kwa hiyo, badala ya kufungua kitu kipya kabisa tungeweza tukaweka hii chini ya *authority* na hii *authority* ingeweza na *in fact authority* ina fedha kwa sababu inapata fedha kutoka katika *operators* mbalimbali ambao wana-*operate* katika nchi yetu hii. Lakini sasa ukija upande wa fedha tunasema kwamba Bunge litoe fedha liweke katika *fund* halafu tunasema wafadhili wema wajitokeze waweke fedha katika *fund*, sidhani kama tutakwenda namna hiyo na mimi ndivyo ninavyoiona.

Mheshimiwa Spika, nikienda haraka haraka katika *Act* yenyewe sasa, *Act* yenyewe nina matatizo mimi. Nashukuru Mheshimiwa Waziri, ametoa *amendments* zake kuhusu mambo mbalimbali katika *Act* hii lakini bado katika upande wa *interpretation* wa hii *Act. Act* inavyoanza kwa mfano *Part I, clause (2)* inasema *act* hii ita-*apply to both Tanzania Mainland and Tanzania Zanzibar.* Halafu hapo hapo inakwenda katika *the following sub-clause* ambayo inasema *with respect to broadcasting this Act shall not apply to Tanzania Zanzibar*. Lakini suala langu la msingi hapa ambalo nauliza watusaidie wanapozungumzia juu kuhusu *with respect to broadcasting exactly* wanazungumzia nini *by definition,* wanazungumza *traditional broadcasting?* Kwa sababu *broadcasting* ina maeneo mbalimbali ambayo sasa hivi ukitazama kuna *web casting for example* ambayo

*actually* imekuwa ni kitu kikubwa na watu wana-*communicate through the web*, kuna *cable casting* na watu wana-*communicate through cable system*.

Kwa hiyo, ningependa kama Waziri angeweza akatupa *a clear definition of what do they mean* kama hapa wanazungumzia juu ya *traditional broadcasting* ama wanazungumzia *broadcasting in its broader sense* hiyo ni ya pili, ya tatu, katika *definition or interpretation rather of this Act* katika *clause* namba tatu mimi ningependa watu *exactly what do they mean, interpretation* yao ya *access*. Kwa sababu naona wametuwekea *communication services,* wamezungumzia juu ya *interpretation* ya *universal services*. Lakini hatukupata *interpretation* ya *what do they mean by the access.* Kwa sababu *access* ina *two ways, way* moja kwa *consumer* na *way* moja kwa *suppliers*. Sasa mimi nafikiri ingekuwa vizuri kama tungeweza tukapata hiyo. *(Makofi)*

La nne, ni kwamba hii *Act* wameweza kufanya mabadiliko *(changes)* kidogo. Lakini kuhusu Bodi, Bodi mimi ningeomba kwamba unapozungumzia kwamba kutakuwa *representative* wa Wizara mbalimbali kwa kweli nafikiri hii imepitwa na wakati. Hapa *what you need* unataka watu ambao ni *competent people who are experts in the field you don't need bureaucracy from the Ministry.* Wanaweza wakaingia pale kama *ex-official fine* lakini unataka upate watu ambao ni watalaam katika maeneo haya ambayo wanaweza wakatusaidia sisi wakati wamekaa katika hiyo Bodi na wakaweza kufanyakazi kwa niaba ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, halafu nikitazama suala la *Manager* wa *fund of course Manager* wa *Fund* sasa hivi naona wame-*move* hapa *amendment* atakuwa anachaguliwa *by the Minister in consultation with the board.* Lakini inapokuja katika *duration and of stay* ya *tenure* ya *manager* wa *fund* kwa kweli mimi nilikuwa naomba awe na *term* ya miaka mitano *apart in additional term of* miaka mitano *and the sit in other words* apate *term* ya miaka kumi. Lakini kusema kwamba anaweza kuwa pale *and each time* hii *term* yake inakuwa *renewed* nafikiri tuweze kutazama utaratibu mpya kwa sababu huku wanasema kwamba *this will be a cooperate thing* kwa hiyo *being a cooperate thing to moving away* katika utaratibu wa mambo jinsi ambavyo tunavyoyafanya.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 10 anapozungumzia juu ya *clause* namba 12 hiyo wameifanyia *amendment* namshukuru Mheshimiwa Waziri. Lakini hapa 12 (a) anazungumzia kwamba mtu anaweza akatolewa kwamba akiwa *declared bankrupt*. Sasa *who is to be declared bankrupt* kwa sababu tunasema katika Bodi tutakuwa na watu kutoka katika Wizara, tutakuwa na *different representative from the Ministry*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa *we referring to the service providers* ambao watakuwa katika *board* kwa kweli mimi sielewi maana yake hii ni nini? Haya mengine naweza kuelewa ya *criminal records, conflicts of interest*. Lakini hiyo kwa kweli sijui, ningeweza kupata ufafanuzi wako ingeweza ikanisaidia zaidi. *(Makofi)*

La mwisho naona muda wenyewe unakwenda kwa haraka zaidi. Mimi kusema kweli siko *comfortable* kwamba hiki kitu kitatekelezwa vizuri kwa sababu *already decisions* zimekuwepo zamani ambazo hazikutekelezwa. Lakini *of course* kwa kuwa

Kamati imeweza kupitia na wenzangu wengi wanaona kwamba ni jambo ambalo linafaa na ninasema kwamba siyo *the absence of the law* ndiyo kwamba hakuna *communications* katika *rural areas*. Lakini nafikiri kumekuwa *lack of implementation of some of the laws that we have already* na kwa hiyo, ukisema kwamba tunasema tunaweka sheria nyingine, utaratibu mwingine na *fund* hiyo itasaidia katika kusukuma maendeleo, *it remains to be seen.* Lakini kubwa zaidi kama alivyosema mwenzangu pale mwisho ni kwamba labda wakafanya *assessment* itaweza kutu-*convert* na *converse* zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kukushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kutoa mchango wangu mfupi kwenye Muswada ulioko mbele yetu kwa kuzingatia kwamba mimi ni Mjumbe na siyo mjumbe tu na ni Mwenyekiti wa Kamati ambayo imeshatoa maoni yake. Lakini ningependa kuchangia maoni yangu kama Mbunge na kusisitiza baadhi ya mambo ambayo naona yanafaa kusisitizwa. Kwa hiyo, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Lakini niipongeze sana kazi nzuri iliyofanywa na Kamati na hatimaye kuweza kuwasilishwa vizuri na Mheshimiwa Paul Kimiti, kama ulivyomsifia wewe mwenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Andrew Chenge na wasaidizi wake wote wawili pamoja na Katibu Mkuu na watendaji wote kwa ujumla kwa maandalizi mazuri yaliyofanywa katika kuandaa Muswada huu. Kama utakavyokumbuka mwanzoni kabisa mwezi Machi Muswada lilikuwa ni *book* kubwa sana. Lakini kwa ushirikiano mzuri kati ya Kamati na wadau na Wizara yenyewe pamoja na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambaye nataka nitumie nafasi hii kumshukuru sana kwa kweli *book* lile sasa limetoweka na kimekuja kitabu kidogo tu ambacho kinakidhi haja. Kwa hiyo, nimshukuru sana Waziri na wasaidizi wake na wote waliochangia katika kufanikisha na kufikisha Muswada huu hapa tulipo leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimpongeze pia Mheshimiwa Andrew Chenge, kwa kuteuliwa kuwa Waziri wetu wa Miundombinu. Matumaini yangu ni kwamba atatusaidia sana. Wizara hii ni kubwa ina makorogesheni mengi. Yeye kwa uzoefu wake na hasa kwa *profession* yake kama mwanasheria nadhani baadhi ya matatizo ambayo yanaisibu Wizara yatapata ufumbuzi wa haraka na mimi napenda nimhakikishie kwamba mimi na hata wajumbe wa Kamati tutashirikiana naye vizuri kama ambavyo tumesema hapo awali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia nimpongeze Mheshimiwa Basil Mramba, kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Viwanda na Biashara, lakini bila kusahau kwamba alifanyakazi nzuri tulipokuwa naye, tunamshukuru sana na tunamwombea kila la heri katika Wizara hiyo mpya ambayo amekwenda kuchukua majukumu mapya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na mimi pia kama walivyofanya wenzangu niwapongeze wote wale ambao wamechaguliwa kuingia katika Bunge la Afrika Mashariki. Matumaini yetu ni kwamba watatuwakilisha vizuri. Lakini pia nitumie, nafasi hii kumpongeza sana ndugu yetu Mheshimiwa Ali Ameir Mohamed, kuwa Katibu wa Kamati ya Wabunge wa

CCM. Nina hakika kwa uzoefu alionao ndani ya Chama, ndani ya Serikali atakuwa kiungo kizuri katika shughuli zote za Bunge na kadhalika, nampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze vile vile kwa kuunga mkono hoja iliyoko mbele yetu, ni Muswada mzuri. Sasa sina hakika kama umekuja wakati muafaka maana yake siku hizi kuna lugha hii jambo hili limekuja wakati muafaka, wakati mwingine sina hakika sawa sawa kama inakuwa ni kweli muafaka. Sasa unaweza kuwa na maoni kwamba labda umechelewa sana ungekuja mapema ungeokoa jahazi au vipi. Lakini nasema naunga mkono hoja kwa sababu kama Muswada, utapitishwa na sheria ikatunga, nina hakika makusudio yaliyoko katika Muswada huu, yakitekelezwa basi wananchi wa Tanzania watapata ukombozi katika suala zima la mawasiliano hasa ya posta, simu na mengine ambayo aliyataja Mheshimiwa Waziri, *radio, television* na kadhalika. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ni Muswada muhimu nina hakika Waheshimiwa Wabunge wote, tutaupitisha ili kusudi malengo yaliyoletwa na Serikali hapa yaweze kutimia. Nimesema ni muhimu nitoe mfano, katika Muswada huu, tunaimarisha shughuli za posta kwa mfano na tutakakuwa tumeimarisha shughuli za posta ni kwamba shughuli hizi zitakwenda mpaka vijijini. Hivi sasa kama tunavyofahamu mwananchi anaweza akatoka kilometa 100, 200 anasafiri anakwenda anatumia nauli kwenda shilingi 3,000 na kurudi shilingi 3,000 jumla shilingi 6,000 lakini wengine wanaweza wakatumia shilingi 4,000 kwenda na shilingi 4000 kurudi ikawa shilingi 8000 inategemea na eneo. Anakwenda ku-*post* barua ya shilingi 300 au 400. Sasa unakwenda ku-*post* barua ya shilingi 300 au 400 lakini unatumia nauli ya shilingi 6,000 mpaka shilingi 8,000, busara hapa haipo. Hata huo uchumi sijui uchumi gani haupo. Kwa hiyo, Muswada huu ukipitisha na sheria ikatungwa na yale yalikusudiwa yakitekelezwa kwa maana ya kwamba huduma hizi zikafikishwa huku kunakohusika katika vijiji, katika tarafa, katika kata n.k. angalau yatamuondolea mzigo mwananchi huyo atumie fedha yake vizuri kwa mambo mengine kulikoni kutumia shilingi 8,000 kwenda ku-*post* barua ya shilingi 300 au shilingi 400 lakini katumia shilingi 3,000 na ndivyo wananchi wetu kweli walio wengi wanafanya hivyo.

Sasa licha ya kwamba ni usumbufu anatumia siku moja/mbili na huko anakokwenda itabidi ale, alale pengine kama hawezi kurudi lakini vile vile hizi fedha hizi ambazo tunajua kwamba wananchi wetu walio wengi hali yao ya uchumi ni dhaifu. Lakini tunaendelea kuwatimiza. Kwa hiyo, Muswada huu utawakomboa wananchi walioko vijijini kwa sababu walau utapunguza hizi gharama ambazo kwa kweli hazina msingi wala hazina mantiki. Profesa hapa alizungumzia sana habari ya simu vijijini, simu ya mkononi vijijini moja ya kazi nzuri ambazo zinafanya ni kutafuta masoko kwa ajili ya bidhaa zilizoko vijijini. Mwananchi aliyoko Singida anauliza bei ya kuku kule Dar es salaam sasa anauzwa shilingi ngapi? Kuku Dodoma sasa shilingi ngapi, kuku Arusha shilingi ngapi, badala ya kusafiri na shehena au kuku halafu anakuta soko lile baya anarudi amekula hasara lakini kwa kutumia simu hizi za mkononi, zinamsaidia kujua bei ya kuku, bei ya ng'ombe, alizeti, ufuta na kadhalika.

Kwa hiyo, kama huduma hizi zitafika vijijini sasa badala ya kusafiri kwenda kuuliza soko liko namna gani kutoka *point* moja kwenda *point* nyingine wananchi sasa watafaidika kupata mawasiliano huko huko yaliko na akitoka pale anajua sasa ng'ombe

huyu nampeleka Dar es Salaam bei yake ni kadhaa, mahindi haya nayapeleka Dar es Salaam bei yake ni kadhaa.Kwa hiyo, huu nao ni ukombozi wa namna yake katika hatua hiyo.

Mheshimiwa Spika, ili sheria hii itakayotungwa iweze kutekelezeka kikamilifu ni muhimu sana kwa vyombo vilivyotajwa viweze kuimarishwa kikamilifu. Katika Muswada tunazungumzia habari ya posta, tunazungumzia habari ya simu na tunazungumzia habari ya vyombo vya utangazaji. Imani yangu ni kwamba ili hao wengine watakaosaidia kama hawa *service providers* kufanya kazi hiyo vizuri, lazima vyombo vyenyewe hivyo viwezi kuimarisha. Sidhani kwamba Serikali itakwepa wajibu wake wa msingi wa kuimarisha vyombo hivi. Hii ya kutafuta mfuko na kutoa ni *(additional)* ni nyongeza katika kuboresha huduma hizi. Lakini bado wajibu wa msingi *Public Services Obligation* iko pale pale kwa Serikali kuhakikisha kwamba inaimarisha taasisi yake, mashirika kama ya posta, simu akina *TVT*. *TVT* kama unakumbuka inafanyakazi nzuri sana lakini bado mpaka leo haijafika katika baadhi ya maeneo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi Singida kule *TVT* mpaka uwe na lile dubwasha ambalo ni *very expensive* kulipata, mwananchi wa kawaida atalipata saa ngapi. Lakini imani yangu ni kwamba Serikali nayo itaendelea kutimiza wajibu wake wakati wawekezaji wengine wanasaidia ili kuimarisha huduma hizi kama za *TVT* na *television* zingine sijui na simu pamoja na posta.

Mheshimiwa Spika, sikusudii kuzungumza sana leo habari ya posta kwa sababu katika Bunge lililopita wakati nachangia katika Wizara ya Mipango, nilieleza matatizo sugu ya habari ya posta. Matumaini kwamba Serikali ilisikia na Serikali inawezekana inachukua hatua. Nikumbushe. Matatizo matatizo makubwa ambayo yanasibu Shirika la Posta kwanza shirika limeanzishwa bila mtaji kwa sheria hiyo, namba 19 ya mwaka 1993. Mpaka leo mtaji haujakuwa *determined*. Nimwombe ndugu yangu Mheshimiwa Andrew Chenge pale, maadam ameingia hapa sasa na sasa ile aliniuliza mbona unalia sana na posta? Sasa na wewe umekuja naomba tulio wote ili kusudi tuwasaidie posta waondokana na matatizo. Kwanza tatizo la mtaji halijatatuliwa mpaka hivi sasa bado liko kwenye kikao cha Makatibu Wakuu, matumaini yangu ni kwamba Mheshimiwa Waziri, sasa ataharakisha kuona kwamba linatoka kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bado posta wana matatizo ya madeni makubwa waliyorithi kutoka *community*, hawajasaidiwa. Bado posta wana matatizo ya *pension* za watumishi wa Afrika Mashariki hawajasaidiwa. Ukilinganisha na wenzao wa *TTCL* ambao madeni yamefutwa, mtaji wamepewa, *pension* zinalipwa kwa kuundiwa utaratibu wa *SIMU 2000 Limited* sasa ndipo unafika mahali unaona kwamba hawa watoto wawili wa Serikali kwa nini huyu mmoja anakuwa *neglected* na huyu mmoja anashughulikiwa vizuri. Nimeomba sana Mheshimiwa Waziri ataliangalia.

Kwa hiyo, nasema wajibu wa Serikali uko pale pale wa kuimarisha vyombo vyake pamoja na kazi nzuri hii ya mfuko utakaofanywa wa kuwapatia hawa wawekezaji waweze kuimarisha. Lakini vile vile ombi langu ni kwamba hawa *service providers*

watakaopewa ruzuku lazima wawekewe *mechanism* ya kuhakikisha kwamba hiyo ruzuku wanayopewa kweli inakwenda kufanyakazi iliyokusudiwa. Katika zoezi la ubinafsishaji kuna watu wamepewa viwanda hapa lakini wamekwenda kufanya mambo mengine. Wengine wakafungua magodauni, wengine ofisi za vinyozi ni na nini wakati kilikuwa sijui cha nyama cha nini hakuna kama hicho. Ombi langu ni kwamba Serikali itafute utaratibu wa kuhakikisha kwamba wale *service providers* wanapeleka zile fedha na kutekeleza yale makusudia ambayo yamekusudiwa. Kama Muswada huu utapitishwa na Sheria ikatungwa na huduma hizi zikaenda vijijini, sisi tunayo matatizo sugu ambayo yako nina hakika yanaweza sasa yakatatuliwa kupitia katika utaratibu kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri, kwamba ukipitisha Muswada huu hata Wizara zingine, taasisi zingine kwa mfano posta zikiwepo kata na kwenye tarafa na kwenye vijiji tunalo tatizo sugu la mishahara ya walimu. Hivi ni kwa nini Serikali sasa isitumie posta iliyopo kwenye Makao Makuu ya Kata, kulipa mshahara kama wanavyofanya wenzetu nchi za nje walioendelea, mishahara ya walimu na mishahara ya watumishi wengine yalipwe kwenye posta na sisi tunaweza tukafanya. Kwa hiyo, badala ya kuhangaika kila siku mishahara ya walimu mara benki, mara wapi, tutumie nafasi hii sasa tupeleke posta kule ili mishahara ya walimu, ya manesi, ya madaktari walioko vijijini walipiwe kule kule. Hilo ni tatizo sugu ambalo lipo linaweza kutatuliwa kwa utaratibu huu. Hilo la kwanza. *(Makofi)*

Lakini vile vile tunalo tatizo la *pension* ya watumishi mtu anatoka Singida ndani ndani Iramba, Urambo ndani ndani kule anasafiri kwenda Dar es Salaam kufuata *pension* yake, *pension* yenyewe ndiyo kama hivyo anatumia nauli kubwa kuliko *pension* yenyewe au anatumia *three quarter* ya *pension* yenyewe. Kama posta zikiwepo kule ndani Urambo na Singida kule *pension* inaweza ikapelekwa pale katika posta kwa sababu ni chombo cha Serikali kinaaminika na watumishi wale wakalipwa *pension* yao katika posta iliyopo pale kijijini au kwenye tarafa au wapi. *(Makofi)*

Lakini vile vile tunazungumzia *SACCOS* na tumehimizana hapa kwamba lazima *SACCOS* zifunguliwe katika kila maeneo. *SACCOS* hizi wataweka fedha zao wapi? Lakini kama posta ziko kule posta ni chombo cha Serikali kinaaminisha watumishi wale wanaaminika wanaweza wakasaidia kuwawekea fedha hawa *SACCOS* katika ofisi zao, lakini pia kuwasaidia kuwalipa wanachama wao wale ambao ambao wanastahili kulipwa malipo mbalimbali kupitia posta. Kwa hiyo, tutakuwa tumetatua baadhi ya maeneo.

Lakini vile vile siku hizi kule vijijini wako madereva, mtu angependa ku-*renew license* watu wengine wenzetu kule nje una-*renew licence* katika mambo kama haya siyo mtu atoke sijui maili kilometa 200 anakwenda ku-*renew license* ya shilingi 10,000 anatumia shilingi 20,000 posta inaweza kutumiwa kwenda ku-*renew license* na kadhalika. Liko tatizo la bima walimu walioko vijijini walio wengi wamejikatia bima ya maisha lakini siku zote wanahangaika hawapati namna ya kulipwa zile bima zao. Bado posta inaweza ikatumika kama ni kituo cha kuwalipa bima wale watumishi mbalimbali ambao wamekata bima ya maisha pale bima zao zinapokuwa zimeiva na kuepusha usumbufu na gharama ya kutoka kule aliko kijijini kwenda makao makuu, sijui ya bima akapoteza fedha chungu nzima.

Kwa hiyo, hiyo ni baadhi ya mifano ambayo nasema kama Muswada huu ukipitishwa na sheria ikatungwa ikasimamiwa vizuri shabaha zikatekelezwa tunaweza tukatatua matatizo sugu ambayo tunayo kwa utaratibu huu wa posta kama walivyosema wenzetu ndivyo wanavyofanya katika nchi zinazoendelea. Kwa hiyo, sisi hatuwezi kuwa watu wa kwanza.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo na kama nilivyosema nimeshiriki katika Kamati yangu, naunga mkono hoja hii, naomba Waheshimiwa Wabunge, niwasihi na kuwaomba waupitishe Muswada huu mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Upande wa ufundi waangalie zile *microphones* ambazo hazifanyi kazi zirekebishwe ili Waheshimiwa Wabunge wasiwe wanapata shida ya kutangatanga kutafuta *microphone* iliyo *live*.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii, na mimi basi nijumuike na wenzangu kwanza kabisa kumpongeza ndugu yangu Mheshimiwa Andrew Chenge kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Miundombinu. Lakini vile vile nichukue nafasi hii kumpongeza sana Rais wa nchi, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa uteuzi alioufanya kwa Ma-*DC*. Shukrani hizi nizielekeza hasa katika uteuzi alioufanya Wilaya ya Meatu, tumepata *DC* mzuri, mchapakazi anayeshughulikia kero za watu usiku na mchana kama alivyo Mbunge wake. Nampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na mimi basi nijiekeleze katika kuchangia Muswada huu ambao unalenga kuwapatia mtandao hususan ndugu zetu wa vijijini ambapo mazingira ya kufanya biashara ni mazingira ya watu hawa wa mtandao kuwekeza wamekuwa wakisita kwa sababu maeneo hayo si mazuri kwa biashara kwa maana ya kwamba utumiaji wa simu ni mdogo katika watu wa vijijini. Kwa hiyo, watu wa mtandao wamekuwa wakisita kuwekeza katika maeneo hayo kwa kuogopa kwamba hawawezi wakapata *returns* mapema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwenzangu mmoja, Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani alikuwa na wasiwasi kwamba huenda huduma ya simu sio muhimu sana kwa sasa katika watu wa Vijijini. Mimi nimwondolee wasiwasi kwamba huduma ya simu kwa sasa hivi Vijijini ni muhimu sana. Wapiga kura wetu wanasubiri kwa hamu hata leo hii baada ya kusikiliza Muswada huu unasomwa hapa Bungeni nadhani wapiga kura wetu wote kule wanasikiliza kwa makini kuona kwamba ni nini tutasema juu ya suala hili.

Nazungumza hili hususan katika eneo ambalo naliwakilisha mimi katika Jimbo la Kisesa, wananchi wangu kwa kweli wana kiu sana ya kupata mawasiliano haya ya mtandao. Katika kero kubwa, basi ni hili la mawasiliano. Katika eneo ambalo limeathirika zaidi Tanzania nzima, naweza kusema ni Kisesa ndiyo imeathirika kwa kukosa mtandao wa mawasiliano wa simu za mkononi.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi katika mtandao wa simu za mkononi, eneo lolote lile ambalo halina mtandao wa simu za mkononi limekuwa si eneo tena zuri kwa kuishi. Hata kwa watumishi wa umma ambao wanafanya kazi kule Vijijini, eneo ambalo

haliwezi likawa na *access* limekuwa sio eneo zuri tena kwa kufanyia kazi. Watumishi wetu wanaondoka kwenye maeneo ambayo hayana mtandao. Anasema mimi siwezi kukaa kwenye eneo ambalo huwezi kupiga simu, huwezi kuwasiliana na dunia, siwezi kukaa. Anaripoti siku moja, siku mbili, anasema narudia mizigo, anakwenda kimoja.

Mheshimiwa Spika, juzi juzi hapa tumepata Walimu wa kwenda kwenye Sekondari zetu. Kwa kweli nampongeza sana Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa kazi kubwa aliyoifanya kutupelekea Walimu kwenye Sekondari zetu ambazo tumeanzisha za Kata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa moja ya sababu ambazo Walimu wameripoti kwenye Shule hizo na kuondoka ni ukosefu wa mtandao. Tumepangiwa Walimu kwenda, mimi kwa mfano kwenye Shule yangu ya Sekondari ya Lingeka, nilipangiwa walimu kama watatu. Kwenye Shule ya Sekondari ya Sakasaka nilipangiwa Walimu wawili. Wote wameondoka, lakini sababu ambayo wameondoka ni kwamba wao hawawezi kukaa kwenye eneo ambalo halina mtandao. Sasa mtandao huu ni wa muhimu mno.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi hata ukiingia kwenye huduma yenyewe ya afya, mahusiano ya Mganga na Daktari wake wanahitaji wazungumze kwa mtandao. Mawasiliano ya Zahanati, Kituo cha Afya na Hospitali wanahitaji wazungumze kwa mtandao. Ufanyaji wa biashara katika maeneo ambayo hayana mtandao hauendi, biashara haziendi, mfanyabiashara anahitaji kujua soko. Mkulima anahitaji kujua bei ya mazao yake, kama alivyoongea kaka yangu Mheshimiwa Missanga pale.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, vitu hivi vyote vinatuambia tu kwamba sasa kuna umuhimu sana wa kuwa na mitandao sehemu zote. Hata sisi Waheshimiwa Wabunge kuyatawala maeneo yetu kama Mbunge, lazima ujue maeneo yako yanaendeshwaje. Hata kwenye usimamizi wa Utawala Bora lazima tujue usimamizi wa uendeshaji wa shughuli za kiserikali zinavyoendeshwa kule lazima tujue.

Sasa kama eneo halina mtandao, mimi Mpina nikija hapa Bungeni huwa ninakaa mpaka niondoke ndiyo sasa naweza nikaenda tena nikafanye Mikutano kule ndiyo naweza nikajua habari za Jimbo zikoje. Lakini *other wise* hamna mtandao, huwezi kufanya mawasiliano. Kwa hiyo, kilio cha wananchi wetu ni kikubwa sana juu ya mtandao. Nasema kwamba kabla sijakwenda mbali niseme kwamba hoja hii mimi naiunga mkono asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini sasa kumekuwa na kigugumizi hata kwenye maeneo ambayo yako kwenye mtandao mzuri wa biashara. Hawa wenzetu wenye Makampuni ya Simu wamekuwa wakituahidi tu tutawajengea mtandao. Ahadi tu, kila siku tutawajengea mtandao. Mimi nina mawasiliano na Kampuni ya *Celtel* toka kipindi cha kampeni kwamba watakwenda kujenga mtandao kwenye Jimbo langu na wamefika kwenye Jimbo langu wakachukua uwanja, wakapima, wakasaini Mkataba na mtu mwenye uwanja. Lakini mpaka leo hatujawaona kusema kwamba tumekuja kutuwekea mtandao, Mpina haina matatizo. Lakini mpaka leo hawajaja.

Sasa unaweza kukuta kwamba pengine wenzetu labda wanakuwa tu hawafanyi utafiti wa kutosha kujua kwamba maeneo yapi ambayo yanastahili kupewa mtandao. Kwa sababu sehemu nyingine unaweza ukakuta tu kuna mlundikano wa mitandao kwa madai ya kwamba ni sehemu *potential* ya biashara. Lakini kuna maeneo mengine ambayo ni *very potential* kwa biashara, lakini wao hawajayaona. Kwa mfano, mnaposema kwamba katika Jimbo langu la Kisesa ambalo Makao Makuu yake yako Mwandoya, ni eneo zuri tu. Wakaaji ni zaidi ya 129,000. Shughuli za kibiashara, shughuli za kilimo na shughuli za ufugaji zinafanyika pale, wafanyabiashara wakubwa wako pale. Wanafanya biashara zao za kuuza na kununua mifugo, wanafanya shughuli zao za kilimo, wanalima pamba, wana uwezo mkubwa hata wa kupiga simu.

Shule za Sekondari zipo na Shule za Msingi zipo ambapo kuna wanafunzi na Walimu. Wote wanahitaji mahitaji ya simu. Zahanati, Ofisi ya Mbunge, Ofisi ya Katibu Tarafa, Vijiji na Kata, vyote vipo. Lakini vile vile katika Jimbo hilo kuna Makao Makuu ya pori la Maswa. Yaani *Maswa Game Reserve* ambapo Ofisi Makao Makuu yake yako pale na bado kuna Makampuni ya Uwindaji ya uwindishaji ambayo yamo kwenye pori lile. Wote wale wanahitaji mtandao.

Sasa ni sifa gani ambayo Mwandoya inakosa mpaka leo hii tunazungumza haina mtandao. Katika *geographical allocation* Jimbo la Kisesa ambalo Makao Makuu yake ni Mwandoya, tupo katikati ya minara ya Wilaya tatu. Wilaya ya Bariadi, Wilaya ya Maswa na Wilaya ya Meatu. Sasa mtandao ulioko Bariadi bado hauja-*cover* Wilaya yote ya Bariadi. Mtandao ulioko Meatu hatuja-*cover* eneo lote lile Meatu. Maswa hivyo hivyo. Kwa hiyo, ujenzi wa mtandao Mwandoya utasababisha kuwa na *full network coverage* katika maeneo haya yote ambayo hayajafikiwa na kwa maana nyingine katika zile Wilaya zile tatu, hakuna sehemu ambako kutakuwa na matatizo la mtandao.

Mheshimiwa Spika, mimi nitumie nafasi hii katika kuchangia Muswada huu kumwomba ndugu yangu, Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, Andrew Chenge, kwamba mimi mdogo wake sasa hapa nalilia mtandao. Tukifika ile saa 11.00 wakati anajibu hoja awe ameongea na watu wa *Celtel* wamwambie kwamba wanakuja lini Mwandoya kuja kujenga mtandao. *(Makofi)*

Ninajua kwamba sasa hivi wananchi wangu wote wananisikiliza na saa 11.00 wote watakuwa wamefungulia redio kusikiliza, watu wa *Celtel* wanakwenda kujaribu? Kwa hiyo, ndiyo ombi langu kwamba nitatarajia saa 11.00 Mheshimiwa Waziri atakuwa amefanya mawasiliano mazuri na watu wa *Celtel* kisha kuona kwamba ni namna gani watu wa Jimbo la Kisesa sasa wanaondolewa shida yao ya tatizo kubwa la mawasiliano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu kusudio kubwa lilikuwa ni hili ambalo nimemaliza kulizungumza, basi niungane na wenzangu wale waliokwishazungumza kwamba wenzetu hawa wenye Makampuni ya Simu, hebu basi wajaribu kukaa chini mkae nao chini waangalie namna ya kupunguza bei, gharama ya kupiga simu kama walivyozungumza wenzangu ni kubwa mno. Sh. 500/= kwa dakika moja ni gharama

kubwa. Hizi gharama zinaweza kupunguzwa kabisa, zinaweza kupunguzwa kutoka 300 hata kuja kwenye 200 kwa sababu tunacholipia kwenye simu ni *air time,* sasa hakuna duka la *air time.*

Sasa kama tunalipia *air time* haya Makampuni yetu ni *going concern* kwa sababu tunajua yanawekeza leo *and forever.* Sasa kama ni *coverage* tu ya gharama zao hizi *fixed costs* watazi-*cover* tu, lakini wafike mahali sasa, wewe una huruma kwa wananchi wetu. Serikali yetu wameona nia yake njema mpaka leo tunakaa. Tunasema kwamba sasa tunaweka bajeti kwa ajili ya kuwasaidia kuwawekea angalau ruzuku kidogo iwasaidie ili waweze uharakishaji wa upelekaji wa huduma kule Vijijini.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Naomba kumaliza kwa kusema kwamba nachangia hoja hii. Naiunga mkono hoja hii kwa asilimia zaidi ya mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA:** Mheshimiwa Spika, nami nichukue nafasi hii kwanza kukushukuru kunipa nafasi hii ili na mimi nichangie kwa machache kabisa kwa hoja hii ambayo iko mbele yetu. Ni bahati mbaya kwamba unapokuwa mtu wa mwisho, basi unafika mahali unakosa ya kuzungumza kwa sababu karibuni mengi yanakuwa yameshazungumzwa na wenzako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niungane tu na wenzangu kwanza kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Andrew Chenge kwa nafasi hii ambayo ameipata baada ya ile nafasi nyingine na vile vile nichukue nafasi hii kuwapongeza wale wengine wote ambao kwa mchakato uliopita hivi karibuni wa uchaguzi wamepata nafasi ya kuchaguliwa katika hizo nafasi. Nawapongezeni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu mengi yameshazungumzwa kuhusu Muswada huu na jinsi ambavyo Muswada wenyewe ulivyo, umuhimu wake, faida yake, mimi nafikiri nisije nikaharibu ule utamu wa yale yote ambayo yamezungumzwa na wenzangu isipokuwa tu niende kwenye suala moja ambalo linanitia wasiwasi. Suala hilo nalo ni la utekelezaji wa huu Muswada.

Mheshimiwa Spika, tuna Miswada mingi ya namna hii ambayo tumeiridhia na vile vile sio Miswada tu, lakini hata Sera, Sheria lakini utekelezaji wake unakuwa una matatizo. Inafika mahali kushindwa kuelewa kwa nini Serikali inaamua kutekeleza kitu fulani lakini baadaye inakuja inakwama. Nina mifano michache. Hivi karibuni kuna mfuko huu, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii, *TASAF.* Kuna mpango wa *SACCOS* na hata Ilani yenyewe ya Uchaguzi ambayo kwa kiwango kikubwa ni ahadi.

Mheshimiwa Spika, nasikitika kwamba sijui labda sehemu ya maeneo mengine, lakini maeneo yangu, hayo mambo hata kule kuanza bado hayajaanza kutekelezwa. Sasa sijui ni kwa sababu ya kile kilio changu nilichokitoa katika Mkutano wa Nne uliopita wa kuisahau hii Wilaya ya Chunya kuitenga hii Wilaya ya Chunya, sijui ndio mfumo huo unakwenda, sijui. Lakini nashukuru kwamba baada ya kilio changu, kuna Mawaziri wawili wametembelea Wilaya ya Chunya ambayo ndiyo ilikuwa kilio changu kwamba sababu kubwa inayofanya Wilaya ionekane imetengwa ni kutokana na hao viongozi wa

Kitaifa kushindwa kufika kwenye eneo hilo na siyo kushindwa kwa sababu gani, ni kwa sababu ya hali hali halisi. Miundombinu ndiyo inayowasababisha hao viongozi wasiweze kufika pale mahali. Lakini nashukuru.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dr. Makongoro ambaye amefika kuangalia lile tatizo ambalo nililiomba mbele ya Bunge lako Tukufu, nina hakika kabisa kwamba lile tatizo baada ya kuliangalia litatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, vile vile naomba nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Mwandosya ambaye naye ametumia nafasi ya kilio changu kuja kutembelea katika Wilaya ya Chunya. Nampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema kwamba utekelezaji ndio unaonipa wasiwasi katika mfuko huu. Ninaamini kabisa kwamba baada ya kuona kwamba kuna umuhimu na baada ya Mheshimiwa Waziri kuona kwamba kuna baadhi ya Miswada ambayo imepitishwa, lakini haijatekelezwa. Pengine anaweza akawa na mfuko wake tofauti wa kuweza kuhimiza utekelezaji wa huu Muswada.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu ni Muswada muhimu kwa sababu unalenga maeneo muhimu ambayo kuna watu wengi, kuna jamii nyingi ambayo inahitaji zaidi huduma hii. Kwa hiyo, nina uhakika kabisa kama hii huduma itapelekwa huko Vijijini kama wenzangu walivyozungumza, nina uhakika kabisa kwamba mabadilikko ya kimaendeleo kwenye sehemu za Vijiji yataonekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nazungumzia hivyo kwa uchungu kidogo hasa zaidi katika Jimbo langu Wilaya ya Chunya, yaani kuna mambo mengi! Najaribu kurudia hili kwa sababu kuna mambo mengi ambayo yameamuliwa, lakini hakuna kilichotekelezeka. Mfano mwingine, mfano wa kitaifa kabisa, Makao Makuu ya Wilaya ya Chunya yaliamuliwa kwamba yahamie Mkwajuni na huo ulikuwa uamuzi wa Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, mpaka leo hii ni zaidi ya miaka 40 halijatekelezwa. Sasa kuna nini? Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri nakuomba kwa sababu sitaki kurudia yale maneno ya wenzangu ambayo wamezungumzia, mimi nakuomba tu kwamba wakati utekelezaji utakapoanza naomba uangalie Wilaya ya Chunya. Wilaya ya Chunya kwa sababu ya matatizo yake kwa mfano kama hizi simu za mkononi, tunachohitaji sisi ni minara mitatu tu. Hii minara mitatu inaweza ikaongezwa kwa sababu tuna mnara mmoja huko uko Mbozi, mnara mwingine uko Mpanda, mnara mwingine uko Chunya pale Makao Makuu. Kwa hiyo, unaweza ukafanya *covering* ukafanya *network* ya Vijiji vyote vya Wilaya ya Chunya. Kwa hiyo, nilikuwa nakuomba tu Mheshimiwa kwa makusudi kabisa uangalie hili eneo langu.

Mheshimiwa Spika, naomba nisipoteze muda kurudia yale maneno ambayo wenzangu wameshayazungumza. Naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dr, Guido Sigonda. Hii inanipa nafasi, kwa sababu muda upo, nimwite msemaji anayefuata. Anayefuata ni Mheshimiwa Felister Bura.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuwa mchangiaji wa mwisho katika muda huu wa asubuhi. Kabla sijaanza kuchangia, nimpongeze sana Waziri wa Miundombinu kwa kuteuliwa kuwa Waziri katika Wizara hiyo ya Miundombinu baada ya kutumikia kwa muda wa miezi kama saba hivi au nane katika Wizara ya Afrika Mashariki. Nimpongeze pia Mheshimiwa Ali Ameir ambaye ni Katibu wa Wabunge wa CCM kwa uchaguzi au kwa kura nyingi alizozipata na kuwa Katibu wa Wabunge wa CCM.

Mheshimiwa Spika, lakini nimpongeze pia Waziri wa Miundombinu kwa kazi nzuri ambayo imefanywa na Wizara yake kwa kuleta Muswada huu ambao uko mbele yako siku ya leo na unaendelea kujadiliwa na Waheshimiwa Wabunge. Lakini kitu ambacho ningependa kusema mara ya kwanza ni kwamba nitafurahi sana kusikia kwamba Muswada huu wadau ambao ni wananchi wenyewe ambao Muswada huu unawahusu wameshirikishwa kwa hali ya juu sana na wao wakasema maeneo ambayo wangeona kwamba Serikali ingefanya marekebisho au mikakati mingine ili maendeleo ambayo wanataka kuletewa kwa njia ya Posta, Simu na mambo mengine, basi wawe wameshiriki kikamilifu.

Kwa hiyo, ningeomba pamoja na kwamba Kamati imesema kwamba wadau walishirikishwa lakini Wizara inasema nini kuhusu wadau hao? Kamati inasema kwamba kulikuwa na *public hearing,* sijui kama iliitishwa na Kamati yenyewe au ni Wizara ndiyo waliitisha *public hearing,* nijue kwamba wadau walishirikishwaje? Lakini pia niipongeze Serikali kwa kuuleta Muswada huu kwa sababu utawasaidia sana wananchi ambao wanaishi katika maeneo ya mbali kupata mawasiliano ya haraka.

Kwa mfano, mimi hapa nikitoka Dodoma kwenda Kondoa, nikishaingia kwenye pori la Mtungutu sipati mawasiliano mpaka nitakapofika Kondoa. Kwa hiyo, kama nitapata hatari au shida yoyote njiani siwezi kupata mawasiliano. Lakini kama tutapata mawasiliano kwa njia ya simu itakuwa rahisi sana kwa wale wote ambao wanaweza kupata shida mbalimabli katika barabara/njia hiyo kupata msaada. Lakini hata kwa njia ya Mpwapwa ninaposafiri kwenda Mpwapwa hapo katikati baada ya kuachana na Chalinze pia hakuna mawasiliano mpaka mtu utakapofika Mpwapwa Mjini.

Kwa hiyo, nitafurahi sana kama Wizara hii itapata wawekezaji ambao watatusaidia kupata mawasiliano kati ya Wilaya na Wilaya. Baada ya hapo, naomba niende kwenye Muswada wenyewe ambao nitazungumza sana katika vifungu ambavyo vimetajwa humu ndani. Katika *part three,* kifungu cha saba na kifungu kidogo cha pili ambacho kinaongelea Bodi ya Mfuko, katika Bodi hii kuna Wajumbe kumi na Mjumbe mmoja akiwa ni Meneja wa Mfuko. Sasa kitu ambacho nashindwa kukielewa hapa ni kwamba huyu Meneja ni *Board Member.*

Je, atawajibishwa vipi kama yeye ni *Board Member* kwa sababu yeye anatakiwa kupeleka taarifa za kazi yake katika Bodi? Lakini pamoja na hayo yeye ni *Board*

*Member* sasa kama atakosea atawajibishwa vipi na Bodi hii ambayo yeye ni *Board Member* na kitu kingine ambacho nimekiona ni kwamba huyu Meneja ana Mkataba wa miaka minne. Lakini sheria haijasema kwamba baada ya hiyo miaka minne: Je, ataruhusiwa kuendelea au ata-*apply* tena kazi upya katika mfuko? Sheria haijasema, Sheria imenyamaza kimya, kwamba je, huyu mtu baada ya kumaliza kipindi chake cha miaka minne anakwenda wapi? Anaendelea na kazi au anakuwa *terminated* au inakuwaje?

Ningeomba Wizara itupe maelezo kuhusu baada ya meneja kumaliza Mkataba wake inakuwaje? Mkataba haukusema kwamba huyu mtu atalipwa nini katika hifadhi ya jamii, atakuwa chini ya hifadhi ya jamii ipi. Kwa sababu hifadhi zote za jamii zina sheria kwamba mtumishi mpaka afanye kazi kwa kipindi fulani ndio anaweza akapata pensheni: Je, huyu Meneja atakuwa *covered* na *social security* ipi? Hilo halikuzungumzwa kwenye Sheria. Kitu kingine ambacho nimeona ni kwamba mtumishi anapokuwa na uhakika wa kazi yake kwamba atafanya kazi kwa miaka 10 anafanya kazi kwa imani kubwa na anafanya kazi akijua kwamba akiharibu hapo katikati mambo yanaweza yakaharibika.

Lakini sasa huyu amepewa miaka minne tu na sheria haikuzungumza kwamba hii Bodi itafanya kazi kwa muda gani. Meneja tu amepewa miaka minne, lakini je, Bodi ya Mfuko itafanya kazi kwa muda gani? Ningeomba Wizara ikatupa maelezo kwamba Bodi imetengewa muda gani wa kufanya kazi kwa sababu Bodi zote zina muda wa kufanya kazi. Kama ni miaka mitatu, kama ni miaka miwili, kama ni *for ever,* basi tutaambiwa kwamba Bodi hiyo itawajibika kwa muda gani.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nimeliona ni katika kifungu cha tisa cha sheria hii. Kifungu cha 9 (3) nimeshaongelea, lakini kitu kingine ambacho nimekiona kwenye sheria hii ni *Secretary* wa Mfuko au Katibu wa Mfuko ambaye ni Mwanasheria na ataajiriwa kwa kufuata taratibu na Kanuni ambazo mfuko utakuwa umejitungia.

Mheshimiwa Spika, lakini kitu ambacho nimekiona hapa ni kwamba huyu Katibu wa Bodi hana muda maalum. Meneja ana muda wa miaka minne kufanya kazi katika Bodi, lakini Sekretari au Mwanasheria huyu ambaye ataajiriwa na Bodi hana muda. Muda haukuonyeshwa kwamba atakuwa mwajiriwa au atakuwa kwenye *contract* wakati akiwa mtumishi wa mfuko huu.

Ninaomba sasa Wizara itusaidie kujue kwamba huyu ambaye ni Sekretari wa Bodi hii atafanya kazi kwa misingi ipi? Wameeleza tu kwamba awe amefanya kazi kwa muda wa miaka mitano, lakini kwamba ajira yake itachukua muda gani? Sheria haikueleza. Halafu kitu ambacho pia ningetaka kujua *ni supervision* ya Bodi kwamba wata-*supervise* vipi mfuko huu kwa wale ambao watakuwa wamepewa ruzuku na Serikali? Kwa sababu hawakusema kwamba kituo chao ni Dar es Salaam au ni Dodoma na baada ya kituo chao watafungua *branches* katika Mikoa mbalimbali au katika Wilaya mbalimbali hapa nchini.

Sasa ningependa kujua kwamba Wizara itusaidie kujua kwamba *supervision* kwa pesa za ruzuku ambazo zitakuwa zimetolewa na Mfuko huu itakuwaje? Je, watakuwa

wanatuma watumishi wao sehemu mbalimbali ambako wametoa mikopo au sehemu mbalimbali ambako wametoa ruzuku au hawa ndio watakuwa wanaleta ripoti zao kwa sababu wamesema kwenye sheria kwamba *account* zao zitakuwa zinakuwa *audited* na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali kila baada ya miaka miwili. Lakini je, hawa waliopata ruzuku pesa za Serikali watakaguliwaje?

Ningeomba Wizara itusaidie kwa sababu hizi pesa ni za walipa kodi na hawa watu wangependa kujua kwamba Serikali inatoa ruzuku kwa ajili ya wao kupata huduma mbalimbali. Lakini kama hakuna taarifa itakayotolewa na Mfuko kwa muda unaotakiwa na kama mfuko hautafuatilia kwa karibu sana matumizi ya ruzuku inayotolewa na Serikali, basi inawezekana wengine watakaopewa ruzuku wakatumia kwa shughuli zao wanazozijua wenyewe. Kwa hiyo, ningemwomba Waziri na Wizara yake kuhakikisha kwamba wanadhibiti ruzuku ambayo itakuwa imetolewa aidha kwa kufungua Ofisi katika Mikoa au katika Wilaya na ripoti wawe wanapata kwamba pesa hizo zimetumika kikamilifu.

Naipongeza sana Wizara kwa kuwa sasa wananchi watapata huduma mbalimbali na kwa karibu zaidi kwa sababu huduma hizi wananchi wanazifuata mbali sana, kama walivyosema Waheshimiwa Wabunge wengine kwamba wananchi wanafuata huduma mbali na wanatumia na pesa nyingi kwa ajili ya kufuata huduma sehemu ambazo ni mbali. Kama hakuna barabara inayopitika wakati wote, mitambo ambayo itapelekwa katika Vijiji itaharibika na haitatengenezwa mpaka kipindi cha kiangazi. Kwa hiyo, wananchi watakuwa hawajafaidika na huduma ambayo Serikali inategemea kutoa kwa wananchi wake kwa sababu ya miundombinu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninakushukuru kwa kupata nafasi hiyo na niiombe Wizara kuwa karibu sana na hawa ambao watapata ruzuku ili kuhakikisha kwamba wananchi wanapata huduma kwa muda unaotakiwa na pesa za ruzuku za Serikali zinatumika kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja asilimia mia. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, umekaribia muda wa kusitisha shughuli za Bunge na kwa hiyo nasitisha shughuli za Bunge sekunde chache au dakika moja kabla ya wakati wake hadi hapo saa 11.00 jioni.

*(Saa 6.59 Bunge liliahirishwa hadi saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, bado tunao wasemaji wawili, tunaye Mheshimiwa Peter Serukamwa atafuatiwa na Mheshimiwa Michael L. Laizer na baada ya hapo tutaendelea na utaratibu wa ku-*wind up* Muswada wetu.

**ME. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza mimi ninatwa Peter Serukamba na siyo Peter Serukamwa.

**MWENYEKITI:** Ninashukuru kwa kuweka kumbukumbu vizuri Mheshimiwa Peter Serukamba.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nishukuru kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia kidogo kwenye Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama walivyoanza wenzangu, nami nianze kuwapongeza Wabunge waliochaguliwa kutuwakilisha kwenye Bunge la Afrika ya Mashariki. Pia, nimpongeze Mzee Ameir Ali Ameir, kwa kuchaguliwa kuwa Katibu wa CCM, kwa Wabunge wa Chama Tawala hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu umekuja kwa wakati muafaka na kuna mambo ambayo ningependa kutoa angalizo kidogo ili labda wakati ambapo Waziri anajibu aweze kuweka sawa. Muswada huu ni wa kuhakikisha tunapeleka huduma hizi za Mawasiliano Vijijini na wanasema *under served areas.* Lakini najaribu kuangalia, kuna mambo ambayo ni ya msingi kuyaangalia hapa ili huduma hizi ziweze kwenda kwenye Vijiji vyote vya nchi hii. Vikiwemo Vijiji vya nyumbani kwako kule Peremiho, lazima tuweze kutoa ruzuku, kwa hawa *Operators,* kama ni simu kwa Posta na kwa namna yoyote ya mawasiliano. Lakini mimi nimekuwa nikijiuliza kwa kina kidogo.

Ruzuku utakayoitoa kwa mfano kwa hawa *operators* wa simu ili wapeleke simu Vijijini, ruzuku hii tunampa nani? Nani atafaidika na ruzuku hii? Ni wale *operators* ama ni wale watu wetu wa Vijijini. Kwa sababu nilikuwa ninajiuliza, kwa mfano unapeleka katika Vijijij vyangu vile vya Kigoma, unapeleka simu inakuwepo Mgumile, kwa kweli kwa hali ya kawaida ingelikuwa ni vigumu kuwapelekea simu kule. Tuna-wa-*subsidize,* hawa watu wanapeleka simu kwenye hivyo Vijiji.

Je, zile gharama sasa za uendeshaji, kwamba mtu ameishakuwa na simu, kwamba simu pale ipo, watu wawe na *access* na hizo simu. Je, gharama za upigaji zinashuka ama tulikuwa tuna m-*subsdize* yule *operator* aweze kupeleka kule Kijijini? Maana kuna mambo mawili hapa. Kumfanya *operator* aweze kupeleka hizo huduma za *communication* Vijijini, ama zile sehemu ambazo hazijaendelea?

Je, tukishamwezesha kupeleka, kitakachofuata ni nini? Tutamsaidia sasa gharama zitapungua kwa yule mtumiaji. Kwa sababu mwisho wa siku tunaweza kum-*subsidize* akapeleka kule Kijijini, lakini bado gharama zile za upigaji zitabaki ni zile zile. *Tariffs* zao zitabaki ni zile zile. Kwa hiyo, maana yake hapa tulichofanya *basically* ni kupunguza *costs* za *production* za hao *operators.* Kwa sababu tumem-*subsidize,* tukisha m-*sibsidize,* maana yake gharama zake zitashuka atapeleka hizo simu kule Kijijini, lakini kama hatufikirii namna ya kuwasaidia watu wa Vijijini kuwapunguzia gharama za

kupiga, kwa mfano kama ni simu bado, nadhani tutakuwa hatujafikia kule tulikotaka kufikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwenye huu Muswada *Part II,* anasema: *"The object of the funds."* *Number 5(e)* Anasema: *"To promote widespread provision of quality services at affordable rates and ensure that rural and under served areas have access to communication and infomation services at reasonable and affordable prices."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichokuwa ninasema hizi *affordable prices* kwa watu wa Vijijini ni zipi, maana kama ni kadi ile ya kununua ya *airtime,* bado *price* itakuwa ni ile ile, *unless* uniambie zinakuwepo kadi kwa ajili ya Vijiji. Kwa hiyo, bado ningependa kupata *mechanism* hii ita-*work* namna gani. Ni vizuri tuwe *very clear,* tusije tukapitisha jambo hapa, lakini kesho tusije tuka-*achieve* tulichotaka ku-*achieve,* kwa maana ya kupeleka mawasiliano Vijijini. Lakini pia ukiangalia kwenye Muswada huu *Part II Number 6(a) "The functions of the Fund shall be to identify the communications project areas that may be subsidized with funds of the fund or that qualify for allocation of subsidy by the fund."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nikawa ninajiuliza itatumika *criteria* ipi kujua kwamba kwa hali hii hapa tuwa-*subsidize,* hapa tusi-wa-*subsidize, criteria* ni ipi. Lakini pia tusisahau kuna baadhi ya *communication* hizi zimeshaanza kwenda na maeneo mengine. Je, na hawa tunawa *subsidize* baada ya hapo? Nilitaka Mheshimiwa Waziri anipe maelezo kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kwangu ninaona ni la muhimu sana, tunataka kupeleka *communication* Vijijini, mimi hili sina tatizo nalo kabisa. Lakini kuna mambo ambayo yako *connected,* kuna *issue* ya *infrastructure,* tutapeleka simu Vijijini, *fine:* Je, *infrastructure* zetu kwa maana ya *electricity roads* zipo? Leo tuna mpango wa kupeleka umeme Vijijini. Umeanza? Au unaanza lini?

Kwa sababu unaweza ukapeleka hiyo mikonga ya simu, wakawa nayo kwa kila Kijiji, lakini wasiweze kutumia zile simu kwa sababu Vijiji vyao havina umeme, watawezaje kutumia hizo *communication?* Hiyo *internet,* hizo *computer,* itakuwaje? Kwa hiyo, lazima mambo haya tuyapeleke kwa wakati mmoja, ili Posta iweze ku-*function* vizuri, barabara ni *crucial.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara za Vijiji vyetu, *unless* wengine labda kama hawatoki Vijijini hali za barabara siyo nzuri sana. Je, tumejiandaaje? Hii *package* nzima ni lazima iende pamoja. Lakini tutaanzisha *funds,* kutakuwepo na pesa tutawa-*subsidize* wapi? Kama bado hatuna umeme Vijijini, bado hatuna barabara nzuri za kwenda Vijijini, bado hatutaweza kufikia lile lengo letu tunalotaka kufikia hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nilitaka kuzungumzia ni hapa *formation* ya *Board Part III.* Mimi sina tatizo nalo hili la *formation* ya *Board.* Lakini kwenye *Board,* nilitaka nitoe angalizo moja. Kumezuka *trends in this country,* unakuta *Board* zote ni *officials* wa Serikali. *Representative* kutoka katika Wizara hii.

Kwa hiyo, unakuta *may be* ni mtu mmoja tu. Matokeo yake hawaendi kufanya ile kazi vizuri. Unakuta mtu mmoja tu labda ana *Board 10,* lakini bado ni Ofisa wa Serikali. Ana *Board* tano, lakini bado ni Afisa wa Serikali, kazi yake yenyewe tu inamfanya ashinde Ofisini na kulala Ofisini. Kazi zake ni nyingi sana. Lakini bado tunamwongezea na *function* za kwenda kuangalia hizi *Board,* matokeo yake sasa, hizi *Board* mambo mengi yanaharibika. Ukijiuliza kwamba hizi *Board* zilikuwepo, kilichotokea ni nini? Kumbe kwa sababu *Board* hizi tumewajaza wafanyakazi wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana unamkuta mtu ni Katibu Mkuu. Katibu Mkuu huyo huyo ni Mwenyekiti wa *Board* mbili au tatu. *Board* hizo zina-*report* kwa Katibu Mkuu huyo huyo! Mimi sielewi hilo! Labda tulifikirie upya hili. Bahati nzuri *Attorney General* yuko hapa, atusaidie kulifikiria upya hili. Mimi ninaona kama kuna *conflict of interest,* lakini pia ukiacha *conflict of interest,* kuna *issue* ya ile *commitment* ya kufanya ile kazi.

Mimi nadhani nchi hii bado tuna watu wengi sana. Ningependa kwenye hili suala la *Board* tulifikirie upya, ikiwezekana twende kwenye *professionalism.* Kama ni suala la kunatafuta watu kwa ajili ya kusimamia *Board* hii ya *Universal Communication Services,* kuna watu wengi nchi hii wazuri sana ambao wanayajua mambo vizuri, ambao wanaweza wakasimamia *Board* yetu vizuri.

*Likewise* kwenye *Board* nyingine. Mimi sisemi kwamba jamani, tunaomba kama wenzangu walivyosema, lakini tunachotaka kusema ni kwamba twende kwenye *professionalism.* Nchi hii tunao watu wengine wamesoma vizuri. Lakini haiwezekani! Kuna mtu mmoja ukienda kwenye *Board* nyingi ni *Registrar* wa Wizara ya Fedha yuko kwenye kila Board, kwa sababu sheria inamtaka kila *Board* yeye awemo, hata Sheria hii inasema mtu wa fedha ni lazima awemo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa unamkuta mtu huyo mmoja *every where* yupo, atakaa muda gani kufanya kazi za Ofisi. Atakaa muda gani kusimamia hizo *Board* alizopewa? Kwa hiyo, mimi nilitaka kwenye hili nalo tuliangalie upya. *At least* kwenye hiki, *fund* tunayoianzisha iwe tuchukue *Board* ambayo tuna hakika kazi yao ya kila siku itakuwa kweli ni kusimamia vizuri hii *fund* ili iweze kufikia yale malengo tuliyoyatarajia. *(Makofi*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala hapa nimeona la kuchagua *Secretary to the Board. The Board shall appoint a Lawyer of not less than five experience to be the Secretary of the Board.* Sasa mimi niseme, *I believe Board* hii itakuwa na Mwanasheria. Lakini Mwanasheria huyu, tunasema asiwe *Secretary to the Board,* bado *Board* ichague *another lawyer, unless* uniambie katika watu watakaoajiriwa kwenye *Board* hii, hakutakuwa na Mwanasheria. Mwanasheria huyo atakayechaguliwa ni kwa ajili ya kuja kufanya kazi ya kuwa *Secretary to the Board.*

Lakini sasa kuna-*another functions* zinazohitajika kwa ajili ya *Lawyer* hapa. Kwa hiyo, mimi nilidhani niombe kama inawezekana. *Secretary to the Board* awe ni Mwanasheria wa hii *Fund,* asiwe mtu mwingine ambaye atakayeteuliwa kwa ajili ya kuja

kufanya kazi za *Board* peke yake. Kwa hiyo, mimi nilidhani waniambie *why* wameiweka hivyo au kama kweli *fund* hii itakuwa haina Mwanasheria, mimi ninasema sawa, achaguliwe kwa ajili ya kuja kuchapa kazi za *Board.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama kwa hali hii atakuwepo Mwanasheria na nimeona iko kwenye Makampuni mengi sana, kama ni *Secretaries* wote wanakwenda kuwa Ma-*Secretaries* kwenye *Board,* sasa kwa nini kwenye *fund* hii tusifanye hivyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nami ninaunga mkono Muswada huu, umekuja kwa wakati, lakini ningeliomba haya ambayo nimetoa kama angalizo, Waziri ajaribu kuliambia Bunge hili, tuwe na uhakika tunainzisha *fund* hii lakini kweli tutafikia yale ambayo tunayatarajia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru sana Mheshimiwa Peter Serukamba na hasa ninakushukuru kwa kukumbuka vile Vijiji vyangu vya Peramiho ambavyo vitazingatiwa kwenye Muswada huu. Ninakushukuru sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninaomba sasa nimwite Mheshimiwa Michael Lekule Laizer na yeye aweze kuchangia Muswada wetu.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie Muswada huu. Kwanza, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri aliyeleta Muswada huu na niseme tu Muswada huu ni muhimu sana hasa kwa sisi Wabunge tunaotoka Majimbo ya Vijijini. Kwa hiyo, tunafurahia sana, tunaunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Miswada ya aina hii ambayo iliwahi kuletwa hapa Bungeni, nazo zinalenga kabisa, zinatoa huduma Vijijini, kwa mfano Mfuko wa *Road Toll,* umeletwa hapa Bungeni tukapitisha na tumeona mafaniko yake. Kwa sababu karibu Halmashauri zote zinapata fedha za barabara, hata zile barabara za Mikoa zinapata fedha kutoka ule Mfuko wa *Road Board.* Kwa hiyo, nategemea kwamba na huu mfuko ukienda vizuri, tunaweza tukafaidika nao.

Juzi juzi tu tumepitisha Mfuko wa Umeme Vijijini ambao bado haujaanza, lakini tunategemea ukianza, utaleta manufaa sana katika maeneo ya Vijijini. Nadhani Mfuko huo na huu, haiwezi ikatengwa, inafaa iende sambamba kwa sababu ni mifuko inayotegemeana. Huwezi kupeleka mawasilino Vijijini bila umeme. Kwa hiyo, mifuko yote miwili inafaa iende pamoja na ifike Vijijini, kwa sababu maendeleo bila mawasilino kwa kweli hakuna maendeleo yatakayofika Vijijini. Vijijini wanataka kuwasiliana na Halmashauri na Halmashauri wanataka nao kuwasiliana na Vijiji. Sasa bila mawasiliano kwanza inaongeza gharama kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu kuna maeneo mengine ambayo yako mbali sana na Halmashauri na wananchi wanakosa elimu. Ukiangalia watu wenye *TV,* kuna elimu kubwa sana inayotolewa kwa matangazo ya *TV* ambayo Vijijini, Vijiji vingi

havijawahi hata kuona *TV*. Kwa hiyo, matangazo muhimu yanafaa wananchi wote wa nchi hii wapate hiyo elimu inayotolewa kwa njia ya *TV*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana katika maeneo ambayo barabara ni mbaya sana, wakapata mawasiliano kwa njia ya simu. Kwa hiyo, ni muhimu huu mfuko, tuupitishe na uimarishwe na ufike Vijiji vyote. Sio kuongeza tena minara katika Miji, iunganishwe minara mpaka ifike katika maeneo magumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kautani ambako maeneo ambayo hayana huduma kabisa, hayana barabara, hayana simu, hayana hospitali, hayana Shule nzuri, unakuta wanaita kule ni Tanganyika. Sawa, ule U-*Tanganyika* ni kwamba wamefananisha na kabla hajutapata uhuru na bado kuna watu wanaoishi katika mazingira hayo. Sasa nadhani mifuko hii miwili, mifuko ya umeme, Mfuko huu wa Mawasiliano tunaoupitisha, ulenge sasa hawa wananchi tunaosema bado wako Tanganyika, wawatoe katika U-*Tanganyika* huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema kwamba, kuna wakati ambapo tumepata shida sana, tulivamiwa na Wasomali. Wilaya ya Ngorongoro na Wilaya ya Monduli hasa Longido, Wasomali waliingia huko, waliwapiga watu, waliwaibia na kuwanyang'anya mali zao na kfuanya mambo makubwa maovu. Kwa muda wa miaka mitatu, Ngorongoro na Longido hawakupata maendeleo kwa sababu hakuna Mwalimu anayetaka kwenda huko, hakuna kiongozi yeyote anayetaka kwenda huko.

Siku moja Mheshimiwa Kapuya amekwenda akaonyeshwa vichwa vya maiti saba. Hakulala! Alikimbia siku hiyo mpaka Arusha. Hakulala tena Ngorongoro na ilikuwa alale Ngorongoro, akaapa kwamba siwezi kukanyaga tena Loliondo. Nadhani kungelikuwa na mawasiliano Mheshimiwa Kapuya asingelikwenda huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa matatizo yaliyotokea kwa wakati huo, Loliondo haina mawasiliano. Longido haina mawasiliano. Yaani wananchi wanatoka maeneo Vijiji vilivyoko kule mbali, *Lake Natron,* kilomita 200 ili wafike maeneo yenye mawasiliano. Wakati huo Serikali imefanya kazi kubwa sana, imengia gharama kubwa sana kubwa kuwapeleka wanajeshi kwenda kupambana na hao Wasomali. Sasa tatizo ni mawasilino. Huwezi kabisa ukaenda popote kutoa mawasiliano kwa sababu hata magari hayafiki. Hakuna mtu anayetaka kupeleka gari lake huko.

Siku moja wamevamia gari inayokwenda Gilai na kuwapiga watu risasi. Hakuna gari tena iliyokanyaga ukanda huo. Kwa hiyo, mtu akija kutoa taarifa anakuja kwa miguu kilomita 200 ndiyo afike Longido kutoa taarifa. Sasa maeneo hayo ndiyo yanayohitajika sasa, umeme ufike na mawasiliano yafike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini bado tunaweza tukafikisha umeme, tukafikisha mawasilino huko, lakini wananchi wakashindwa kutumia huduma hizo zilizofika katika maeneo yao kwa ajili ya gharama. Nadhani wote ni mashahidi. Kule Kijijini wakitaka kuwasiliana na sisi hakuna anayepiga, ana-*bip* tu.

Kwa hiyo, wananchi Vijijini wana simu kwa ajili ya ku-*bip,* kwa sababu hawewezi kumudu gharama ya simu. Juzi, Bunge lililopita tumepitisha kodi ya *airtime.* Kama mmegundua hiyo imekwishakuwa gharama kubwa sana. Ukiweka dola tano huongei na watu wawili bila kuongeza dola nyingine. Hivi watu Vijijini wanaweza kumudu gharama hiyo kweli? Kwa hiyo, ningelipenda kusema kwamba ruzuku hii, Serikali inayotoa kwa ajili ya mfuko huu, ipunguze kabisa gharama za simu, la sivyo, tutafikisha watu wakashindwa kutumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeliomba niseme tu gharama hii isiwe kama gharama au ruzuku Serikali inayotoa kwa *TANESCO.* Nadhani mimi sijawahi kuona faida yoyote ya hiyo ruzuku inayotolewa na Serikali *TANESCO,* kwa sababu kwanza *TANESCO* wenyewe ni wafanyabiashara wakubwa na kila mtu anategemea kwamba *TANESCO* wanakusanya fedha nyingi sana. Kwa hiyo, mimi sitegemei, siyo watu wa kupewa tena na kuongezewa ruzuku. Kwa hiyo, ningependa kusema kwamba hebu tuangalie. Tuangalie hii ruzuku inayotolewa kwa ajili ya kupunguza gharama za wananchi, iwe ni ruzuku kweli inayolenga kupunguza gharama ili wananchi wakaweza kufaidika na ruzuku hiyo ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende tu kusema kwamba katika maeneo, Vijiji ambavyo wana mawasiliano ya simu, lakini hawana umeme, kwa sababu mpaka sasa kuna Vijiji vingine ambavyo wana mawasiliano ya simu, lakini hawana umeme, wana gharama kubwa sana. Kama kuna mtu mwenye jenereta, huyo mtu ndiye anayefaidika zaidi kwa sababu ku-*charge* simu kwa muda wa dakika 10 ana-*charge* Sh. 1,000/=, sasa kama wananchi wanazo siku nyingi tu, hiyo inakuwa biashara kwa yule mtu mwenye jenereta.

Kwa hiyo, ningependa kusema kwamba huu Mfuko wa Umeme, tunahitaji sasa kuanza kuona baadhi ya Vijiji ambavyo vinapata huduma hiyo ili isiwe gharama zaidi kwa wananchi kulipia umeme kama wanavyolipia umeme katika maeneo hayo.

Mheshimwia Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache, napenda kusema kwamba ninaunga mkono Muswada huu uanze mara moja. Asante sana. *(Makofi)*

## MCHANGO KWA MAANDISHI

**MHE: SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, naomba nichangie mambo madogo tu kuhusu mawasiliano. Kuna sehemu ambazo zina matatizo makubwa sana kuhusu mawasiliano na ni muhimu sana. Katika pori la Biharamulo kuna Kambi ya Polisi wanasindikiza magari, wanakumbwa na mambo mengi na matatizo makubwa sana, wanapata madhara makubwa. Naomba Wizara yako iweze kukumbuka sehemu ambazo mawasiliano ni ya shida, kwani Maaskari wetu wanapata taabu sana ya mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, kutoka Biharamulo kwenda Muleba, katika pori hilo sio mara moja au mara mbili huwa wanatekwa na hakuna msaada wowote wa simu au mawasiliano yoyote, hawana! Hivi karibuni gari lilikuwa na maiti linatoka Uganda linakwenda Biharamulo, lilikuwa na Askari, Askari huyo bahati aliwahi kumpiga risasi

jambazi. Kuna matukio mengi katika pori la kimisi pamoja na pori la Karagwe. Kwa hiyo, naomba msaada kwa Mheshimiwa Waziri au kama haiwezekani, naomba hawa Mapolisi wanaosindikiza magari kwenye pori au mapori wasaidiwe kupatiwa *radio call* kuliko Maaskari hasa kama Dar es Salaam unakuta wanazo hizo *radio call.* Afadhali kuwapa Maaskari wa porini kuliko wa Mjini.

Mheshimiwa Spika, nitashukuru nikijibiwa maombi yangu na kutekeleza vizuri na sisi tuwe tunapita porini vizuri. Nashukuru sana kwa kupokea maombi yangu.

**MHE. VUAI ABDALLA KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nakupongeza kwa kuweza kuendesha Bunge hili na kusimamia Bunge la Kikao cha Tano. Pia naipongeza Wizara ya Miundombinu hasa Waziri na Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa malengo yake ya kuleta au kuangalia upya Muswada wa Serikali kuhusu huduma za mawasiliano. Naomba Muswada usisite uendelee na upate Baraka za Wabunge.

Mheshimiwa Spika, kuhusu huduma ya mfuko, naomba uchangiwe vyema na ukipita utumike vizuri kwa maslahi ya Tanzania. Wizara iwe mfano au kioo na Bodi yake iwe imara na huduma zifike kwa wananchi kwa hali zote.

Mheshimiwa Spika, kama Muswada huu ukipitishwa, huduma za Posta zifikishwe Wilayani Vijijini, hata kwa Vitongoji ili kuondokana na unyonge, umasikini na kadhalika na kuleta maisha bora kwa kila Mtanzania. Naomba haya tunayotarajia basi yawafikie walengwa wenyewe isiwe msemo tu.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Magogoni na mimi kama Mbunge mwenyewe, naunga mkono hoja kwa asilimia zote Muswada upite. Ahsante.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, ninaamini kuwa mawasiliano ni *transfer of information from the given to receiver and vice versa.* Lakini ni jambo la kusikitisha kuwa mawasiliano ya simu hapa Tanzania hasa sehemu za Vijijini ni mbaya mno. Tunashukuru kuwa angalau sasa hivi *radio* zinasikika maeneo mengine. Tunashukuru pia Kampuni za Simu za Mkononi zinavyojitahidi kupunguza tatizo la mawasiliano ya simu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi hizo, gharama zimekuwa kubwa sana. Pamoja na kuwa Tanzania ni nchi masikini sana *(per capita income)* lakini gharama za simu ni kubwa mno ukilinganisha na nchi zote, sio tu za *COMESA,* bali hata zile zilizoendelea kama Ulaya na Marekani ziko chini. Ni kwa nini hali hii hasa ikizingatiwa kuwa Tanzania ina Makampuni *(operators)* wanne, wakati nchi nyingine zina *operators* wawili au mmoja? Hivyo, nilitegemea kungekuwa na *competitions* katika hawa *operators* ili wadau wapate unafuu, lakini wapi.

Mheshimiwa Spika, nadhani pana tatizo kubwa sana na Wizara iangalie na kuona ni jinsi gani itasaidia. Kwa hali halisi, ile maana ya mawasiliano haitakuwepo kwani kama mtu atataka kuwasiliana na mwenzie anakwama kwa sababu ya gharama kubwa, nadhani sio sahihi. Mawasiliano ya simu, *radio*, *TV* na C*omputer*, yanakwenda sambamba na kuwepo kwa umeme. Vijiji vingi vya Tanzania havina umeme, sasa haya mawasiliano yatatekelezwa vipi bila umeme? Simu zinahitaji kuwa *charged* katika umeme; sasa itakuwaje?

Mheshimiwa Spika, suala la *Board* ya mfuko huu inashangaza. Nijuavyo mimi, Mwenyekiti wa *Board* huteuliwa na Rais; ni kwa nini *Board* hii iwe tofauti? Lakini pia uteuzi wa ujumbe hauna Mwakilishi Mbunge hata mmoja. Nategemea Waziri atachukua hili kama jambo la dharura na kuhakikisha Wabunge angalau wawili wanakuwa Wajumbe wa *Board* hii muhimu.

Mheshimiwa Spika, ni jambo la kawaida kwa wananchi wa Vijijini kutumia fedha nyingi na wengine hufia njiani kwa kufuata huduma za mawasiliano. Mfano Wengine hutumia hadi Sh.10,000/= ku-*post* barua au kutuma barua pepe *email*. Lakini pamoja na gharama ya fedha, pia wananchi wamekuwa wakipoteza muda mwingi safarini na kuacha shughuli zao za kila siku za kilimo na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, vijana wengi wanakosa taarifa muhimu mfano za kujiunga na Vyuo au hata ajira/kukosa *interviews* kutokana na kukosa mawasiliano kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, Muswada unaelezea zaidi *accessibility* ya mawasiliano. Mimi nadhani ingezungumzia zaidi *availability* ya mawasiliano. Nasema hivi kwani huduma inaweza kuwa *accessible* lakini isiwe *available*. Hivyo, suala la *availability* ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, mwisho, ninaomba sana gharama za simu za mkononi ziangaliwe upya ili wananchi wengi waweze kuwasiliana na ndugu, jamaa na marafiki.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiofichika kuwa wakulima na wafanyabiashara wanategemea sana mtandao wa simu ili aweze kujua mfano bidhaa fulani inauzwa kwa bei gani katika soko fulani ili aweze kupelekea biashara ile kwenye soko lenye bei ya juu. Lakini pia mfanyabiashara anapanga ni lini atasafiri ili kuchukua mzigo na asipoteze gharama nyingi kwa kusubiri mzigo kwani akijua mzigo unaingia lini atafunga safari kwa wakati unaofaa?

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kujua ni kwa nini Katibu wa *Board* awe Mwanasheria? Kwani ukatibu una uhusiano gani na Uanasheria? Lakini pia kwa kuwa mfuko huu unahusika na fedha, ni kwa nini *Manager* awe na sifa ya Uanasheria au Uhandisi? Kama fani hizo zinakubalika, ni kwa nini yule wa *Public Administration* asikubalike pia?

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. Ahsante sana.

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa ninapenda kumpongeza Waziri na Wizara yake kwa kuanzisha mpango huu wa mawasiliano Vijijini, kwani hiyo itarahisisha shughuli za maendeleo Vijijini hasa katika utalii, biashara na kadhalika. Nami ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, kusudi langu ni kuomba Mheshimiwa Waziri, kwa hisani yake, naomba sana aanze kwanza kufikiria kufanya huduma za mawasiliano.

Katika ngazi za Wilaya, kwanza Wilaya zile ambazo hazina mawasiliano kabisa, zipo Wilaya hazina kabisa mawasiliano yoyote ya simu, ya Posta, wala simu za mkononi na sio Wilaya nyingine bali ni Wilaya ya Ruangwa, Mkoani Lindi ambako kuna Mkuu wa Wilaya, Polisi Wilaya, Halmashauri ya Wilaya na ngazi zote za Wilaya ambako kuna umuhimu wa wao kuwasiliana na Mkoa kikazi. Tafadhali naomba waanze kuweka huduma ya mawasiliano katika ngazi za Wilaya kwanza, ndipo muelekee Vijijini. Naunga hoja mkono.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Spika, Muswada huu ni mkombozi kwa mwananchi wa vijijini ambako mawasiliano hayajafika. Wananchi wengi wanakosa huduma muhimu sana kama tiba sababu ya kukosa mawasiliano. Naiomba Wizara husika pamoja na mfuko huu, ifanye upembuzi wa kina kujua *underserved rural areas* zote nchini kwa *priority*. Baada ya kuzitambua, basi mfuko uelekeze huduma ya mawasiliano Vijijini kwa *priority* hiyo. Pale ambapo mfuko utashirikiana na *private sector* kutoa huduma hii Vijijini, basi mfuko uwe makini sana maana hawa *private sector* wasiposimamiwa, watapeleka hii huduma kule ambako tayari wana miundombinu ili kupata faida zaidi.

Mheshimiwa Spika, jambo la kutengeneza mipango mizuri na kutunga sheria ni moja, lakini utekelezaji wa mipango hiyo ni lingine kabisa. Naiomba Wizara iwe makini sana katika kusimamia utekelezaji wa kazi za mfuko huu wa mawasiliano. Kwa mfano, Ilani ya Chama cha Mapinduzi inaongelea wazi wazi ujenzi wa barabara ya Mbeya – Chunya – Makongorosi kwa kiwango cha lami. Katika kutekeleza hili Serikali ilitenga Shilingi bilioni kumi toka Bajeti ya mwaka 2005. Mwaka huu Serikali imeongeza billioni moja. Kwenye Mkutano wa Nne, Wizara ilitamka kuwa ujenzi utaanza mwaka huu wakati inajibu swali langu kuhusu barabara hiyo. Mwezi wa tisa Mheshimiwa Waziri alifanya ziada Chunya (namshukru sana) na pia aliwaambia wananchi kuwa ujenzi huo utaanza mwaka huu. Lakini hakuna kinachotokea mpaka sasa. Kuna nini *TANROADS?* Kwa nini utekelezaji unakwama? Ndio maana nimesema kwenye Muswada huu wa Mawasiliano, Wizara iwe macho sana kwenye utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. IDRIS ALI MTULIA:** Mheshimiwa Spika, naomba niipongeze Wizara yako kwa kuleta Muswada huu. Huu ni ukombozi mkubwa kwetu sisi tunaoishi Vijijini hasa katika Jimbo la Rufiji.

Mheshimiwa Spika, naomba gharama za huduma za mawasiliano Tanzania zipunguzwe sana ili wengi wamudu matumizi ya huduma hizo. Naomba pia kipaumbele kitolewe kwa Vijiji vinavyohitaji huduma hii zaidi, kabla ya hapo tufanye *baseline survey* ya kujua sehemu gani ya nchi yetu inahitji huduma hii zaidi kuliko sehemu nyingine ya nchi yetu. Tuanze na Kata, Makao Makuu kila Wilaya ipate huduma hizi. Wajasiriamali, watakaopewa ruzuku hii wawe makini ili tupate faida ya fedha zetu.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naunga mkono hoja hii. Lakini naomba kutahadharisha mambo yafuatayo:-

(i) Huduma hii ya mawasiliano kweli iwafikie wananchi wote Vijijini bila upendeleo wa maeneo na hata Wilaya na Vijiji vyenye mazingira magumu wanahitaji huduma hii hata kama maeneo hayo hayana maslahi ya maana kibiashara.

(ii) Imekuwa kawaida maeneo ya wafugaji kusahauliwa au kuwekwa nyuma katika mipango ya maendeleo likiwemo la mawasiliano ya simu, barabara, umeme, Posta na kadhalika. Naomba hili la mawasiliano hususan simu za mkononi lipewe kipaumbele katika Wilaya ya Ngorongoro, Longido, Monduli, Simanjiro na Kiteto.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Miundombinu. Pili, nampongeza kwa kuleta Muswada huu muhimu wa huduma za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia maeneo yafuatayo, lakini kabla ya hapo naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, ili kupata wateja wengi na kwa kuwa Serikali itatoa ruzuku kutoka katika Mfuko huu kuendeleza mawasiliano: Je, kwa nini gharama za kupiga simu zisipunguzwe?

Je, maeneo yale ambayo hayana mawasiliano ya simu Serikali ina mpango gani wa kuweka mawasiliano kwa ajili ya maendeleo ya nchi na hasa Wilaya ya Mpwapwa?

**MHE. NIMROD E. MKONO:** Hon. Speaker, *part 1 Preliminary Provisions, Section 3 provides the definition of universal services as: "means a defined minimum set of communications service of specified quality which is available to all users independent of their geographical location, and in the light of specific national conditions, at an affordable price.*

*However, there is no definition of "affordable." This is particularly relevant because the term affordable is used throughout this Act (for instance, in Section 5(e), 6(h) and in the Objectives and Reasons).*

*My recommendations are as follows, Part I should be amended by including the following definition of "affordable": "Affordable" means any rate, price, charge or fee that ensures that those on low incomes or with special social needs are not prevented from accessing or using the publicly available telephone service.*

*Part II, the fund, please note that the typographical error at section 5(b), "…rural and under served areas" should read "…rural and under-served areas." Please note the typographical error at section 5(b), "create a framework for an open and efficient access" should read "create a framework for open and efficient access."*

*Part III, the board, please note the typographical error at section 9(7)(i), "initiate funding proposal to replenish the Fund" should read "initiate funding proposals to replenish the Fund."*

*Honorable Speaker, Please note the typographical error at section 9(7)(i), "budgetary control of Fund and projects resources" should read "budgetary control of Fund and project resources." Also please note that the typographical error at section 12(1), "…may, upon advice by the Permanent Secretary" should read "…may, upon advice by the Permanent Secretary."*

*Also please note that typographical error at section 12(1)(e), "…a period of consecutive twelve months" should read "…a period of twelve consecutive months."*

*Part IV Provisions of Universal Communication Access Services, section 13(1)(b)(ii) calls for "responsible geographic access to public definition of what constitutes "reasonable" access.*

*Recommendation, the section should be amended to read as "reasonable (as defined by the fund in consultation with universal communication service providers) geographic access to public call boxes across the United Republic of Tanzania."*

*Section 13(1)( c) states that one universal service obligation is to make "generally available to everyone" services which are "provided to most people" and have become r "essential." However no definition of "most people" nor "essential" is given. This is particularly relevant seeing as a majority of Tanzania's rural populace, which forms a bulk of telecommunications services. Thus if the term "most people" were to be interpreted literally this would encourage a "race to the bottom" or a search for the "lowest common denominator." The term "essential" is prone to subjective judgment and needs to be defined for avoidance of doubt.*

*The recommendations on this is, on section 13(1)( c) may be amended to read as "ensure that the services which the market has provided to a majority of the people*

*within areas to be defined by the Fund and which have become essential according to the National Telecommunications Policy become generally available to everyone."*

*Please note that the typographical error at section 13(4) "…required to meet the services targets…" should read "…required to meet the service targets…"*

*Section 13(8) of Part IV of the proposed Act states that the Fund may make sure of various schemes in the promotion of universal service obligation.*

*The recommendation on this is to ensure that the condition of these schemes are fully transparent and applied in accordance with the principle of non-discrimination an additional sub-section should be added: "the conditions for any scheme, per sub-section (8) above, shall be published whenever such a scheme in put into effect by the Fund."*

*Part IV has no section dealing with review of the universal service obligation. As time goes by the Tanzanian Telecommunications sector develops it will be necessary to revisit the scope of the universal service obligations from time to time.*

*A new section should be added providing fro periodic review of the universal service obligations, a proposed section would read: "the fund shall periodically review the scope of universal service obligations, in particular with a view to proposing that the scope be changed or defined. A review shall be carried out, on the first occasion within two years after the Fund is established and subsequently every three years. The Fund shall be guided in its review by social and market development in terms of the services used by consumers and technological developments in terms of the way services are provides to consumers."*

*Section 14(2) of Part IV needs comment for two reasons. Firstly there are typographical errors, "…by reducing on the number of disconnection of end-users…" should be replaced by "…by reducing the number of disconnections of end-users…"*

*However the entire sub-section is questionable because it is not commercially viable to continue providing access to end-users when those users are not paying. Telecommunications firms would be unwilling to shoulders this burden unless given government guarantees. The government in its turn is highly unlikely to be able to support a possibly open-ended liability. Thus the entire subsection should be deleted.*

*Section 18 deals with universal service levy, however there is no mention of periodic reviews of this levy, nor is there mention of review of the net cost of compliance on which the universal service levy is based.*

*An additional section should be inserted after section 18 allowing for periodic reviews of the universal service levy and the net cost of compliance. A recommended clause would read;*

*"The fund must publish an annual report from a period of twelve months after the coming into force of this Act, on; the market benefits for each designated universal service provider, on the market benefits that have accrued to him during that period from*

*his designation and from the application to him of universal service conditions; and the contribution made under section 18 by every person who has made a contribution during that period.*

*The fund will also conduct annual reviews concurrent with the annual report set out in the subsection above , on; the net cost compliance after allowing for market benefits accruing to the designated universal service provider from:-*

*(a) his designation; and*
*(b) the application to him of universal service conditions.*

*After carrying out a review under this section the Fund must either:-*

*(a) cause the calculations made by them on the review to be audited by a person who appears to them to be independent of designated universal service providers; or*
*(b) themselves carry out an audit of those calculations."*

*Section 22 provides for the Fund to publish in Gazette and local newspapers the list of universal service providers "upon the issuing of funds." This term is not clear; which funds and when are they to be issued?*

*Section 22 should be modified to include reference to section 23 of Part IV, which deals with the Funds finances: "Upon issuing of funds per section 23, the Fund shall publish in the Gazette and local newspapers the list of universal service providers."*
*Please note that, the typographical error at section 2, "Any member may at time resign" should read "Any member may at any time resign."*

*Please note the typographical error at section 4(2), "the notice specify the place" should read "the notice specifying the place."*

*Please note the typographical error also at section 4(2), "…where the Chairman is unable to act by reason of illness or other case" should read "…where the Chairman is unable to act by reason of illness or other cause."*

*Please note the typographical error at section 4(3), "…the Vice Chairman, may on his own motion, and shall, if are quested in that behalf by at least half the members,…" should read "…the Vice Chairman may, if on his own motion, and shall, if requested by at least half the members,…"*

*Honorable Speaker, please note that the typographical error in the first paragraph, "…which is to enhance the welfare of Tanzania society…" should read "…which is to enhance the welfare of Tanzania society…" "…a framework for an open and efficient access and use communication…" should read "…a framework for open and efficient access and use of communication" and "…external markets for the rural products" should read "external markets for rural products" since no rural products have been mentioned beforehand in the Act, thus "the" is confusing and superfluous.*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sasa tumemaliza mjadala wa pamoja na Kanuni Na. 49(a)(b), kinatoa nafasi sasa kwa watoa hoja kuanza kujibu hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge.

Kwa hiyo, tutaanza na Mheshimiwa Naibu Waziri na yeye atatumia dakika 15 na baada ya hapo tutamwomba Mheshimiwa Waziri, mtoa hoja na yeye atatumia dakika zisizozidi dakika 60. Mheshimiwa Naibu Waziri, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimwia Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia katika hoja iliyoko mbele yetu.

Lakini kwanza niseme tu kwamba kama Wizara, tumepokea mapendekezo na michango ya Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia na kama atakavyoeleza baadaye Mheshimiwa Waziri, tutafanyia kazi katika mchakato mzima wa kutekeleza Sheria hii kama itakuwa imepitishwa. Nitajibu baadhi ya maswali na maoni ya Wabunge na Mheshimiwa Waziri atakamilisha kwa kujibu mengine ambayo nitakuwa sikuyajibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nianze kwa kusema kwamba asubuhi kulitolewa Jedwali la Marekebisho au *Schedule of Amendments,* na kama Waheshimiwa Wabunge wangelipitia kwa makini Jedwali hilo, kuna baadhi ya mengine yalijitokeza ambayo tayari tumeshayarekebisha. Kwa mfano, Mheshimiwa Felista A. Bura na Mheshimiwa Peter J. Serukamba, kuhusu masuala ya muda wa Bodi au ajira ya Katibu wa Mfuko na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Saverina Mwijage wa Viti Maalum, akichangia kwa maandishi, alisema Wizara ni vyema ikambuka sehemu ambazo Mawasiliano ni shida sana na akatoa mfano wa Biharamulo, kwenda Muleba na Karagwe ambapo huwa kuna matukio mengi ya ujambazi, sasa mawasiliano yasipokuwepo huwa ni hatari.

Tunasema kwamba ushauri huu, tumeuzingatia, huu ni wakati wa utekelezaji na kwa kweli ndio madhumuni ya mfuko huu, kwamba tulenge katika maeneo ambayo ni ya Vijijini na hayafiki kwa Mawasiliano kwa urahisi.

Mheshimiwa Fatuma Mikidati, vile vile alizungumzia suala la kupeleka mawasiliano katika Wilaya ambazo hazina mawasiliano kabisa za simu za mkononi na Posta na alitoa mfano wa Ruangwa. Bila shaka na Nachingwea kule katika Wilaya ya Lindi na sisi tunakubaliana na hilo kwa sababu mimi mwanzoni mwaka huu nilitembelea Wilaya hizo nikakuta bado simu ni zile za kukoroga. Kwa hiyo, ninakubaliana naye sana. Nina hakika mipango ile ya kuweka simu za kisasa juhudi zile zinaendelea. Vigezo vitawekwa kwa kweli katika kuangalia *priority* kwamba tuanzie wapi na hii aliyoisema ni mojawapo ya *priority* zitakazoangaliwa.

Mheshimiwa Victor Mwambalaswa - Mbunge wa Lupa, naye kwa kweli hakuwa mbali katika mchango wake, kulingana na hawa ambao nimeshawataja, naye alipochangia kwa maandishi, alitaka Wizara ifanye upembuzi yakinifu au upembuzi wa kujua ni zipi hasa *under served areas* na tuweka *priority* sasa za kuhudumia maeneo hayo kwa kutambua hiyo *priority.* Tunakubaliana na ushauri huu na kama nilivyosema awali, tayari kazi hii ya kutambua *under served areas* kwa kweli imeshafanywa. Lakini kadri tunavyoendelea kutekeleza sheria tutaendelea kuangalia hizo *priorities.* Akasema ya kwamba mfuko uwe makini na hawa *private operators* ambao tutawapa ruzuku kwa ajili ya kupeleka huduma hii Vijijini. Tunasema kwamba utaratibu utawekwa wa namna ya kulitambua kwamba ni eneo gani lianze kupata huduma hiyo. Lakini vile vile kwa sababu tutakuwa tunabaini eneo hilo hilo ambalo ndiyo *under served,* hatutawaachia tu hao *operators* ndiyo waamue. Tayari sisi au mfuko utakuwa umebaini kwamba ni maeneo gani yanayohitaji huduma hiyo kwa haraka zaidi na wao kama *operators* itawalazimu kupeleka *services* huko ambako mfuko utakuwa umeamua.

Mheshimiwa Mwambalaswa, aliendelea kuitaka Wizara kuwa makini sana katika kusimamia na kazi za Mfuko huu, kwani kutengeneza mipango mizuri na kutunga sheria moja. Lakini utekelezaji wa Mipango ni jambo lingine. Hili ni jambo ambalo ni la kawaida, ametukumbusha na tunakubaliana naye na tutaendelea kuwa makini katika kuzingatia kwamba tunapata huduma bora na kwamba tunatekeleza mipango husika kama ambavyo imeainishwa.

Mheshimiwa Prof. Idris Ali Mtulia naye alipochangia kwa kuzungumza aliipongeza Wizara kwa kuleta Muswada huu ambao alisema ni ukombozi kwa wananchi wanaoishi Vijijini na sisi tunakubaliana naye na tunapokea pongezi hizo na amesema Jimbo lake la Rufiji litafaidika sana kutokana na hali yake ilivyo na sio Rufiji tu, tunasema kwa kweli maeneo ambayo mawasiliano ni shida, kwa kweli watafaidika na Mfuko huu.

Mheshimiwa Prof. Idris Ali Mtulia aliendelea kuomba kwamba gharama za simu zipunguzwe ili wengi waweze kuzimudu. Sasa hili la gharama tunaendelea kulifuatilia kama Serikali ili kuweza kupata lile lengo la kufanikisha huduma hii kuwafikia watu walio wengi. Kwa kweli njia mojawapo ambayo tunaichukua kuhakikisha kwamba gharama za simu zinapungua ni pamoja na kuunda Mfuko huu. Amesema kipaumbele kitolewe Vijijini na hili kwa kweli limesemwa na Waheshimiwa Wabunge wengi na tunazidi kusema kwamba kwa kweli ndio vigezo ambavyo vitatumika na amesema tuanzie kwenye Kata na Makao Makuu ya Wilaya ndipo twende Vijijini. Nadhani vigezo hivyo vitatumika kama ambavyo nimeeleza hapo awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Prof. Idris Mtulia amesema pia kwamba hao wajasiriamali nadhani ndiyo hao *service providers* ambao watapewa ruzuku hiyo ili waweze kuhudumia maeneo hayo, wawe makini ili tupate faida ya fedha zetu. Mimi nakubaliana naye, nadhani ni jambo la msingi na tutahakikisha kwamba hilo linafanyika kwa makini kabisa ili kweli makusudio ya Mfuko huu yaweze kupatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshmiwa Nimrod Mkono alitoa mapendekezo mengi tu mazuri kwa mchango wake wa maandishi ambayo yalilenga katika marekebisho mbalimbali katika Muswada pamoja na mapendekezo ya namna ya kuboresha baadhi ya vifungu katika Muswada huu. Tunamshukuru kwa mapendekezo yake mazuri na yamepokelewa yatazingatiwa hasa yale ambayo yatasaidia uboreshaji wa utekelezaji wa sheria yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis naye alichangia kwa maandishi na akaipongeza Wizara kwa kuleta Muswada huu wa Huduma ya Mawasiliano, tunashukuru kwa pongezi hizo. Lakini alitoa angalizo na akaomba Muswada ukipitishwa utumike vizuri kwa maslahi ya Taifa na Wizara iwe kioo na Bodi iwe imara ili huduma ziwafikie wananchi wa hali zote, yaani wa hali ya chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunasema kwa kweli angalizo hili ni la msingi na sisi tutalizingatia wakati tunatekeleza sheria hii ili huduma hii kwa kweli iweze kuwanufaisha wananchi walio wengi hasa wale wa Vijijini na katika maeneo mengine ambayo ni *under serve the area* Mijini kama kule Chanika na Msongola katika Jimbo la Ukonga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Vuai Abdallah Khamis alisema Mfuko ukipitisha Huduma za Posta zifikishwe Vijijini na Wilayani hadi katika vitongoji na hili tunakubaliana nalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mbunge wa Ngorongoro ambaye ni Mheshimiwa Kaika Telele alitoa angalizo lake kwamba tuhakikishe kwamba Huduma hii ya Mawasiliano kweli inawafikia wananchi wote Vijijini bila upendeleo. Ushauri huu utazingatiwa na kwa hakika ndiyo lengo la Mfuko wenyewe, na akazungumzia maeneo ya wafugaji yasisahauliwe, na kwa kweli tunasema maeneo hayo yote ikiwemo Ngorongoro, Monduli, Longido, Simanjiro na Kiteto yatahudumiwa na Mfuko huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Susan Lyimo alizungumzia gharama za simu Tanzania kuwa kubwa mno ikilinganishwa na nchi za *COMESA* na zile zilizoendelea kama Marekani na sisi tunasema ni kweli gharama za simu ni kubwa, ndiyo maana Serikali inachukua hatua mbalimbali. Kwa mfano, kuanzishwa kwa Mfuko huu ni katika juhudi za kupunguza gharama hizo za simu na vilevile kujenga mkondo wa Taifa wa Mawasiliano *ICT back bone* vilevile inajielekeza katika kupunguza gharama za simu. Aliendelea Mheshimiwa Susan Lyimo kuzungumza kwamba mawasiliano ya simu, *Radio, TV* na *Computer* yaende sambamba na kuweka umeme Vijijini kwa sababu Vijiji vingi katika Tanzania havina umeme. Kwa hiyo, mawasiliano yakipelekwa huko yatatekelezwaje bila umeme?

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba ni sahihi na ni vyema juhudi za kupeleka umeme Vijijini ziende sambamba na upelekaji wa Huduma za Mawasiliano. Hata hivyo, chini ya usimamizi wa Wizara ya Nishati na Madini juhudi za kupeleka umeme Vijijini zinaendelea na nina hakika Waheshimiwa Wabunge watakuwa mashahidi kwamba ule mpango mkubwa wa *Energy Rural Transformation* utaweza kwenda

sambamba na Mfuko huu na kwa hiyo, Mfuko utapata makusudio yake kama itakwenda sambamba na Mpango ule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Susan Lyimo ameuliza kwa nini Mwenyekiti wa Bodi wa Mfuko hateuliwi na Mheshimiwa Rais na kwa nini uteuzi wa Wajumbe hauna Mwakilishi Mbunge hata mmoja? Niseme tu kwamba uteuzi utafanyika kwa kuzingatia kanuni za sheria za Utumishi wa Umma mwaka 2003, yaani *the Public Service Regulations* 2003 ambapo kwa kweli Wenyeviti wa Bodi nyingi wameachiwa Waziri awateue pamoja na Wajumbe, ni jambo ambalo ni la kawaida. Lakini kuhusu Mbunge, nadhani sheria haifungui kwamba Mbunge hawezi kuteuliwa kwa sababu sio vyema tukaiweka kabisa kwamba Mbunge lazima awepo, tusiweke kwamba kila mtu lazima awepo tumwachie Waziri aweze kuangalia kwa mantiki nyingine nani awateue.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Susan Lyimo vilevile amesema kwamba Muswada unaelezea zaidi *accessibility* ya mawasiliano, yeye anadhani kwamba ungezungumzia *availability* ya mawasiliano. Sasa nasema kwamba dhana ya *accessibility* ni sahihi kwa sababu *availability* ya mawasiliano itakuwa na maana ikiwa wananchi wataitumia. Kwa hiyo, mimi nadhani hiyo iliyotumika ya *accessibility* bado ni sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho katika mchango wangu kama nilivyosema Mheshimiwa Waziri atakuja atoe maelezo katika michango ya Waheshimiwa Wabunge wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nigusie tu suala la Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda ambaye naye alizungumzia suala nzima la kufikisha huduma Vijijini na hasa katika maeneo yaliyosahaulika. Kwa kauli yake ameseme Chunya imesahaulika na akanitaja mimi kwamba nilikwenda huko na nilishuhudia ni kweli kwamba nilifika Chunya na kweli hali ni mbaya kimawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lile la kutopeleka Makao Makuu Mkwajuni siwezi kulijibu kwa kuwa halihusiani sana na Wizara yetu ya Miundombinu. Lakini mimi kama Milton Mahanga, nasema, kwa kweli sijui kwa nini uamuzi ule haukufanyika wa kupeleka Makao Makuu kule Mkwajuni kwa sababu na mimi niliona miundombinu iliyopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuhusu mawasiliano, niliona pale kwamba *Celtel* walikuwa wameanza kujenga mnara, nadhani hali hiyo inaendelea na tutaendelea kusisitiza wengine. Lakini kwa kweli Mfuko huu utakuwa ni mkombozi kwa maeneo kama yale ya Jimbo la Songwe kule Chunya na hata Jimbo la Lupa katika Wilaya hiyo ya Chunya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, nimalizie tena kwa kusema kwamba ninaunga mkono Muswada huu. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii jioni ili niweze kuhitimisha hoja ambayo nimeiwasilisha

asubuhi hii. Nianze kwa kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao mizuri na kwa kuunga mkono Muswada huu walioongea kwa kauli humu Bungeni na waliochangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu ambacho kinatoa faraja kubwa ni pale unapoona Waheshimiwa Wabunge kama viongozi wa nchi hii wanasema wanaunga mkono jitihada za Serikali katika haya mnayopendekeza kuyafanya. Tunawashukuruni sana. Sisi hilo ndiyo tunapenda kwa sababu inatupatia nguvu kwamba haya tunayoyafanya tunaungwa mkono. Tunawashukuruni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuwatambua Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia kwa maandishi. Waheshimiwa Wabunge hao ni Mheshimiwa Fatma Mikidadi, Mheshimiwa Savelina Mwijage, Mheshimiwa Nimrod Mkono, Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Mheshimiwa Prof. Idris Mtulia, Mheshimiwa Vuai Khamis, Mheshimiwa Kaika Telele, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa George Lubeleje na Mheshimiwa Mathias Chikawe - Naibu Waziri wa Katiba na Sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa kuongea hapa Bungeni, nikianza na Msemaji aliyewasilisha Taarifa ya Kamati ya Miundombinu ni Mheshimiwa Paul Kimiti na kwa upande wa Kambi ya Upinzani ni Mheshimiwa Bakari Shamis Faki. Samahani sana Mheshimiwa Bakari Faki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, niombe radhi kwa sababu kumsahau Mheshimiwa Bakari Faki, mtu ambaye ninafahamu siyo kitu kizuri. Nashukuru sana. Waheshimiwa Wabunge wengine ni Mheshimiwa Prof. Idris Mtulia, Mheshimiwa Margreth Mkanga, Mheshimiwa Prof. Raphael Mwalyosi, Mheshimiwa Balozi Hamis Kagasheki, Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mheshimiwa Luhaga Mpina, Mheshimiwa Dr. Guido Sigonda, Mheshimiwa Felister Bura, Mheshimiwa Peter Serukamba, Mheshimiwa Lekule Laizer na Mheshimiwa Naibu Waziri Dr. Milton Mahanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema Naibu Waziri ambaye amenisaidia sana katika baadhi ya hoja hizi. Muswada huu unajibu hayo ambayo tayari yako katika sera zetu ambazo nimezitaja zipo sera nne na katika kila sera hizo iwe ni sera ya Posta, sera ya Utangazaji, sera ya *Technohama* utakuta kuna Ibara ambazo zinasema kupeleka Huduma za Mawasiliano Vijijini. Maana hatuwezi kujenga nchi hii kama Huduma za Mawasiliano zinakuwa katika maeneo fulani tu na maeneo ya Mijini, sasa hayo siyo maendeleo ya uwiano mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote tunafahamu wananchi walio wengi wanaishi katika maeneo ya Vijijini. Kwa hiyo, Serikali ndiyo inatekeleza haya ambayo yamo katika sera zetu. Utekelezaji wa kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Huduma za Mawasiliano ni njia kama nilivyosema ya kutekeleza malengo yaliyomo katika *MKUKUTA* katika kupambana na umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatekeleza Dira ya Taifa ya Maendeleo, yaani *the National Development Vision* 2025 na pia tunatekeleza malengo ya Maendeleo ya *Millennium* ya Umoja wa Mataifa ya kusema kwamba ifikapo mwaka 2015 hali ya umaskini duniani hasa Vijijini angalau tuwe tumeipunguza. Haya ndiyo malengo ambayo tunataka tuyafikie. Katika kufanya hivyo, tunataka tujenge jamii habari, jamii yenye uelewa wa mambo yanayoendelea nchini na yanayoendelea duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mazingira ya uchumi wa soko, jamii inaweza ikatumia huduma za mawasiliano kama ilivyoelezwa na Waheshimiwa Wabunge wengi hapa walipokuwa wanachangia kuweza kupata masoko, biashara, elimu, huduma za afya, bei ya mazao na pembejeo, ukajua hali ya hewa, taarifa za utalii na unataka kusafiri kwenda Mwanza, hali ya njia ikoje, wana-anga wanataka wafahamu.

Sasa yote haya katika dunia ya leo tunapoongelea jamii habari maana yake ndiyo hiyo. Sasa hatuwezi kuwa na jamii habari katika sehemu chache tu za nchi yetu. Hilo nimeona niliseme kwa sababu ndiyo la msingi sana katika *thrust* ya mapendekezo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niishukuru sana Kamati ya Miundombinu, wametoa ushauri mzuri sana na maagizo katika maeneo fulani fulani ambayo ni ya msingi.

Tunawashukuru sana, wamesema kwa wazi kabisa, miundombinu itolewe kwa gharama nafuu ili kumpatia nafuu mtumiaji na hii ndiyo imekuwa *carrying theme* kwa wachangiaji wengi iwe kwa michango kwa maandishi na kwa wale ambao wameongea humu Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imesema Mfuko wa Mawasiliano uanzishwe haraka sambamba na uteuzi wa Bodi ya Mfuko, ni sawa kabisa. Sisi haya ndiyo tunataka, lakini lazima Sheria hii Bunge liipitishe na ndiyo maana tunaliomba Bunge lipitishe na Mheshimiwa Rais akubali Muswada huu aweke saini yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kubwa zaidi ni kwamba ili misingi iliyomo katika Sheria hii iweze kufanya kazi vizuri, tunahitaji sasa zile kanuni ambazo zinaandaliwa kuweza kutekeleza haya ambayo yamo. Kwa hiyo, tunashukuru sana kwa ushauri huo. Kamati imeendelea kusema wamiliki wa miundombinu waelezwe wajibu wao wa sheria, wakikiuka wachukuliwe hatua. Sawa kabisa! Wadau wengi washirikishwe kuandaa kanuni za Mfuko, sawa kabisa. Meneja wa Mfuko awajibike kwa Bodi ili kuondoa utata na migongano, sawa kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini napenda hapa hapa niseme moja, maana wameligusia sana katika taarifa yao. Napenda tu nitoe maelezo kidogo tu kuhusiana na uanzishwaji wa mgongo wa Taifa wa Mawasiliano, *National Back Bone* ya *ICT* hii *network* yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tathmini ya mradi huu tayari imefanywa na Mgongo unakuwa na urefu wa kilomita 6,000 na ni kusudio kwamba uunganishe Miji

yetu Makao  Makuu ya Wilaya zetu nchini kote. Hiyo ndiyo dhana. Kiasi cha fedha ambacho kinatarajiwa kitakuwa  ni *dollar* za Marekani milioni 200 sio fedha kidogo hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini maendeleo yana  gharama na kama Serikali tunaamini kwa kushirikiana na hao washiriki wetu wa maendeleo, baadhi yao wameonyesha nia ya kushirikiana na Serikali katika hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo hapa ni kuunganisha kwa undani lakini pia tunataka kuboresha mawasiliano, siyo ya ndani tu, lakini pia mawasiliano na nchi nyingine duniani, nchi jirani *in Africa* na nje ya Afrika na hii ndiyo kama ilivyoelezwa na Serikali humu Bungeni, kuna ule Mpango wa *Eastern African Submarine Cable System* ambayo itatoka *South Durban* unaambaa kwenye bahari ya hindi inafika Dar es Salaam, Zanzibar inaendelea kwenda Kenya mpaka *Egypt*.

Sasa huo ndiyo mtandao ambao tunataka kuujenga na tunaamini tutakapofanikiwa kuwa na mtandao huo baadhi ya gharama hizi zinazotozwa na watoa huduma hizi zitaanza kuteremka.  Ndiyo shabaha  ya Serikali kwamba hilo tuendelee kulifanyia kazi kwa haraka. Serikali ilifanya *commission*, wataalam wa kufanya hili naona watu wa *World Bank,* wananitafuta, taarifa  hii iko tayari na tungependa tuone wote kwamba tuna mtazamo mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mathias Chikawe, amesema Nachingwea wanaomba simu za kisasa, bado wanatumia simu za kukoronga na huduma za *internet* kule kwao ni ndoto bwana.  Mimi nasema hayo ndiyo tunayotaka tuhangaike nayo kwa sababu haiwezekani ukanda fulani  wa nchi yetu ukawa na huduma, lakini katika maeneo mengine ya nchi yetu hayana huduma kama hizo.  *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hao  watoto wa Nachingwea na vijana wetu wanaosoma tunataka na wenyewe wapate huduma zile zile, ujanja ujanja wa kuchezea hii teknolojia ya leo.  Mimi zamani nilidhani kwamba haya ni mambo magumu sana, hapana. Hao watoto wakianza nayo wakiwa wadogo wala hakuna tatizo, watayamudu mpaka wewe uliye na *Ph.D* huwezi kuwafikia wale.  Lakini ndiyo maana nimesema lazima tuonyeshe *equitable distribution* ya *ICT* katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Mathias Chikawe namshukuru kwa hayo  aliyoyasema, lakini nadhani amewasemea na wengine ambao hawawezi kuyasema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niunganishe tu, ni kweli amelisemea Mheshimiwa Peter Serukamba na wengine, lakini unakwendaje Vijijini kama umeme haupo.  Sasa ndio tunasema tunao huu mradi ambao *fund* yake  mliidhinisha juzi hapa *Energy Rural Transformation*, umeme Vijijini na Wizara ya Nishati na Madini wamelifanyia kazi kweli kweli hasa ni sawa na hii, lazima ianze na upembuzi yakinifu, unaweza ukafanya uchunguzi wa kwanza ambao ulifanyika.

Sisi tumelifanya hili, lakini tutarudia tena kwa sababu tunataka tuwe na uhakika unaanzia wapi na ndiyo kifungu cha sita cha Muswada huu ukikisoma kinaeleza hilo, *formula*r ambayo itawekwa ya kuweza ku-*identify* maeneo hayo. Lakini kanuni sasa tunataka zije zifafanue zaidi utaratibu ambao utatumika katika kuyatambua maneno ambayo ni *under served* ya Vijijini, lakini vilevile na maeneo ya Mijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashirikiana kwa karibu sana na wenzetu wa Wizara ya Nishati na Madini kwa sababu hili tunataka tulifanikishe kwa pamoja. Umeme peke yake bila jamii habari bado haujafanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu masuala ya Mheshimiwa Felister Bura, mengi amenisaidia Naibu Waziri wangu, inawezekana ilikuwa bahati mbaya alikuwa hajapata *schedule of amendments*, lakini nadhani yameelezwa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kulikuwa na ushauri sasa kwa upande wa Kambi ya Upinzani, wamesema Mfuko usije ukawa mzigo kwa wananchi walio wengi wa Vijijini ambao hali yao kiuchumi sio nzuri. Tunakubaliana na ndio lengo la hili. Tunakubaliana kabisa na ushauri huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko haulengi kupata fedha kutoka kwa walipa kodi, hapana. Vyanzo vya mapato ya chombo hiki tumevitaja *levy*, tozo, Taasisi ambazo zitapenda kutupia katika kapu la kusaidia na hao washiriki wetu, yaani wadau wetu wa maendeleo, baadhi yao wako tayari sana kutuunga mkono, lakini bajeti ya Serikali, Serikali haiwezi ikasimama kando ikasema mje nyie mfanye, hapana. Ni jukumu letu kama Serikali kuhakikisha tunavutia wengine waone umuhimu wa kutusaidia katika eneo hilo. Kwa hiyo, lengo ni kumpunguzia mwananchi mzigo, sio kumwongezea mzigo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwepo na *implementation* fulani ya Mfuko huo tunasema mara tu Sheria hii itakapoanza kufanya kazi lazima Bodi iandae hiyo *implementation plan,* hiyo ni lazima, *otherwise* itakuwa ni ubabaishaji tu hapo. Wizara itahakikisha kwamba hilo linafanyika. Ushauri kwa Serikali Mfuko uundwe kama Kitengo chini ya *TCRA* wamesema Uganda wamefanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uganda *approach* yao ni tofauti kidogo na ya kwetu, lakini hili suala tumelifanyia kazi kweli kweli na uamuzi wa Serikali ulikuwa ni kwamba Mfuko huu usiwe chini ya *TCRA*. Tunataka *TCRA* iendelee kutekeleza majukumu yake ya kukidhibiti, *regulatory functions* kama Sheria inavyotaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hki chombo ndicho kinadhibiti Sekta nzima ya Mawasiliano nchini na tunataka hilo walifanikishe. Kupata ratiba kamili ya Serikali kupeleka umeme Vijijini kwani ni msingi wa mawasiliano, sawa kabisa. Umeme lazima uendane na jamii habari. Kwa hiyo, *ERT* tutashirikiana nao kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya *satellite* ni gharama kubwa, mikakati itakayotumiwa kushusha gharama za utoaji wa huduma za mawasiliano kwa wananchi iandaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimelieleza hili kwamba tunataka kwa ndani tuunganishe mpaka Wilayani kwa nchi nzima na kwa nje ya Tanzania huu mkakati wa Mgongo wa Taifa ambao tutaunganisha sasa na huu wa Kimataifa ambao tunaupigania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko utaongeza uanzishaji wa matumizi ya *internet services,* kuwepo na mikakati na mipango maalumu kuwaelimisha jamii hususan vijana juu ya matumizi mazuri ya *Internet Café, TCRA* ipo na moja ya kazi yake ni kusimamia kikamilifu jukumu hilo kwa upande wa kudhibiti maadili ya utumiaji wa huduma hizo za *internet*. Sasa katika utandawazi huu, tulimsikia Mheshimiwa dada yangu Esther alilitolea maelezo suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chombo cha udhibiti kipo, wale ambao wanaonekana wanakwenda kinyume na maadili tunasema mkondo wa sheria utafanya kazi yake. Nadhani wametoa tahadhari kwamba lengo la sheria kuwa na Mfuko ni nzuri, tahadhari ichukuliwe katika kutoa fedha za *Universal Service Provider* kuhakikisha gharama za huduma zinapungua. Mfuko huu kama Muswada unavyosema utasimamiwa na Bodi ambayo itaweka kanuni na taratibu za wazi na namna matumizi na udhibiti wa fedha za Mfuko huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa amelijibu Naibu Waziri wangu, sitarudi, utaratibu wa kuunda Bodi ya Mfuko kwa mujibu wa kifungu cha saba amelijibu vizuri. Kwa hiyo, hayo ndiyo yalikuwa maoni kwa upande wa Kamati ya Miundombinu na maoni ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Felister Bura nakushukuru kwa hayo uliyoyasema, lakini Naibu Waziri wangu amenisaidia kuyajibu. Pawepo na udhibiti wa kufungua Ofisi katika Wilaya au Mkoa. Sawa, tunasema kupitia chombo cha udhibiti yaani *TCRA* kikishirikiana na Mfuko huu ambao tunaupendekeza uanzishwe utahakikisha kuwa huduma zinatolewa kwa kuzingatia sheria zilizowekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu alichangia hoja nzuri tu, lakini moja ni hii ya matatizo ya Shirika la Posta kwamba ilianzishwa bila mtaji na ina madeni mengi pamoja na jukumu la kulipa Pensheni. Serikali inayatambua yote hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini napenda tu nilitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba ni kweli Shirika hili lina matatizo ya mtaji pamoja na madeni. Lakini sasa hivi mchanganuo mzima umeshafanywa kuhusu namna ya kushughulikia matatizo haya. Sasa na mapendekezo ambayo yametokana na mchanganuo huu yako tayari na sasa yamepelekwa kwenye Mamlaka husika kwa ajili ya kutolewa maamuzi. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mohamed H. Missanga na wafanyakazi wa Shirika la Posta wawe na subira kidogo, tuko njiani kulikamilisha suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Prof. Idris Ali Mtulia alizungumzia kuwepo uchunguzi wa kina kwa watoa huduma na maeneo ya kupeleka mawasiliano

*(Pre-service survey for information gathering)* na kwamba ruzuku itolewe kwa haki na misingi ya wazi bila upendeleo. Ushauri huo tunaukubali na Mfuko utazingatia umuhimu wa kuwa na tathmini ya kubaini ni maeneo gani yapate fedha za Mfuko. Nimeanzia na kifungu cha sita kile cha Muswada, ukienda unasoma nadhani kifungu cha 10(4) cha Muswada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *part four* ya Muswada unaweza ukasema ndio mshipa wa damu wa Muswada huu na ndio kanuni sasa zitawekwa wazi ili tuweze kutekeleza misingi iliyomo katika *part four*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini ya awali tunasema imeshafanywa na bado Meneja wa Mfuko atahitaji kuendeleleza tathmini kila wakati. Kwa hiyo, tathmini hizi zitakuwa endelevu na tunasema Mfuko utaainisha kwa kufanya upembezi ili kuwa na kumbu kumbu sahihi za uhitaji na upatikanaji huduma kuwezesha usimamizi sahihi na wa haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dr. Guido G. Sigonda, amezungumzia wasiwasi katika utekelezaji wa sheria kwa kuhakikisha huduma za mawasiliano kufikishwa kwa walengwa. Lengo ndiyo hilo hilo, tunataka hao wa Vijijini ndio tuwafikie. Sasa tutaweka zile taratibu na kanuni mbalimbali kama Wizara, *TICRA* na Mfuko wenyewe kuhakikisha madhumuni ya malengo haya yanafikiwa na tutakuwa tunafanya hizi *periodical reviews* ili kuhuisha pale ambapo tunaona kuna matatizo, tunasema tuyanyooshe hayo matatizo kwa lengo lile lile tuwafikie walio wengi na kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Margreth A. Mkanga kwa kuwasemea vizuri sana hili kundi maalum la walemavu nchini. Tunakushukuru sana na ndiyo maana Muswada na wenyewe una sura hiyo hiyo ya kutambua hilo. Tutajitahidi kwa kadri ya uwezo wetu tuyafanye hayo katika ushauri alioutoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mfuko kuangalia mazingira ya walemavu na wazee katika utoaji huduma, sawa kabisa! Jukumu mojawapo la Mfuko ni kuhakikisha kwamba huduma zinatolewa kwa kuzingatia mahitaji halisi na hali za watumiaji wakiwemo wazee na walemavu. Hilo ndio suala la msingi. Hii itakuwa ni pamoja kuwezesha kuwepo mazingira na vifaa, kwa mfano alisema kwamba hizi simu za kisasa, nyingine hazina vile vibonyezo ambavyo mtu ambaye haoni anapenda tu apapase, anajua hiki ni nini.

Kwa vifaa vitakavyoletwa kwa upande wa simu, siwezi kujibu hoja aliyoisema. Kwa upande wa *TV*, watangazaji hawa watafsiri wawepo kutafsiri ile *content,* maana hii ndiyo sheria ya *broadcasting* kwa maana ya eneo hili, ndio unakuta haya. Tuhakikishe kwamba wanakuwepo watafsiri wa ishara kwenye *TV* kuwezesha watu wote kupata mawasiliano na kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Prof. Raphael B. Mwalyosi kama kawaida yake *professional*, katoa mchango mzuri tu. Mawasiliano ni ya muhimu na lazima katika

nyanja zote za maendeleo, *perfect* hatuna tatizo na hili. Ila kasema ifanyike *regulatory impact assessment* juu ya manufaa na athari za Muswada. Kwanza, niseme moja, tunakubaliana naye kidhana, huwezi uka-*quarrel* na ushauri huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa *whether* tuanzie na Muswada huu, maana sasa hivi niko Bungeni mbele ya Bunge lako Tukufu. Lakini ni vitu ambavyo tungelipenda tuvichukue, ni usahauri mzuri tuone jinsi gani tunavyoweza kutumia ukatunufaisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nikushukuru sana kwa sababu njia moja ambayo inasaidia sana kuboresha Miswada hii ni utaratibu ambao Bunge lako limeanzisha kwa Miswada mingi ya *Public Hearing*, maana hapa ndio unawashirikisha wadau wenye sekta, walengwa wanaoguswa na hiki wanayasema kwamba mkienda hivi, mtapata matatizo na sababu zetu ni hizi na hizi na hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ambalo mimi nasema ni zuri sana, maelekezo ya Serikali kwamba Miswada ya Mkutano ujao wa Bunge inasomwa mara ya kwanza katika Mkutano huu na hiyo inawezesha Miswada hii kuwapa Waheshimiwa Wabunge na wadau wengine nafasi ya kutosha kabisa kuweza kuboresha Miswada inayopendekezwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, yote haya tukiyatekeleza vizuri, mimi naamini tutakwenda vizuri na kuhakikisha kwamba tunakuwa na Miswada ambayo imefanyiwa kazi vizuri. Lakini hii haimaanishi kwamba pendekezo la Mheshimiwa Prof. Raphael B. Mwalyosi kwamba siyo zuri, hapana! Lakini nasema namna ya kuli-*fit* na namna ya kuliboresha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa sheria, maana unaposema athari ni kwamba yawezekana zikawepo sheria ambazo hamkuzingatia katika kuandaa Muswada huu. Hilo napenda nikuhakikishie kabisa, maandalizi ya Muswada huu yamezingatia kwamba zipo sheria nyingine zinazoongelea na kuweka utaratibu kwa suala hili la huduma za mawasiliano, ndio maana Sheria Na. 12 ya 2003 ya *TICRA* tumeitaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia tunafahamu, tuna *MKUKUTA* kama nilivyowaeleza, tuna malengo ya Milenia na tuna *Vision 2025*. Yote haya ndiyo yanayotuongoza kuangalia faida ya kuelekea huko tunakotaka kwenda. Lakini kama nilivyosema, tunamshukuru sana kwa ushauri wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Luhaga J. Mpina amezungumzia *Celtel*. Niseme kwamba, sisi ni majirani, Meatu na Bariadi ni sehemu moja. Kijiografia, hii ni mipaka tu ya kiutawala. Watu ni wale wale, mila ni zile zile, ni ndugu wote wale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sasa kwa tatizo lake hili, ni tatizo langu mimi pia. Lakini napenda nimhakikishie kwamba kwa taarifa tuliyopata leo saa 9.10 adhuhuri, kutoka *Celtel*, wao wenyewe wamesema Mheshimiwa Chenge ni kweli tunakubali pamekuwepo na tatizo kidogo la mawasiliano katika eneo la Meatu. Lakini

wamesema wamechukua hatua za kuongeza mnara mwingine ili kuhakikisha mawasiliano yanakuwa mazuri na yanaimarika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kupitia kwako namwomba tu Mheshimiwa Luhaga J. Mpina, iwapo yataendelea kuwepo matatizo, mimi nipo, tushauriane kwa haraka. Lakini ningependa wananchi wa Wilaya ya Meatu kama ninavyopenda kwa wananchi wa maeneo mengine, nchi nzima waweze kupata huduma bora na ya uhakika ya simu na pia kwa upana huduma za mawasiliano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Balozi Hamis Sued Kagasheki na eneo hili pia Mheshimiwa Dr. Guido G. Sigonga naye alilisemea. Yapo mambo ya msingi ambayo tunapaswa kwanza tuyatazame, waliyaelezea vizuri tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunaamini katika kuleta Muswada huu mbele ya Bunge lako hili, ni wazi kabisa kwamba nia ya Serikali ni kutaka tuone kwamba panakuwa na ukakamavu katika kutekeleza sera zake. Lakini ukakamvu huo, tuhakikishe kwamba tunajipanga vizuri ili tuutekeleze kikamilifu. Tunapokea ushauri aliotupatia Mheshimiwa Balozi Hamis Sued Kagasheki. Pamekuwa na matatizo, ametoa mifano ya *TTCL* katika Mkataba na Mwekezaji ilikuwa waweke *landline* 800,000 ikaenda kuwa 80,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mengine mazuri tu amesema kukosoa, safi kabisa! Lakini kakosoa kwa nia ya kujenga. Nitakachoweza kusema ni kwamba tugange yajayo. Katika eneo hili Serikali imedhamiria kulisimamia vizuri kwa sababu *TECHNOHAMA* ndiyo tunataka kweli kweli tuifanyie kazi lakini tuwafikie hao ambao ni wengi zaidi katika maeneo ya vijijini na mijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kitu kimoja alitoa mifano kwamba kwa nini sisi tuna *Operators* Service *Providers* wanne, Kenya wana wawili lakini hata ukichukua tu idadi ya *Subscribers*, tuko chini! Lakini nilisemee tu hili kwa sababu ni zuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa takwimu tulizonazo, mwaka 2001 tulikuwa na *subscribers,* yaani hawa waliokuwa *customers* wanaotumia simu, kwa upande wa *TTCL* walikuwa 177,802. Ukiwachukua sasa *Vodacom*, *mobitel*, *Zantel* na *Celtel*, *Celtel* alikuwa hajaja wakati huo, lakini wote walikuwa 453,359. Leo ninapoongea mbele ya Bunge lako Tukufu, miaka mitano baadaye, tuna *subscribers* 5,876,868. Sasa unaweza ukaona katika kipindi kidogo hicho ukilinganisha na Kenya ambao kwa takwimu ambazo wamezitoa kwamba wako milioni sita, *we are almost there*.

Lakini kubwa zaidi, tulisema tungependa ifikapo mwaka 2020, katika kila wananchi 100, *at least* wananchi sita wawe na simu. Leo mwaka 2006, katika kila wananchi 100 ni wananchi 16 wana simu. Sasa hili sio dogo, tumefanya kazi kubwa. Tunawashukuruni sana Waheshimiwa Wabunge wametuunga mkono na sera zile na utekelezaji wake. Kwa hiyo, tunaanza na kuwapiku wale ambao wao walikuwa wanaonekana wako mbele. Sasa huu ndio ukweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bei za huduma za Tanzania, kusema kweli katika wadhifa ambao mpaka juzi Mheshimiwa Rais alikuwa amenikabidhi kwa maana ya *East Africa.* Eneo hili tulikuwa tunalifuatilia kwa pamoja. Unaona kabisa bei za huduma za Tanzania zinafanana kwa karibu na zile za nchi za Afrika Mashariki hasa nikichukua Kampuni ambayo iko ndani ya nchi zetu tatu, *Celtel*, unaona kabisa ziko karibu sana. Lakini ni changamoto ambayo Mheshimiwa Balozi Hamis Sued Kagasheki ametupatia na tunaichukua, ni sehemu ya changamoto ambazo lazima kama Wizara kama Serikali tuweze kupambana nazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Peter J. Serukamba, amesema wote tumemsikia humu, ruzuku hii nini hasa? Ni yale yale maana dhamira ya Mfuko ni kuhakikisha kwamba huduma hii inawafikia walengwa kule Vijijini wote waweze kuipata fursa hiyo kwa gharama nafuu. Alisema sasa *criteria* iko wapi? Maana kifungu cha 6(e), sawa kabisa. Amekisoma vizuri kabisa. Lakini ndio tunasema, tutafafanua yote hayo kwenye kanuni na tutaziweka wazi na Waheshimiwa Wabunge kwa sababu ni Kanuni ambazo zinakuwa *laid before the table*, mtaweza kupata fursa ya kuziona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la umeme amehimiza kama walivyohimiza Waheshimiwa wabunge wengine waliochangia kwa maandishi na kwa kuzungumza kwamba umeme lazima uende sambamba na miundombinu mingine kama barabara na ndio maana tunahangaika sana na suala la *connectivity* la nchi nzima kwa maana ya barabara. Lakini, tunaposema tuboreshe miundombinu, siyo kwa maana ya mawasiliano peke yake, lakini tunaongelea barabara zetu, kwa maana ya reli. Tunaongelea usafiri wa kwenye maziwa, baharini, tunaongelea suala zima la Bandari zetu na viwanja vya ndege. Yote haya ukiyafanikisha, ndio unaona jinsi uchumi, maendeleo kwa maana ya *social* kwa jamii na kiuchumi, yanavyoibuka haraka. Kwa hiyo, yote haya tunakubaliana sana na ushauri ambao ametoa Mheshimiwa Peter J. Serukamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge amesema huduma zinazopelekwa Vijijini ni kumwezesha mkazi wa Kijiji kupiga simu kwa bei nafuu au yule *Operator*? Suala la msingi hapa ni hilo la unafuu wa huduma.

Ndiyo maana tunasema Mfuko huu ukisoma, ukisoma kile kifungu cha 10 nadhani, unaona Mfuko unaweza ukaweka *Price Caps* na hawa waombaji watatakiwa wawasilishe mapendekezo yao, maana tunataka tuwashindanishe hawa. Hatukulazimishi kwenda huko, lakini kwa sababu na sisi tunatambua kwamba ukienda huko bila kupata ruzuku, hutakubali kwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo letu hapa ni kuhakikisha kwamba huduma hiyo ifike kule kwa walengwa, wananchi, lakini kwa bei ambayo tutakuwa tumekubaliana na tunataka iwekwe *schemes*, mapendekezo iwapo yale uliyotuambia utayafanya na ukashindwa kuyafanya, hawa *customers* wako ambao wamesaini na wewe, wana mikataba, njia ya kuwafidia. Kwa hiyo, haya yote utayafafanua vizuri kwenye kanuni.

Lakini lengo tunataka *Universal Service* kwa wote, mtu aweze kuunganishwa akatumia huduma hiyo. Sasa hapa katikati yupo yule anaye-*own* ile miundombinu, anayemiliki. Lakini huyu tunamuunganisha pale na huyu naye anayeunganisha

anatawaliwa na *TICRA*. Lakini na hawa kumbukeni, hawezi mtu akajitumbukiza kufanya biashara hii bila kupewa leseni na *TICRA*. Kwa hiyo, *safe guards* ziko nyingi sana ndani *(in bult safeguards)* katika Muswada huu, lakini kama nilivyosema katika sheria nyingine, lakini muhimu zaidi katika Kanuni ambazo zitaandaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Michael L. Laizer kwa yale aliyosema. Tumechukua ushauri wake, wafugaji kama alivyosema Mheshimiwa Kaika S. Telele. Wafugaji ni sehemu ya nchi hii! Sasa hivi ninapopita barabarani kule naona rafiki zangu Wamasai, Yero, naye anayo simu hapa! Sasa, Mheshimiwa Waziri Mkuu mambo ni mazuri! Tunakwenda vizuri. *(Makofi/Kicheko)*

Kwa hiyo naelewa, tusichukie Waheshimiwa, *beeping* hasa kwa Waheshimiwa Wabunge, hali ndio hiyo! Wana-*beep* ili uwapigie wewe. Lakini tunaamini huko tunakokwenda, bei hizi zitashuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba *TICRA* ifanye kazi yake lakini na Mfuko huu, Meneja huyo na Bodi hiyo, tukiwasimamia vizuri na shabaha yetu ni kufanya hivyo, tutahakikisha kwamba wananchi wanapata huduma hii ya mawasiliano kwa bei nafuu. Hilo ndio lengo la Serikali na ndio lengo la Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo, yawezekana nikawa nimeruka sehemu moja au nyingine lakini, nadhani kwa ujumla mimi ningesema tu tuanze kutekeleza haya ambayo yamo katika Muswada huu na mimi *I am sure* kama Wanasheria wengine ambao wanayafahamu masuala haya, *you see*, maendeleo katika sheria *(The Development of the Law)* huwa haitokani na mantiki hapa, inatokana na uzoefu . Ninaamini kadri ambavyo tutakavyoanza kutumia sheria hii na kanuni ambazo zitatengenezwa, mapungufu yatakayojitokeza, Serikali itayaona na yale ambayo hayahitaji sheria ya kiutendaji tu, tunaamini yatasahihishwa, yale yanayohitaji marekebisho ya sheria, ninaamini Serikali itakuja Bungeni na Muswada wa Marekebisho ili kuimarisha azma na malengo ya Muswasda huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nawashukuruni sana Waheshimiwa Wabunge na niseme naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili)*

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**Muswada wa Sheria ya Huduma za Mawasiliano wa Mwaka 2006**
***(The Universal Communications Access Services Bill 2006)***

Ibara ya 1
Ibara ya 2

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 3

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 4
Ibara ya 5

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge zima bila Mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 6
Ibara ya 7

*(Ibara ziliyotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 8

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 9

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 10
Ibara ya 11

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 12

*(Ibara ilizotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 13
Ibara ya 14
Ibara ya 15
Ibara ya 16
Ibara ya 17

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 18

*(Ibara ilizotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 19
Ibara ya 20
Ibara ya 21
Ibara ya 22
Ibara ya 23
Ibara ya 24
Ibara ya 25
Ibara ya 26
Ibara ya 27
Ibara ya 28
Ibara ya 29
Ibara ya 30
Ibara ya 31

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge zima bila mabadiliko yoyote)*

Jedwali 1

*(Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitiswa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Mabadiliko yake)*

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Huduma za Mawasiliano wa Mwaka 2006**
***(The Universal Communications Access Services Bill 2006)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lilikaa kama Kamati ya Bunge Zima, limeupitia Muswada wa Sheria ya Huduma za Mawasiliano wa Mwaka 2006 *(The Universal Communications Services Access Bill of 2006)*, kifungu kwa kifungu na kukubali pamoja na mabadiliko yaliyofanywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Huduma za Mawasiliano wa Mwaka 2006 *(The Universal Communications Services Access Act, 2006)*, sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki!

*(Hoja ilitolewa Iamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, ninaomba sasa kuwatangazia kwamba shughuli iliyoko mbele yetu na Muswada huu wa Sheria ya Huduma za Mawasiliano wa Mawaka 2006, sasa umeishapitishwa rasmi na Bunge letu Tukufu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninalo labda tangazo dogo tu. Ninaomba kutambua kurejea kwa Waheshimiwa Wabunge ambao walituwakilisha katika mazishi ya Marehemu kaka yake na Mheshimiwa Mhonga S. Ruhwanya ambayo yamefanyika nafikiri jana na ninaona wako hapa ndani leo.

Kwa niaba yenu naomba niwashukuru kwa kutuwakilisha kwenye shughuli hiyo muhimu. Ninawakaribisha tena hapa Bungeni na ninawapa pole kwa safari na tutaendelea kumfariji mwenzetu kwa tatizo hilo la ghafla lililompata.

Waheshimiwa Wabunge, shughuli zilizokuwa zimeorodheshwa katika *Order Paper* yetu ya leo, zote zimekamilika na tumezifanyia kazi kwa umakini na tumezikamilisha zote na hatuna kitu chochote tena ambacho kiko hapa kwenye meza yangu.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo basi shughuli za leo zimekamilika na kwa maneno hayo, sasa ninaahirisha Bunge mpaka kesho saa Tatu Asubuhi.

*(Saa 12.37 jioni Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Ijumaa,*
*Tarehe 10 Novemba, 2006 Saa Tatu Asubuhi)*